RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KWANZA

JUDI alimalizia kujifunga mkufu shingoni baada ya kukamilisha
kujikwatua kwa vipodozi tofauti vya gharama huku akiwa amevaa vazi lililompendeza mwilini. Alikuwa ameamkia nyumbani kwa Richard ambako alikuja usiku uliopita na kulala hadi asubuhi hiyo. Yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kumaliza kuoga na alikuwa akimsubiri Richard amalize kuoga kisha watoke pamoja kwenye gari la Richard. Kituo chao cha kwanza kingekuwa kwenye mgahawa wa Monde uliopo katikati ya jiji
kwa ajili ya kifungua kinywa, kisha baada ya hapo, Richard angempeleka kazini kwake.
Akiwa amekaa kitandani baada ya kutoka kujiangalia kwenye kioo
kilichopo kwenye kabati la kuvalia, Judi alianza kujiuliza kama ulikuwa ni wakati mwafaka wa kumuuliza Richard kuhusu matumaini yake ya kuolewa naye. Walikuwa ndani ya uhusiano wa mapenzi kwa muda mrefu na alikuwa akijisikia fahari mbele ya wanawake wenzake kuwa na uhusiano
huo na Richard ambaye ni mtoto wa mfanyabiashara tajiri na maarufu jijini Dar es Salaam. Pamoja na kuwepo na uhusiano huo wa muda mrefu, lakini haikuwahi kutokea hata siku moja kujikuta wakizungumzia suala la kuoana.
Haikuwa ni mara yake ya kwanza kulala nyumbani kwa Richard.
Alishakuwa mwenyeji wa nyumba hiyo tokea uhusiano wao ulivyoanza na kumfikisha hadi siku hiyo. Mara nyingi, husan siku za mwishoni mwa wiki kuanzia Ijumaa hadi Jumatatu alikuwa na mazoea ya kuhamia nyumbani kwa Richard na kuumiliki umama wa mwenye nyumba kuanzia usafi hadi mapishi na mengineyo, kiasi kwamba hata nguo zake zikawa zimegawanyika sehemu mbili; baadhi zikiwa nyumbani kwao ambako aliishi na wazazi wake na nyingine zikiwa nyumbani kwa Richard.
Uhusiano wao ulifahamika hadi kwa wazazi wao na kila mmoja alikuwa amejenga uhusiano mzuri kwa upande wa wazazi wa mwenzake. Richard alikuwa na uwezo wa kwenda nyumbani kwa akina Judi na kuomba kuondoka naye kwa muda wowote. Hali kadhalika, Judi aliweza kwenda nyumbani kwa Richard kwa muda wowote alioamua. Ingawa wote walikuwa huru kuyafanya mambo hayo, lakini walikuwa wakitofautiana kimawazo. Kwa upande wa Judi, yeye alikuwa hajiamini kama alikuwa peke yake kwenye penzi la Richard. Hakujua ni kwa nini alikuwa akipatwa na
hisia hizo mara kwa mara, kuna wakati alikiri huenda ni kwa vile Richard alikuwa ni mtoto aliyezungukwa na utajiri wa baba yake na mwonekano wake kumvutia msichana mwingine yeyote kutaka awe naye!
Wivu! Hilo ndilo lililokuwa likimsumbua na kumwingiza kwenye
wasiwasi huo. Alikiri dhana hiyo ya wivu ndio iliyokuwa ikiisumbua
nafsi yake na kumjengea woga kuwa, Robert alikuwa na wanawake wa nje! Pamoja na kuwa na hisia za aina hizo, lakini hakuwahi kumfumania na mwanamke mwingine japo mara moja!

Kwa upande wa Richard, yeye mawazo yake yalikuwa yakikinzana
kimkabala na mawazo ya Judi. Yeye alikuwa akiamini Judi alikuwa
hana mwanamume mwingine zaidi yake kutokana na uaminifu aliokuwa nao Judi. Pamoja na kuwa na mitazamo tofauti kati yao, ajabu ni kwamba, hakuna hata mmoja aliyediriki kuzizungumza hisia hizo kwa mwenzake.
Mahusiano yao ya muda mrefu yaliwawezesha kuwajengea mazoea ya kuzoeana, wakawa na uhuru kwa kila mmoja kwenda kwa mwenzake kwa muda wowote na wakati mwingine bila hata ya kutaarifiana. Uhuru

huo ulimfanya Judi na wazazi wa pande zote mbili kuamini kuwa, suala la ufungaji wa ndoa kati yao lilikuwa lipo njiani na lingetangazwa wakati wowote. Lakini kama ilivyo ada kwa tamaduni za Kiafrika, mwanamume ndiye aliyepewa jukumu la kutamka dhamira hiyo, Judi akaamini, ipo siku Richard angekuja kulitamka jambo hilo kwake.
Richard hakufanya hivyo! Na Judi naye akashindwa kuvumilia!
Ndipo asubuhi hiyo, Judi alipoamua iwe siku ya kuuvunja ukimya
huo!

* * * * *

Richard alitoka kuoga na kuingia chumbani. Kitendo cha kufunguliwa kwa mlango wa maliwatoni ambayo ilikuwa imo humo humo chumbani, ile hali ya kutoka kuoga aliyokuwa nayo Richard na kufunguliwa kwa mlango huo kulisababisha harufu ya sabuni ya kuogea iingie chumbani humo, lakini ilichukua sekunde chache harufu hiyo kumezwa na manukato yenye harufu ya nuni yaliyokuwa yamepulizwa mwilini na kwenye nguo alizovaa Judi.
Judi akaanza kumpigia mahesabu Richard aliyekuwa ameanza kuvaa nguo ya ndani na kisha akamwona akivaa suruali aliyoitoa kwenye kining'inizo cha kuwekea nguo kwa kutumbukiza mguu mmoja baada ya mwingine kwenye suruali hiyo. Judi akashusha pumzi kwa nguvu bila ya kutarajia. Hali hiyo ilimjia baada ya kugundua jambo alilokuwa anataka kulizungumza kwa Richard lilikuwa na uzito mkubwa kwenye mustakabali wa maisha yake ya baadaye.
Hali ya utambuzi wa mustakabali huo ilimuweka kwenye unyonge, hata kule kujiamini kuwa yeye ndiye mwenye nafasi ya kuolewa na Richard, ghafla kukaanza kumuweka kwenye njia panda. Hofu hiyo ikamuweka kwenye mizani kwa kuzivuta kumbukumbu za matukio kwa kipindi chote alichokuwa na Richard, ikawa kama vile anajifanyia usaili utakaomwezesha kumpa moyo wa kuendelea na dhamira yake aliyoidhamiria; dhamira ya kulizungumza suala la ndoa kwa Richard!
Aliyakumbuka matukio mengi mazuri yaliyoonyesha upenzi kati yao; kama vile kununuliwa vito na nguo za thamani kwenye maduka yanaouza bidhaa hizo kwa bei ghali; kutoka pamoja kwa ajili ya kula chakula cha usiku kwenye hoteli za kifahari au migahawa ya Kimataifa; kuhudhuria
kwa pamoja mialiko tofauti ya sherehe walizokuwa wakialikwa au wakati mwingine kufurahisha nyoyo zao kwa kwenda kwenye mahoteli yaliyopo nje ya jiji la Dar es Salaam au kwenye majumba tofauti ya starehe.
Ujumla wa kuyakumbuka matukio hayo ulimfanya ajione ni nembo
maalumu ya Richard na kuamini kuwa, ni yeye ndiye aliyechaguliwa!
Lakini pia, pamoja na kuyakumbuka mazuri yote yaliyofanyika kati yao, pia aliikumbuka mizozo waliyokuwa wakizozana kwa mambo madogo. Kama vile kukasirikiana kutokana na maudhi yaliyokuwa yakisababishwa na vijijambo vya kipuuzi, wakati mwingine kuwafikisha kununiana kwa saa kadhaa au zaidi ya hivyo.
Baadhi ya matukio waliyoudhiana waliweza kuombana misamaha,
lakini pia kuna baadhi yaliyowafanya wasiombane misamaha kwa sababu kila mmoja alijiona ana haki ya kuvuta kamba upande wake. Mizozo ambayo hakuwakuombana misamaha iliweza kumalizika kimya kimya na kuwa kama vile hakukuwepo na mtafaruku uliotokea kati yao.
Alipoyaweka kwenye mizani matukio hayo, mengi yakawa ni mazuri na zile kasoro chache zilizokuwa zikijitokeza, akazichukulia ni sehemu ya kawaida kwa binadamu wanaoishi kwa karibu. Ukweli huo ukamuweka Judi kwenye imani aliyoikubali kuwa, walikuwa wakipendana kwa dhati.

Akajiona yupo kwenye nafasi kubwa ya kuolewa na Richard!

Hali hiyo ikamrejeshea nguvu ya kuitupa karata yake juu ya meza!
“Richie,” Judi aliita. Alikuwa amezoea kumwita Richard kwa jina hilo.
Richard aliyekuwa amesimama mkabala na kioo kilichopo kwenye
kabati la kuvalia akiwa anazichana nywele zake, aligeuka na kuitikia huku akimwangalia Judi aliyekuwa bado amekaa kitandani.
“Kuna jambo nataka nikuulize,” Judi alisema huku akijaribu
kuyatuliza macho yake kumwangalia Richard usoni na wakati mwingine kuyakwepesha.
Richard alishitushwa na kauli hiyo baada ya kugundua Judi alikuwa
amekosa utulivu usoni mwake wakati akiitamka. Akahisi kulikuwa na tatizo!
“Jambo gani?” Richard aliuliza huku akiwa ameganda na kitana chake mkononi.
“Una mpango wowote wa kunioa?”
Richard alionekana kama aliyesukumiwa ngumi ya ghafla iliyotua
usoni mwake! Akiwa ameishiwa nguvu ghafla baada ya kupigwa swali hilo, alijikokota kwa kujisogeza taratibu hadi kwenye kabati la kuvalia, akaliegemea. Uso wake ulikuwa umepigwa na tahayari iliyomwonyesha kuwa, alikuwa akihaha kulitafuta jibu. Macho yake yalishindwa kuyakabili macho ya Judi yaliyokuwa yakimwangalia. Akaiangalia sakafu iliyojengwa kwa marumaru kama vile eneo hilo ndilo lingetoa majibu ya swali alilokuwa ameulizwa.
Ukimya uliofanywa na Richard ukaanza kumchanganya Judi. Akili
yake ilianza kukataa kuamini kile anachokishuhudia kutoka kwa Richard.
Richard alikuwa akionekana kupata kigugumizi kulijibu swali ambalo lingehitimisha ndoto ya Judi; ndoto ya kuolewa!
“Mbona hunijibu?” Judi aliuliza huku sauti yake ikionyesha
ukakamavu wa kutaka ajibiwe, lakini moyo wake ukisambaratika kwa maumivu yaliyoanza kumkatisha tamaa. Woga na hofu ya kupewa jibu litakalomwumiza vikawa vinaitafuna nafsi yake, hali hiyo ikauweka moyo wake kwenye mapigo ya kasi yaliyotishia uhai wake!
Richard alianza kwa kupiga kite na kushusha pumzi huku uso wake
ukiwa bado unaangalia sakafuni.
“Hapana Judi!” Richard alijibu kama vile alikuwa akiongea na sakafu aliyokuwa akiitazama. Kisha akauinua uso wake kumwangalia Judi. “Sina mpango wowote wa kukuoa!” alimalizia.
“Yesu wangu!” Judi alinong’ona peke yake na kuishiwa nguvu huku
akiwa amefumba macho.
“Najua haitokuwa rahisi…” Richard alianza kuutetea uamuzi wake.
Judi akawahi kumnyooshea mkono Richard kumzuia asiendelee
kuzungumza.
Kimya kikapita kati yao.
Judi akashusha pumzi kwa nguvu akiwa bado amefumba macho. “Uko serious na jibu lako?” aliuliza.
Richard akaonekana kuwa kwenye wakati mgumu, lakini pamoja na kuwa kwenye hali hiyo, bado alikusudia kuwa kwenye msitari wa ukweli.
“Ndiyo! Niko serious!” Richard alisema.
Judi akanywea, kila kiungo chake cha mwili kikaonekana kama
kimekataa kufanya kazi! Akatulia pale kitandani alipokuwa. Ghafla
akalikumbuka tukio la kufanya mapenzi na Richard saa chache zilizopita baada ya kurudi kutoka disko kabla hawajalala na kuamka asubuhi hiyo.
Halikuwa tukio geni kwao, lakini tukio hilo la saa chache zilizopita likawa kama tukio pekee katika maisha yake na Richard lililompa picha halisi jinsi Richard alivyokuwa akimchezea katika maisha ya ngono

walizokuwa wakizifanya huku yeye akiamini kwa imani zote kuwa, ilikuwa ni njia ya kuelekea kwenye kufunga ndoa!
Lilikuwa pigo kwenye maisha yake! Aliusikia moyo wake ukikatika
pande mbili kwa maumivu makali aliyokuwa hajawahi kukumbana
nayo. Alihisi kama anayeelekea kuzirai, akajaribu kupambana na hali hiyo isimtokee akiwa ndani ya nyumba hiyo ambayo sasa ilishakuwa ni nyumba asiyotaka aendelee kuwemo tena. Akamudu kuizuia hali hiyo, lakini akashitukizwa na tukio jingine ambalo laiti angepatwa na hisia za mapema kuwa lilikuwa njiani kumtokea, kamwe asingeweza kuliruhusu limtokee mbele ya Richard; Richard alishakuwa Shetani mbele yake!
Yalikuwa machozi aliyoshindwa kuyazuia!
Kitu kikaja kumbana kooni na kumwanzishia kilio chenye kwikwi
iliyomuweka kwenye kilele cha majuto! Richard akamsogelea na kumshika maungoni ili ambembeleze, Judi akaupangua kwa nguvu mkono wa Richard usimshike!
“Tafadhali usinishike!” Judi alisema kwa sauti yenye chuki iliyotawaliwa na hasira zilizokuwa katikati ya kilio.
Kuanzia siku hiyo uhusiano wao ukawa umeingia doa!

*****

JOHN Sailas akiwa varandani mwa nyumba anayoishi yenye chumba kimoja cha kulalia, varanda moja, jiko na choo ambayo alipanga, alitengeneza tabasamu dogo mdomoni mwake wakati akiisoma barua iliyoletwa na mshenga wake iliyokuwa imejibu barua yake ya uchumba aliomchumbia rafiki yake wa kike anayeitwa Dina siku kadhaa zilizopita.
Barua aliyokuwa akiisoma ilikuwa ikielezea jinsi alivyokubaliwa uchumba wake na tabasamu alilokuwa amelijenga lilikuja baada ya kusoma masharti yaliyokuwa yanahitaji yatimizwe siku itakayopelekwa mahari. Baadhi ya masharti aliyaona kama aina ya mzaha unaochekesha.
Kukubaliwa kwake kumuoa Dina alikutarajia kwa sababu alikwisha
kuizungumza nia yake hiyo kwa mwenyewe Dina, wakakubaliana na ndipo alipomtuma mshenga kuipeleka posa hiyo. Lakini pia, hata kabla ya kulizungumza hilo, uhusiano wao wa mapenzi uliokwishadumu kwa zaidi ya mwaka mmoja, nao ulikuwa ukifahamika na wazazi wa Dina, hali kadhalika na wazazi wake mwenyewe. Pamoja ya kuwa mila za Kiafrika huwa zinawaweka mbali mtu na mkwewe, lakini uhusiano wake na Dina
uliweza kumuweka karibu na mama mkwe wake kiasi kwamba kukawa na urafiki fulani ulioongezea aina ya utani wa hapa na pale.
Ukaribu huo na mama mkwe wake ndio uliompa John uelewa kuwa, posa yake hiyo isingekumbana na vikwazo vyovyote. Alikuwa akijua mama yake Dina ndiye aliyekuwa na sauti ndani ya nyumba huku baba yake Dina ambaye ni mstaafu akiwa hana kauli ya kumpinga mama huyo. Mama yake Dina ambaye bado ni mwajiriwa, ndiye aliyekuwa mwendeshaji wa nyumba kwa karibu kila kitu.
John aliikunja barua aliyokuwa akiisoma na kuirudisha kwenye
bahasha, kisha akaiweka juu ya meza na yeye mwenyewe kujilaza kivivu kwenye sofa aliyoikalia. Uso wake aliuelekeza juu na kuliangalia pangaboi lililokuwa likizunguka kwa kasi ndogo. Uzungukaji wa pangaboi aliokuwa akiuangalia ilikuwa ni kama vile alikuwa akizirudisha nyuma tafakuri zake kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja uliopita kwa kuikumbuka siku ambayo yeye na Dina walionana kwa mara ya kwanza. Ilikuwa siku ya Jumamosi!
Aliikumbuka vizuri siku hiyo. Siku hiyo alikwenda eneo la Ndege Beach akiwa na pikipiki yake. Hakuwa

mgeni na eneo hilo, alikuwa na mazoea ya kwenda mara kwa mara kwa ajili ya kuogelea kutokana na fukwe ya eneo hilo kuwa ya kupendeza ukilinganisha na fukwe nyingine zilizopo Dar es Salaam kama ukiziondoa zile za eneo la Kigamboni.

Akiwa na begi lake lililobeba nguo yake ya kuogelea baada ya kufika kwenye fukwe hiyo, alilitua begi juu ya mchanga mweupe hatua chache
kutoka baharini. Aliwaangalia kwa sekunde chache watu waliokuwa
wakiogelea kwenye bahari ambayo haikuwa na mawimbi makubwa kwa siku hiyo. Kisha aliinama tena, akalifungua begi lake na kutoa bukta aliyoiandaa kuogelea nayo. Kabla ya kuivaa bukta hiyo, alijifunga taulo kubwa iliyoziba maungo yake ya kati hadi miguuni, akaivua suruali yake ya jeans kwa kuiunganishia na chupi aliyokuwa ameivaa na kuzikunja vizuri nguo hizo kisha akaivaa bukta ya kuogelea. Baada ya kuwa kamilifu kwenye hali ya kwenda kuogelea, alizichukua nguo zake alizozivua na
kuzitia kwenye begi pamoja na ile taulo.

Badala ya kwenda kuogelea, John alikaa kwenye mchanga kando na lilipo begi lake na kuanza kuwatizama waliokuwa wakiogelea baharini.

Akavutiwa na kundi dogo la wasichana watatu, wawili wakionekana
angalau wanaweza kujaribu kuogelea na yule watatu akiwa hajui kabisa kuogelea. Msichana huyo wa tatu ndiye aliyemvutia; na si kwamba kwa vile alikuwa hajui kuogela, lakini pia alikuwa na mvuto kuliko wenzake aliokuwa nao. Msichana huyo mwenye umbo la kupendeza lenye urefu wa wastani, alipendezwa na nguo za kuogelea aina ya bikini ambayo ilimfanya John apate ushawishi wa kumkaribia msichana huyo ili amwone vizuri!

Aliendelea kumwangalia msichana huyo alivyokuwa akijilaza kwenye maji kama anayetaka kuogelea, lakini kwa kukosa ustadi wa kujua kuogelea, akawa anaishia kwenye mwelekeo wa kuzama kila alipokuwa akijaribu kuogelea. Wakati wote alipokuwa akijaribu alijikuta akiishia kupiga magoti na sura yake kuangukia majini. Kitendo hicho kilimfanya ajiinue kwa haraka kila tukio hilo lilivyofanyika na kuonyesha woga wa kuogopa kuzama huku akijifuta maji ya usoni na kuhema kwa kuacha
mdomo wazi na kuzitafuta pumzi kwa kuruka ruka kwenye maji huku akipenua macho yake. Hali hiyo ilimfanya John atabasamu peke yake.

John aliondoka alipokuwa amekaa na kuelekea kwenye maji, akaenda upande walipokuwepo wasichana hao na kumfuata yule aliyekuwa hajui kuogelea.

“Samahani,” John alimwambia yule msichana. “Una nia ya kujua
kuogelea?”

Uso wa msichana yule ukajengwa na aibu kwa kugundulika kuwa hajui kuogelea, hata hivyo aibu hiyo akaiziba kwa tabasamu lenye haya.

“Kwa jinsi unavyojaribu kuogelea, katu hutojua kuogelea,” John
aliendelea bila ya kusubiri jibu la msichana huyo. “Kwanza ni mwoga. Pili, maji hayawezi yakakuinua kwa sababu tu, unataka kuelea. Kuna mbinu za uogeleaji ambazo lazima ufundishwe ndipo utakapoweza kuogelea,” John alisema. Akakumbuka kujitambulisha. “Jina langu ni John, John Sailas.
Unaitwa..?”

Moja kwa moja macho ya msichana yule yakawaangalia wenzake
walioacha kuogelea, nao wakawa wanakuja pale aliposimama na John.

“Vipi?” mmoja wa wale wenzake wawili alimwuliza huku akijaribu
kumwangalia John kwa kutaka kujua kinachoendelea.

“Nataka kumfundisha mwenzenu namna ya kuogelea,” John alijibu
ingawa swali lililoulizwa lilikuwa halikulenga kwake.

Nyuso za mshangao zikajengwa na wasichana hao wawili na kuonyesha dhahiri hawakulitarajia jibu hilo.

Wakajikuta wakimwangalia mwenzao kama kutaka kujua ameliafiki vipi wazo hilo. Mwenzao hakujibu chochote, ukimya wake ukawajumuisha wote watatu kupigwa na ganzi ya kutojua wajibu nini kwa mtu huyo au wawili hao wamshauri vipi mwenzao.
“Nitarudi baadaye nijue mmeamuaje!” John alisema kisha alijilaza
kwenye uso wa maji na kuanza kuogelea kwa ustadi wa kukusudia
kuwaonyesha wasichana hao namna gani jinsi anavyojua kuyakata maji.
John aliogelea kwa umbali mrefu kama njia ya ushawishi kumfanya
msichana huyo endapo atakubali kufundishwa naye basi ajione atakuwa salama mikononi mwake.
John aliporudi tena kwa wale wasichana, wakakubali amfundishe
mwenzao, lakini kwa sharti kuwa hata nao walihitaji kufundishwa.
“Basi nitaanza na huyu ambaye hajui kabisa,” John alisema.
Wazo la John likakubaliwa.
Wakiwa wawili peke yao kabla ya kuanza kufundishana kuogelea, John akakumbuka kujitambulisha tena, “Jina langu ni John Sailas…”
Macho ya John na yule msichana yakaangaliana. John akauhisi moyo wake ukipiga kwa kasi. Akakijua kilichopo moyoni mwake dhidi ya msichana huyo.
“Naitwa Dina,” msichana alisema huku akionyesha tabasamu dogo
lililojificha kwa dhamira.
Ni siku ambayo John hakuisahau kamwe!

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME.

SEHEMU YA PILI

Wazo la John likakubaliwa. Wakiwa wawili peke yao kabla ya kuanza kufundishana kuogelea, John akakumbuka kujitambulisha tena, “Jina langu ni John Sailas…” Macho ya John na yule msichana yakaangaliana. John akauhisi moyo wake ukipiga kwa kasi. Akakijua kilichopo moyoni mwake dhidi ya msichana huyo. “Naitwa Dina,” msichana alisema huku akionyesha tabasamu dogo lililojificha kwa dhamira.
Ni siku ambayo John hakuisahau kamwe!

* * * * *

Aliacha kuliangalia pangaboi lililokuwa likizunguka na kukiangalia kiambaza cha varandani mwake. Akiwa hajaondoka kimawazo kuzikumbuka siku za mwanzo alivyoonana na Dina, John alizikumbuka siku hizo jinsi walivyokuwa wakipanga na wasichana hao siku za kuendelea kuwafundisha. Akiwa ameanza kwa kumfundisha Dina kama makubaliano yao yalivyo, John alijikuta akipata wakati mgumu wa kutoonyesha

hisia zake jinsi alivyokuwa akiteketea kimapenzi kwa msichana huyo hasa pale alipokuwa akiuzuia mwili wa Dina kwa mikono yake ambayo ilikuwa ikilaliwa na Dina aliyekuwa akijilaza juu ili asizame wakati akimfundisha mbinu za kutumia mikono na miguu wakati wa kuogelea. Kitendo hicho ambacho kilifanya mgusano wa mara kwa mara kwenye matiti ya Dina na ulaini wa tumbo la msichana huyo kukawa kunampelekea John kwenye hisia za matamanio zaidi, isitoshe wakati mwingine Dina alikuwa akionyesha woga wa kuzama na kujikuta akimkumbatia John. Kitendo cha mgusano wa miili yao kwa kukumbatiwa na

Dina kilimfanya John awe anajihisi kama anayepigwa na shoti ya umeme! Kadri walivyokuwa wakizoeana, macho yao yakaanza kuonyesha ukweli wa mambo kila walipokuwa wakitazamana. Ujumbe wa kuonyeshana kuwa wote wawili wanahitajiana ukawa dhahiri kati yao!
Siku moja John akauvunja ukimya! “Dina,” John aliita wakati wakiwa ndani ya maji yaliyowafika kwenye vifua vyao wakiangaliana ana kwa ana. “Nataka uwe girl friend wangu!” Ajabu ni kwamba, Dina hakuonyesha mshituko na kauli hiyo, ikiwa ni kinyume na John alivyotarajia kuwa ingeleta ubishano kati yao.

“Nilijua ipo siku ungeniambia hivi,” Dina alisema na kuikunja miguu yake ndani ya maji na kuanza kuelea na kichwa chake kuwa juu na hapo hapo akayapuliza nje maji yaliyoingia kinywani mwake. “Nataka upajue ninapoishi,” John aliendelea. “Tutapanga!” Dina alisema kirahisi kama vile jambo hilo halikuwa na umuhimu kwake, kasha alianza kuogelea na kumuacha John akiwa amesimama palepale alipokuwa.

Hawakupanga! John alisita kulikumbushia, alihofia angeonekana anaharakisha mambo. Dina naye akawa anaonyesha kama vile hakukuzungumzwa jambo la mapenzi kati yao! John akaendelea kuwafundisha kuogelea wasichana hao huku Dina akiwa kwenye hatua kubwa ya kujua kuogelea.
John akaona subira yake inaweza ikamwangamiza. Akamvaa tena Dina! “Dina nataka Jumapili uje nyumbani kwangu!” John alimwambia Dina kwenye simu, safari hii likawa sio ombi tena, bali ni mwendelezo wa kile alichokianza! “Si tutaonana Jumapili beach? Tutakapoonana tutalizungumza hilo,” Dina alijibu kwa utulivu. John akatambua yupo kwenye kuyeyushwa na Dina. Akakaza buti!
“Jumapili sitokwenda beach,” alisema. “Nitaitumia siku hiyo kwa ajili ya kukusubiri wewe uje nyumbani.”
“Huoni kama utakapokuja beach utaweza kunielekeza vizuri nyumbani kwako na tutakapoipanga siku itakuwa ni suala la mimi kuja moja kwa moja?”
“Naishi Kimara Baruti, niambie ni saa ngapi utakuja hiyo Jumapili ili nikusubiri kituoni?” John aliingiza karata ya ubishani. “John mbona hivyo?” Dina alilalamika. “Nimekwambia tutakapoonana beach tutayazungumza yote hayo. Kwani una wasiwasi gani?” “Kwa hiyo unanikatalia?” Kimya kikajiunda kwenye simu.
“Dina,” John aliita.
“Bee,” Dina aliitika.
“Kwa hiyo nijue hutaki?” John aliuliza.
John akamsikia Dina kwenye simu akishusha pumzi.
“Basi nitakuja saa nne,” hatimaye Dina alikubali.
“Nisubiri kituoni.”
Saa nne! John aliwaza. Akaufikiria muda huo jinsi unavyotumiwa kwa siku za Jumapili kwa watu mbali mbali kupeana ahadi. Hakujua ni kwa nini ulionekana ni muda bora kuliko muda mwingine! “Utanikuta nikikusubiri,” John alisema.

Baada ya kukata mawasiliano, John akatambua zilikuwa zimebaki siku mbili kuiwezesha Jumapili ifike!

Akaomba ahadi ya Dina iwe ya kweli na akamwomba Mungu siku hiyo kusitokee tatizo lolote litakaloingiza doa ahadi hiyo.

Jumapili ikafika, John akawa kituoni kabla ya saa nne. Akatarajia kumwona Dina akiwasili kwa daladala, akashangaa alipomwona akiteremka kutoka kwenye teksi!
Ukawa mwanzo wa penzi lao, sasa wanataka kuoana!

* * * * *

John aliinuka kutoka pale varandani alipokuwa amekaa, akaichukua barua yake ya majibu na kuingia nayo chumbani kwake. Aliyafikiria mahari aliyotajiwa, kidogo yalikuwa juu lakini hayakumwumiza kichwa. Akafikiria namna ya kuzipeleka habari hizo kwa wazazi wake. Alijua angelaumiwa kwa kiasi fulani kwa kuyafanya mambo kipeke yake hadi kufikia hatua hiyo bila ya kuwahusisha wao. Hilo nalo halikumsumbua kichwa, wazazi wake hawakuwa wakiendekeza lawama zisizokuwa na tija. Walikuwa waelewa na wenye ufahamu wa kuyajua mazingira tofauti. Simu yake ikaita. Alikuwa Muddy, rafiki yake wa karibu sana.
“Sema Muddy,” John alisema baada ya kuipokea simu.
“Nakuja kwako, upo nyumbani?”
“Wewe uko wapi?” John aliuliza.
“Nina kama dakika tatu au mbili nitakuwa nimeshatia timu hapo
kwako.”
“Utanikuta,” John alisema.
Muddy alimkuta John akilifunga jokofu lake baada ya kujimiminia maji ya kunywa kwenye glasi na kuirudisha chupa.
“Na mimi nahitaji hayo maji,” Muddy alisema na kwenda kuchukua glasi iliyokuwa ndani ya kabati la vyombo la kisasa.
John aliyekuwa ameitoa tena nje ya jokofu chupa ya maji aliyoitumia awali, alimmininia kwenye glasi maji aliyokuwa akiyahitaji Muddy. Muddy akayanywa maji akiwa amesimama.
“Posa imejibu,” John alisema.
“Usiniambie!” Muddy alisema huku akijifuta mdomo kwa kiganja chake na kuiweka glasi juu ya meza.
“Subiri nikuletee barua yenyewe,” John alisema akiwa na furaha huku akielekea chumbani kwake.
Muddy aliisoma barua hiyo na kadri alivyokuwa akiendelea kuisoma, uso wake ulizidisha tabasamu hadi alipoimaliza.
“Mwanangu unaoa!” alisema huku akiirudisha barua hiyo kwa John.
“Ndio manaake!”
“Lakini mahari wamegonga!”
“Kitu chenyewe kile ghali.”
“Kweli mwanangu, Dina mgogoro!”
Wote wakacheka na kugongesheana mikono.
“Umeshamwambia mwenyewe?” Muddy aliuliza.
“Nani, Dina?”
“Yeah.”
“Sijamwambia, lakini si atakuwa anajua?”
“Hata kama anajua, kumwambia nako kuna raha yake.”
“Jioni atakuja, nitamwambia. Isitoshe nina mpango wa kumnunulia na kumvisha pete ya uchumba, lakini

hatutafanya sherehe yoyote.”
“Ahh, hebu mtwangie umpe news.”
“Unajua hata wazee bado sijawaambia!” John alisema.
“Eti?” Muddy aliuliza huku uso wake ukionyesha kutoamini kile alichokisikia.
“Sijawaambia!”
“Lakini si wanajua kuwa umechumbia?”
“Hilo nalo sijawaambia!”
“Hayo masihara John?”
“Kweli sikuwaambia!”
Muddy akaonekana kuchoka ghafla, akakaa kwenye sofa. “Yaani wewe siku zote hizi za mchakato wa kutaka kumchumbia Dina, ina maana wazazi walikuwa hawajui?” aliuliza.
John akionekana kama aliyekosa amani, naye alijikuta akikaa kwenye sofa.
“Leo nitakwenda kuwafahamisha,” alisema.
“Duu!” Muddy aliguna, kisha hakuendelea.
“Lakini wazazi ni waelewa, watanielewa tu.” John alisema na sauti yake ilionyesha wazi alikuwa akijitetea.
“Hivyo ulivyofanya kama dharau ya kiaina mwanangu,” Muddy alilalamika.
“Wao ndio watakaokuwa kila kitu kwenye harusi yako, halafu hawajui kama umechumbia na wakati wanamjua Dina. Hiyo noma na haipendezi!”
“Nitakwenda kuyaweka sawa, usiwe na presha.”
“Tatizo lako John unajiamini sana. Shauri yako!”
John akaamua kuyabadilisha mazungumzo.

*****

MZEE Ken Richard Korogwe, tajiri maarufu jijini Dar es Salaam mwenye kumiliki meli mbili ndogo za mizigo zinazoitwa vidigidigi zinazosafirisha mizigo kwenye mwambao wa Afrika ya Mashariki kama vile Mombasa, Zanzibar na Comoro na ambaye pia ni mmiliki wa malori ya mafuta na vituo vya mafuta kwenye maeneo tofauti jijini na vingine vikiwa mikoani, ndiye baba mzazi wa Richard, mtoto pekee aliyezaa na mkewe kwa miaka thelathini na mitano wanayoishi ndani ya ndoa yao. Baada ya kuzaliwa Richard, miaka michache baadaye mkewe aligundulika kuwa na matatizo
ya tumbo na kufanyiwa operesheni ya kuondolewa kizazi, hali iliyowafanya wabaki na mtoto mmoja tu. Kubaki kuwa na mtoto mmoja kukawafanya yeye na mkewe wamwone Richard kama jicho lao, nembo na tunda la ndoa yao.
Mzee Ken na mkewe walihakikisha wanampa Richard elimu iliyo bora na kumfanya Richard afanikiwe kupata Shahada yake nchini Uingereza.
Mzee Ken kitaaluma ni Mhasibu, awali aliwahi kuajiriwa kuwa Mhasibu Mkuu kwenye Kampuni ya Mafuta kwa miaka kadhaa kabla ya kuteuliwakuwa Mkurugenzi wa Fedha na Utawala kabla ya kuacha kazi na kufungua biashara zake.
Mafanikio ya Richard kupata Shahada yalitokana na umahiri wake
kwenye somo la hisabati na kulidhihirisha kurithi kipaji cha baba yake. Richard baada ya kupata Shahada yake alirudi nchini na kujiunga na biashara za baba yake na kuwa mmoja wa viongozi kwenye kampuni inayomilikiwa na baba yake.
Malezi yalimfanya Richard awe na jeuri na kiburi cha kudharau watu.
Ujio wa Richard kwenye kampuni hiyo ya baba yake kukazua malalamiko ya kuwanyanyasa wafanyakazi

na malalamiko hayo yakamfikia mzee Ken. Lakini mzee huyo kutokana na shinikizo kutoka kwa mkewe ambaye ni
mama yake Richard, akawa anashindwa kumchukulia hatua kali mwanae, badala yake akawa anamsihi asiwe anawanyanyasa wafanyakazi hasa wa ngazi ya chini. Usia wake ukasaidia kupunguza kwa kiasi fulani manyanyaso hayo, lakini haukumaliza dharau za kijana huyo aliyekuwa akiringia utajiri wa baba yake na elimu aliyokuwa nayo. Baadhi ya wafanyakazi walilazimika kuacha kazi kwa ajili yake, ikawa inamlazimu mzee Ken apate kazi ya kuziba nafasi zinazoachwa kwa kuajiri wafanyakazi wengine
kila matukio hayo yalipojileta!
Richard alikuwa haiishi na wazazi wake, alikuwa akiishi kwenye moja ya nyumba nzuri zilizokuwa zikimilikiwa na baba yake iliyopo eneo la Mlalakuwa. Huko ndiko alikokuwa akiutumia muda wake na rafiki yake wa kike Judi, hadi walipokorofishana kuhusiana na masuala ya ndoa!

* * * * *

Kitendo cha Richard kukataa kumuoa kilimdhihirishia Judi kuwa alikuwa ahitajiki tena na Richard! Jambo hilo lilimpa wakati mgumu, likakatisha tamaa mustakabali wa hatima ya maisha yake ya ndoa kuishi na Richard.
Alimpenda Richard, alimpenda si kwa sababu ni mtoto wa tajiri, lakini pia alimpenda kwa sababu ni kweli alikuwa akimpenda! Alimheshimu kwa kila hali. Alimfanya aikatae mialiko ya kumtaka kimapenzi aliyokuwa akipewa na wanaume tofauti wenye uwezo wa juu wa kimaisha. Kamwe hakutarajia kama ingetokea siku Richard angemtamkia kauli kama hiyo!
Lilikuwa pigo kwake!
Ingawa Richard alijaribu kumbembeleza waendelee kuwa wapenzi, lakini kwa kutoa sharti la kutofunga ndoa wakati alipokuwa akijaribu kumfafanulia uamuzi wake huo wa kutomuoa, hata hivyo Judi hakuliridhia ombi hilo ingawa alijua kama angelikubali lingetoa nafasi nyingine ya kuendelea kufaidika kupata huduma za Richard. Judi alikiri kama angekubaliana na ombi hilo angekuwa sawa na kukubali kutumika kingono huku akijua haolewi! Ingawa alikiri, endapo angekubaliana na ombi hilo la Richard ingekuwa ni nafasi yake ya kuweza kuificha siri ya kukataliwa kwake kuolewa, lakini pia, kungewezesha kuendelea kuwakomoa kwa kuwaumiza wanawake wenzake waliokuwa wakimwonea wivu. Hata hivyo aliuona uamuzi wa kukubali kuendelea kuwa hawara wa Richard usingemsaidia.
Hakuwa tayari kuchezewa kisa tu, aonekane na wanawake wenzake kuwa amemdhibiti Richard! Alichokihitaji ni ndoa na sio kuchezewa!
Uamuzi huo wa Richard wa kukataa kumuoa ulimwumiza kila
alipoikumbuka kauli hiyo iliyokana kumuoa na wakati mwingine ilifanya aina ya mwangi uliomtesa kichwani mwake. Aliiona ni aina ya dharau aliyofanyiwa na alikuwa hakujiandaa na tukio la aina hiyo kutokana na kujiamini kwa asilimia zote kuwa, alikuwa ni chaguo la Richard! Judi alijijua kuwa ni mmoja kati ya wanawake wenye sifa za uzuri na mwenye mvuto kiasi cha kujiona alikuwa ni chaguo maridhawa kwa mtu aina ya Richard. Alikumbuka jinsi alivyokuwa hakusita kuonyesha dalili za kumkubalia wakati Richard alipokuwa akimzengea siku za nyuma kabla hawajafikia kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Na baada ya kuwa wapenzi, urafiki wao ukawa wa wazi, popote walipokwenda walikuwa pamoja. Uhusiano wao ukawa sehemu ya mazungumzo kwa vijana wenye
umri wao hususan wasichana ambao wengine hawakuzificha hisia zao za kumwonea wivu.
Viongozi wenye vyeo tofauti, Serikalini, Mashirika binafsi na Taasisi
nyinginezo walikuwa wakimjua Richard kuwa ni mtoto wa mzee Ken, mfanyabiashara tajiri. Na kila walipokuwa wakikutana naye wakati akiwa na Judi, Richard hakusita kutoa ujulisho kuwa, Judi ni rafiki

yake wa kike!
Ujulisho huo ukampa Judi umaarufu wa kujulikana kama mchumba wa Richard. Ukamzidishia kupata marafiki waliojikomba kwake na wakaibuka vile vile waliokuwa wakimwonea donge!
Umaarufu wa kujulikana kwake ulimfanya apewe kipaumbele kwa
kuletewa kadi kadhaa za mialiko kutoka kwa watu mbalimbali wenye daraja la juu kimaisha, zilizokuwa zikimtaka ahudhurie vikao vya harusi, michango ya sherehe na Harambee nyingine tofauti. Na mahudhurio yake katika shughuli kama hizo yalikuwa yakitukuzwa kwa kupokewa kama mtu maalumu. Judi alikiri heshima zote alizokuwa akizipata zilitokana na uhusiano wake wa kuwa na Richard ubavuni mwake!
Akajiuliza, kwa nini Richard alitumia nguvu zote za kumtambulisha kwa watu mbalimbali
kisha aje kumtosa kirahisi hivyo?
Ilimuuma!
Ilimuuma kwa sababu hakuijua sababu iliyomfanya Richard akatae
kumuoa. Moyo wake ulipata tabu ya kuamini labda kuna mwanamke mwingine ambaye Richard alipanga kumuoa. Alishindwa kuliamini hilo kutokana na ukweli wa mzunguko wa maisha aliyoishi akiwa na Richard. Richard alikuwa akimtimizia kila alichokuwa akikihitaji, lakini pia,
aliweza hata kumfungulia benki akaunti yenye kiwango kizuri cha pesa huku akaunti yake ya zamani ikiendelea kuwepo.
Judi alizidi kutatizwa na tukio la kukataliwa kuolewa na Richard ilhali Richard tokea awali alikuwa akimwonyesha dalili zote kuwa alikuwa akimpenda na hakuwahi kumfanyia visa vya aina yoyote pamoja na kuzungukwa na hisia za kumhisi kuwa ana wanawake wengine.
Kwa nini Richard amekataa kunioa? Swali hilo likabaki kuwa mwiba
uliomwumiza moyoni kila alipojiuliza!
Judi hakuwa mtoto wa maskini, lakini pia hakuwa mtoto wa tajiri. Wazazi wake wote wawili walikuwa wasomi na wenye uwezo wa pesa wa kawaida uliotokana na ajira zao wakiwa ni watawala makazini wanakofanyia kazi.
Maisha hayo ya wazazi wake ambao anaishi nao kwenye nyumba nzuri waliyoijenga eneo la Makongo na yeye mwenyewe kupewa elimu ya kutosha iliyompatia kazi nzuri, aliamini yangeweza kumsaidia kumuweka kwenye uamuzi wa kuachana na Richard, kisha angejenga subira kwa kutoa nafasi kwa mwanamume mwingine msomi mwenye kazi nzuri na maisha mazuri
kujitokeza ambaye atakuwa na mapenzi ya dhati na hatimaye kufunga naye ndoa.
Kwa kuupitisha uamuzi huo, Judi akajiandaa kupambana na wakati
mgumu wakati uhusiano wake na Richard utakapojulikana kuwa
umevunjika. Alijua wapo watu ambao wangemkabili bila ya aibu na
kumwuliza ukweli wa jambo hilo. Na wengine wangetaka kuijua hata sababu ya uhusiano wao kuvunjika, wengi wao wakiwa ni wanawake!
Wanawake! Judi aliwaza. Kweli tuna matatizo!

* * * * *

Ofisi za kampuni ya mzee Ken zipo kwenye jengo moja maarufu jijini Dar es Salaam lililokuwa na maofisi mengine ya makampuni tofauti lililoko katikati ya jiji. Ofisi za kampuni yake zilikuwa kwenye ghorofa ya nne ndani ya jengo hilo lenye ghorofa zaidi ya kumi na mbili. Mzee Ken mwenyewe alishikilia vyeo vya Mkurugenzi Mtendaji na Mhasibu Mkuu huku mwanae Richard akiwa ni Mkaguzi wa Ndani wa Mahesabu.
Asubuhi ya siku hiyo Richard aliingia ofisini na kumkuta karani wake wa kike akiwa shughulini na

kompyuta.
“Niitie Rama!” Richard alimwambia karani wake bila ya kutanguliza salamu yoyote, alionyesha kisirani asubuhi hiyo na sauti yake ilifanya amri.
Karani huyo aliyeitwa Rehema alimwangalia Richard na kugundua bosi wake yupo kwenye kisirani asubuhi hiyo. Alikuwa akizijua vizuri tabia za Richard na alikwishazizoea na kumzoea Richard mwenyewe. Aliubinua mdomo wake kwa aina ya dharau wakati Richard akiingia ofisini kwake.
Rama ambaye ni dereva anayetumiwa mara kwa mara kuliendesha gari la Richard pale anapohitajika dereva wa kuliendesha, umri wake ulikuwa wa mtu mzima aliyevuka miaka hamsini. Wafanyakazi wote kasoro Richard, walikuwa wakimuita kwa jina la ‘mzee Rama.’ Mara zote alikuwa akivaa kofia ya baragashea na suti ya Kaunda yenye rangi ya ugoro ambayo ni sare yake ya kazini. Alifika ofisini kwa Rehema kuitikia mwito, akasimama mbele ya meza aliyokuwepo Rehema.
“Umesema bosi ananiita?” mzee Rama aliuliza.
“Yuko ndani!” Rehema alisema kwa sauti iliyoonyesha kumchukia Richard.
“Na leo uangalie, naona jamaa hakuamka vizuri!”
Macho yaliyoonyesha woga yakajitokeza usoni kwa mzee Rama, akajikuta akiuangalia mlango wa ofisi ya Richard kama vile Richard angejitokeza muda huo huo. Akaurudisha uso wake kwa Rehema kasha akaiinamia meza na kujizuia kwa mhimili wa mikono yake.
“Kwani anasemaje?” alinong’ona huku akiwa ametengeneza kibyongo mgongoni
mwake. Sauti yake haikufanya mzaha, alionyesha dhahiri alikuwa akimwogopa Richard.
“Mi, ntajuaje?” Rehema alimshushua mzee Rama kwa kumpa jibu la mkato. Kisha akaendelea, “Na wewe mzee acha woga! Unamwogopa huyo Richard utadhani ni Mungu wako!”
Mzee Rama akajaribu kutengeneza tabasamu lililokataa usoni kwake.
“Huyu kijana ni mkorofi sana!” alisema.
“Hee! Unaanza kuogopa kabla hujajua anachotaka kukwambia? Huyu si kama mwanao tu! Naona siku atakayokwambia kibarua kimeisha, utarudishwa nyumbani ukiwa maiti!”
Mzee Rama akajichekesha. “Wewe mtoto acha maneno ya uchuro!” alisema huku akiendelea kujichekesha.
Mlango wa ofisi ya Richard ukafunguliwa, Richard akatokeza! Mzee Rama akashituka, akaganda pale alipokuwa, akabadilika kama siye yeye aliyekuwa akizungumza. Kujichekesha kukayeyuka, akauchuna uso kama samaki aliyekaushwa! Rehema akawa anaumia mbavuni kwa kujizuia kucheka huku akijitahidi kuendelea na kazi kwenye kompyuta kama vile hajui kinachoendelea.
Richard alikuwa amekamata funguo za gari mkononi, akamwangalia mzee Rama, kisha bila ya kusimama akamtupia funguo hizo, zikampiga mzee Rama maungoni na kuangukia miguuni mwake huku akihangaika kutaka kuzidaka.
“Kalikoshe gari langu!” Richard alisema bila ya kugeuka nyuma, akatokahuku akimuacha mzee Rama ameinama akiziokota funguo alizotupiwa.
Baada ya Richard kutoka nje ya ofisi, Rehema alisikitika peke yake na kulalamika kwa hasira, “Huyu baba huyu!” kisha asiendelee.
Uso wa mzee Rama ulikuwa bado umejengwa na hofu ya nidhamu ya woga, akamwangalia Rehema na kusema, “Wacha nitoke, asije akarudi na kunikuta!”
Rehema alimwangalia mzee Rama alivyokuwa akitoka kisha akaendelea tena kusikitika peke yake.
Akajisemea moyoni: Laiti ningetupiwa mimi funguo zile, nami ningeziokota na kumrudishia kwa kumtupia nazo na kazi leo hii ningeacha!

* * * * *

Mzee Ken alimaliza kifungua kinywa akiwa na mkewe kwenye meza ya chakula, wote wawili wakiwa wamejiandaa kutoka, kila mmoja na safari yake na usafiri wake.
“Unakumbuka leo kuna kikao kingine cha harusi?” mkewe alisema.
“Nakumbuka lakini sitokwenda!” mzee Ken alijibu.
“Kikao kilichopita hukwenda na hiki pia huendi?”
“Leo mchana nitakuwa kwenye mkutano utakaokutanisha wafanyabiashara wa hapa nchini na ujumbe maalumu wa kibiashara kutoka Uturuki unaoongozwa na Waziri wao wa biashara aliyewasili hapa nchini jana. Ukienda wewe inatosha, sio lazima wote tufike.”
“Sawa, basi nitamfahamisha Adam kuwa na leo hutofika.”
“Na mimi baadaye nitampigia simu kumjulisha kuwa sitofika,” mzee Ken alisema huku akionyesha kutaka kuondoka.
Mkewe akamwangalia kwa sura yenye jambo. “Una haraka sana?” aliuliza.
“Kwani vipi?”
“Kuna kitu nataka kuzungumza na wewe!”
Kauli hiyo ikamfanya mzee Ken atulie na kumwangalia mkewe kwa utulivu. “Kinahusiana na hicho kikao cha harusi?” aliuliza.
“Hapana. Kinamhusu Richard!”
“Ana nini?”
“Hivi Richard anataka mpaka mmoja wetu afe ndio aoe?”
Swali hilo kidogo lilionyesha kama kumchanganya mzee Ken, akaonyesha uso wenye mshangao. “Kwa nini unasema hivyo?” aliuliza.
“Ulishawahi kumshauri lolote kuhusu suala la kuoa?” mkewe aliuliza swali badala ya kujibu swali.
“Mbona sijakuelewa unachotaka kukizungumza?”
“Nataka kujua ni lini Richard atapata wazo la kuoa?”
“Nadhani hilo ni suala lake binafsi. Kwa nini usimwulize?”
“Najua ni suala lake binafsi, lakini sisi wazazi wake ni jukumu letu kumshauri au kujua mawazo yake kuhusu jambo hilo. Unadhani yeye na Judi wataishi maisha ya uhawara mpaka lini? Wamekwishakaa hivyo kwa muda mrefu, nadhani sasa umefika wakati wa kumshauri afunge ndoa na mwenzake.”
Mzee Ken hakufanya haraka ya kujibu. Alionekana kutafakari huku akivigonga vidole vyake juu ya meza.
“Ni vyema tukamshauri hivyo,” mkewe akawahi kusema kabla ya mzee Ken hajajibu na kuichukua nafasi hiyo kulieleza alilotaka kulieleza.
“Ukaaji wao wa uhawara kwa muda mrefu unaweza ukawafikisha kwenye vishawishi vingine vinavyoweza kuwaingiza kwenye migogoro itakayowafikisha kuachana. Matokeo yake, Richard anaweza akadakwa na shangingi. Akapungwa vilivyo na hatimaye kudai kumuoa. Si unawajua wanawake wa mijini walivyo werevu hasa wakishanusa harufu ya fedha.
Wakijua Richard ni mwanao unadhani watamwachia? Watahakikisha wanamdhibiti hata kama ikibidi kwenda kwa waganga ili mradi wamuinamishe, kama wenyewe wanayosema kulishwa limbwata. Usije ukashangaa ukamwona mwanao akatuletea mwanamke ambaye siye na akadai kutaka kumuoa!”
“Unayoongea ni kweli, lakini pia tunatakiwa tuangalie na upande wa pili. Inawezekana wenyewe wakawa hawajapanga hivyo.”

“Kuna ubaya gani tukiwashauri hivyo? Utajuaje ikiwa hujakaa na
mwanao na kuzungumza naye?”
“Kwa hiyo, unachokitaka nikae na Richard ili nimwulize kama ana
mpango wowote wa kuoana na Judi? Au nimwulize kama ana mpango wowote wa kuoa?”
“Sasa ni yupi mwingine wa kumuoa zaidi ya Judi? Judi ndiye
tunayemfahamu na hata wewe mwenyewe umekwisha kumsifia kuhusu tabia zake. Kwanza ana elimu nzuri, kazi nzuri na tabia yake ni nzuri. Ni yupi mwingine zaidi yake? Richard atakaponiletea kiruka njia unafikiri nitakubaliana naye?”
“Sawa,” mzee Ken alisema kwa sauti ndogo.
“Usiitikie kama vile nakulazimisha!” mkewe alisema huku akionyesha kuugundua unyonge ulioonyeshwa kwenye sauti ya mumewe. “We huoni fahari endapo Richard ataoa sisi tukiwa hai? Au hujisikii vibaya kila baada ya muda tunaletewa kadi za kuhudhuria vikao vya harusi za wenzetu wanaotaka kuozesha watoto wao? Sisi kazi yetu itakuwa ni kuwachangia hadi lini? Na sisi tutachangiwa lini? Au unataka tuchangiwe michango ya sanda badala ya harusi? Aaa bwana, lazima ifikie mahali na sisi tuchangiwe, na sisi tusikie fahari kumwona mtoto wetu anaoa. Nimeshachoka kuwapigia watoto wa wenzangu vigelegele, nataka na mimi mtoto wangu apigiwe vigelegele!”
“Sasa lawama za nini tena mke wangu? Umeongea nimekukubalia!
Nimekwishakwambia nitakwenda kuzungumza na Richard asubuhi hii ili tumsikilize na yeye ana maoni gani!”

RICHARD hataki kumuoa Judi, mama Rich anaulizia mwanae anaoa lini?? Mzee Richard ameahidi kuzungumza na mwanae juu ya hilo.
Kwanini Richard hataki kumuoa Judy??
Nini hatma ya ndoa ya John na Dina???

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME.

SEHEMU YA TATU

RICHARD baada ya kumtupia funguo mzee Rama na kutoka ofisini, alielekea moja kwa moja hadi ilipo ofisi ya baba yake. Aliingia na kumkuta Katibu Muhtasi wa baba yake ambaye ni mama wa makamo, akamsalimia kwa Kiingereza kwa dhamira ya kukwepa kutoa shikamoo.
“Baba yupo?” Richard aliuliza baada ya kusalimia, wakati huo huo akauangalia mlango wa ofisi ya mzee Ken. “Bado hajafika,” mama huyo alijibu huku akimwangalia Richard usoni.

Richard akashukuru na kutoka. Akaelekea kwenye korido inayoelekea kwenye lifti, akaisikia kengele ya lifti inayoashiria kuwasili kwa lifti kwenye ghorofa hiyo na kuusikia mlango wake ukijifungua. Wakatoka watu wawili, mzee Ken na dereva wake aliyekuwa amebeba mkoba wa ofisini. Richard akasimama.
“Nimetokea kukuulizia sasa hivi,” Richard alisema na kumsalimia baba yake baada ya kukaribiana huku dereva wa baba yake akisalimiana naye bila ya kusimama.
“Vipi una tatizo?” mzee Ken aliuliza.
“Nilikuja kuhusu masuala yale ya TRA.”
“Bado sijayamaliza, nitakujulisha yakiwa tayari.”
“Halafu pia, nilitaka kutoka na huenda nikachelewa kidogo kurudi,”

Richard alisema kwa kujiamini, akauparaza mkono wake kwenye mgongo wa tai iliyompendeza.
“Kabla hujatoka, kwanza nataka tuzungumze,” mzee Ken alisema na kuondoka. Kauli hiyo ikamlazimisha Richard amfuate baba yake. Wakati wakianza kuingia kwenye ofisi ya Katibu Muhtasi, wakapishana na dereva wa mzee Ken aliyekuwa akitoka. Richard akatangulia kuingia ofisini kwa baba yake wakati mzee Ken akiwa amesimama akisalimiana na Katibu Muhtasi wake. Wakiwa ofisini, mzee Ken akiwa amekaa

nyuma ya meza yake ya thamani na Richard akiwa amekaa mbele kwenye sofa ya wageni, mzee Ken alianza kwa kusema, “Mama yako..,” akasita ghafla. Akabadilisha kauli, “Kuna jambo tumelijadili mimi na mama yako, na tumeona ni wajibu wetu kukushauri, hata kama jambo hilo litakuwa linaingiliana na maisha yako binafsi,” hapa alinyamaza na kumwangalia kwa utulivu Richard. Kisha akasema, “Richard, mna mpango wowote wa kuoana, wewe na Judi?”

Swali hilo likaonekana ni la ghafla kwa Richard aliyeonyesha dhahiri kutolitarajia. Kwa sekunde kadhaa alionekana akiwa kwenye wakati mgumu wa kuweza kulijibu. Akakumbuka kuulizwa swali kama hilo na Judi siku chache zilizopita.
“Hatuna mpango wowote,” hatimaye Richard alijibu.
“Kwa hiyo mtaishi kwenye uhawara mpaka lini? Au hamna mpango hata wa kutangaziana kuwa ni wachumba?”
Richard akajenga ukimya mwingine. Kisha aliinua kichwa chake kumwangalia baba yake. “Nitakapokuwa tayari kuhusu suala hilo nitawaelezeni,” alisema. “Sipingani na kauli yako, lakini napata shida kuamini kama kwa kipindi chote mlivyoishi pamoja mkiwa marafiki mtakuwa hamjawahi kujadiliana jambo hilo?”
Swali hilo likaonyesha kumpa tena wakati mgumu Richard. Akakitengeneza kimya kingine.
“Tulishawahi kulijadili,” hatimaye Richard alisema.
Safari hii mzee Ken hakuingiza neno. Akamwonyesha Richard kuwa anasubiri maelezo zaidi ya jambo alilolizungumza.
“Lakini hatukuelewana!” Richard alisema huku akiiangalia sakafu ya vigae ing’aayo.
“Kwa nini?”
“Nilimkatalia!”
“Nadhani sijakuelewa vizuri! Ulimkatalia…?” mzee Ken alisema huku akionyesha kutokiamini alichokisikia.
“Nilimwambia sina mpango wa kumuoa!”
Kauli hiyo ikakamilisha mshituko wa mzee Ken, hata hivyo utulivu wake aliouonyesha uliweza kuuficha mshituko wake.
“Judi alisemaje baada ya kumtamkia hivyo?” mzee Ken aliuliza na alijaribu kujiweka kwenye utulivu zaidi.

Safari hii Richard aliuinua uso wake na kumwangalia baba yake, kisha aliinama tena kuiangalia sakafu.
“Hatukuwa na maelewano tena!” alisema na kunyamaza. Ghafla akaendelea, “Sasa hivi hatuko pamoja!”
Bila ya kutarajia, mzee Ken alijikuta akishusha pumzi kwa nguvu. Akaikumbuka kauli ya mkewe iliyoonya hatari ya Richard kuangukia kwenye mikono ya shangingi. “Kama ulijiona huna mpango wa kumuoa karibuni, kwa nini usingemweleza ukweli kuwa, kwa sasa hivi huna mpango huo, lakini ungempa matumaini ya baadaye!” mzee Ken alisema huku akionyesha wazi kutoridhika na maamuzi hayo ya mwanae na hata sauti yake ilifanya mkwaruzo. “Kwa nini umweleze kuwa huna mpango wa kumuoa?”
“Nilimweleza hivyo kwa sababu sio chaguo langu!”
“Jesus!” mzee Ken alihamanika na kushindwa kuamini kuisikia kauli hiyo ikitoka kwa mwanae. “Kwa hiyo chaguo lako ni nani?”
“Dina!” Richard alisema bila ya kutafuna maneno.
“Dina?” mzee Ken aliuliza huku akiwa amepigwa na butwaa na hofu ya kuwa analetewa shangingi aliyetabiriwa na mkewe ikiwa imekwisha kumvaa. “Ni nani huyo Dina?” safari hii sauti yake aliipandisha kidogo.
“Sisi tunamjua?” aliuliza kwa lugha ya Kiingereza.
“Dina Nzasa. Mama anamjua!”

* * * * *

Usiku baada ya mkewe kurudi kutoka kwenye kikao cha harusi na yeye kurudi kutoka kwenye mkutano, wakiwa tena kwenye meza ya chakula, baada ya kumaliza kula ndipo mzee Ken alipomwelezea mkewe yaliyojiri kwenye mazungumzo kati yake na Richard.
“Na anasema unamjua huyo Dina!” mzee Ken alimalizia.
“Dina Nzasa…Dina Nzasa…” mkewe alijaribu kuvuta kumbukumbu.
“Ah, nimekwishamfahamu!” alisema na uso wake kujaa nuru. “Si yule binti wa Bwana Nzasa anayeishi karibu na duka la vinywaji hapa mtaa wa nyuma yetu?”
“Nzasa yupi?” mzee Ken aliuliza huku akionyesha bado hajamtambua mtu anayefahamishwa.
“Nzasa huyu aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii, sasa hivi amestaafu. Ana kama miaka miwili tokea astaafu. Mkewe ni huyu dada anayefanya kazi Ardhi ambaye alitusaidia kupata hati ya umiliki wa kiwanja chetu kilichopo Boko. Mara hii umekwisha kumsahau?”
“Nimekwisha kumkumbuka!” mzee Ken alisema. “Si huyu aliyekuwa
akimtuma binti yake hapa nyumbani kutuletea zile nyaraka…”
“Haswaa!” mkewe alidakia. “Basi ndiye huyo anayeitwa Dina!” kisha sauti yake ikatulia na kuendelea, “Dina anavyoonekana ni msichana aliyetulia na miye nilikuwa sijui kama wana uhusiano wowote na Richard. Au Richard alikwambia kama nilikuwa naujua uhusiano wao?”
“Yeye alisema, wewe unamjua Dina.”
“Ni kweli namjua! Richard jamani!” mkewe mzee Ken akapiga kite cha kuhamanika. Kisha akasema kwa sauti ya kuhuzunisha, “Hili la Richard kusema eti Judi sio chaguo lake, kwa kweli limeniumiza mno. Unajua nashindwa kumwelewa mwanao! Alimtongozaje kama sio chaguo lake? Inahuzunisha kumwona mwanangu amempotezea muda wake yule msichana, kwa kweli siamini! Maskini Judi, nilikuwa nampenda huyu binti wa watu na yeye mwenyewe alikuwa anampenda sana Richard. Hivi nitamwangaliaje siku tutakapokutana?” mke wa mzee Ken akaonyesha kukata tamaa. “Ndio hivyo, hatuwezi tukayaingilia maamuzi ya Richard. Yeye ndiye anayemjua vizuri Judi kuliko tunavyomjua sisi na hatujui kwa nini amemchagua Dina, labda ndiye aliyemwona anamfaa. Pengine amependezwa na tabia zake!”
“Lakini kuna tatizo jingine linaloumiza kichwa kuliko hilo,” mzee Ken alisema, kisha kabla ya kuendelea aliinamisha kichwa na kusikitika.
“Ni mtafaruku juu ya mtafaruku,” alisema. Mkewe mzee Ken akaingiwa na mshangao, akasubiri kusikia mumewe atasema nini.
“Dina hamtaki Richard!” mzee Ken alisema kwa msisitizo.
Mkewe mzee Ken akaishiwa nguvu! “Amekwambia Richard mwenyewe?” aliuliza kama asiyeamini alichokisikia.
“Yeye mwenyewe Richard ameniambia, tena bila ya wasiwasi wowote!
Anasema amejitahidi sana kumbembeleza Dina kwa kutumia mbinu tofauti lakini anadai Dina alikataa katakata kukubali kuolewa naye. Cha ajabu mwanao bado anasisitiza kuwa, Dina ndiye chaguo lake!”
“Huyu mtoto ana wazimu?” mke wa mzee Ken aling’aka. “Mwanamke amemkataa si basi!”
“Labda ana sababu ya kumng’ang’ania.”
“Hawa watoto wetu wa siku hizi watatuua kwa presha. Kama mwanamke amekukataa si unatafuta mchumba mwingine wa kuja kumuoa?”
“Naona unayazungumza mambo yaliyopitwa na wakati mke wangu. Hayo unayoyazungumza ni ya enzi zetu, enzi zetu unatafutiwa mchumba halafu unaonyeshwa, baadaye unaulizwa kama umemkubali au umemkataa. Ukisema humtaki, basi unatafutiwa mchumba mwingine. Leo hakuna hilo. Wenyewe kwa

wenyewe wanatafutana huko huko wanapoonana na wakishakubaliana kuoana ndipo wanapokuja kwetu na kutufahamisha na mara nyingine hata kama wazazi wakikataa, wao wanalazimisha kuoana.
Lakini hili la mwanao limekuja kiaina yake, mwanao hatakiwi, yeye analazimisha! Utaliingiliaje jambo kama hilo?"
"Tena umenikumbusha baba Richard!" mkewe mzee Ken alisema.
"Nakumbuka mama yake huyu msichana aliwahi kuniambia yuko mbioni kutaka kumwozesha binti yake… ndio nakumbuka! Aliniambia angeniletea na kadi ya mchango!"
"Binti yake yupi?"
"Nadhani atakuwa ni huyu huyu Dina."
"Anataka kuolewa na nani?"
"Sijui."
Uso wa mzee Ken ukaangukia kwenye mshangao. "Ina maana Richard
hajui kama huyo anayetaka kumuoa kuwa anaolewa na mtu mwingine?" aliuliza.
"Sijui. Naona huyu mtoto anataka kutuchanganya!"
"Wacha niongee naye sasa hivi!" mzee Ken alisema na kuichukua simu yake ya mkononi iliyokuwa mezani. Akampigia Richard.
Kimya kilipita kati yao wakati mzee Ken akisubiri kujibiwa kwenye simu aliyoipiga. Hatimaye mzee Ken alijitikisa mwili na kusema, "Richard! Mbona huyu msichana uliyemzungumza kumbe naye anataka kuolewa?"
"Najua!" Richard alijibu kutoka upande wa pili wa simu.
"Lakini ni yeye ndiye niliyempenda na moyo wangu unaniuma kuona anaolewa na
mtu mwingine!" Richard alisema.
"Nitakupigia baadaye!" mzee Ken alisema na papohapo alikata simu. Akamwangalia mkewe, "Unajua huyu mtoto hovyo sana!" aling'aka.
"Kwani anasemaje?"
"Anasema analijua jambo hilo!"
"Jambo gani?"
"La Dina kuolewa!"
"Ebo!" mkewe mzee Ken alisema kwa mshangao.
"Ndivyo anavyodai! Halafu anaendelea kusema, eti huyo ndiye aliyempenda na moyo wake unamuuma sana kuona anaolewa na mtu mwingine! Huyu mtoto ana wazimu?"
"Ama kweli moyo ukipenda..!" mkewe alisema bila ya kumalizia.
Akasikitika peke yake.
"Sasa ana maana gani kusema hivi?" mzee Ken aling'aka tena.
Mkewe akafikiri, kisha akasema, "Hawa watoto wetu wa siku hizi si ajabu ukasikia amefanya jambo la ajabu kwa vitu vya kipuuzi kama hivi!"
Mzee Ken akamwangalia mkewe kwa kushituka. "Una maana gani?" aliuliza.
"Lakini sidhani kwa Richard kama anaweza akafanya upuuzi wa aina hiyo," mkewe alisema huku akijaribu kuituliza sauti yake.
"Upuuzi gani?" mzee Ken aliuliza huku akionyesha kama vile alikuwa akikijua kinachotaka kutamkwa na mkewe.
"Anaweza akajiua!"
"Ohoo, sasa mke wangu unaongea nini!" mzee Ken alihamanika.
"Khee! Unashangaa hilo? Kwa nini asiweze? Hawa watoto wetu wa leo wana akili? Au unafikiri huko kusoma nje ndio kutamfanya asiweze kufanya upuuzi wa aina hiyo?"

“Sasa kwa mfano akiung’ang’ania huo upuuzi wa kutaka kumuoa
tutafanyaje?”
“Itabidi tukaingize fitna ili Dina asiolewe na huyo anayetaka kumuoa!”
“Halafu?”
“Aolewe na Richard!”
“Wakati huyo Dina kishamwambia wazi mwanao kuwa hamtaki?”
“Yeye Dina ni nani hadi awe na jeuri hiyo?” mke wa mzee Ken alisema kwa sauti ya dharau.
“Sasa utafanyaje?”
“Sijajua, lakini naweza nikaivuruga ndoa yake asiolewe na huyo anayetaka kumuoa, kisha nikakigeuza kibao mwanangu Richard akageuka kuwa mume wa kuja kumuoa Dina. Babu, mwanamke mwenzake ni mwanamke, asikwambie mtu!”
“Utakwenda kumwambia nini huyo Dina ili akuelewe unachokizungumza?”
“Sina muda wa kuongea naye!” mke wa mzee Ken alisema kijeuri na kubenua mdomo wake.
“Kumbe utakwenda kuongea na nani?” mzee Ken aliuliza kwa kauli iliyoonekana kama kitu anachokizungumzia ni kigumu kufanyika.
“Mama yake!”
“Tutakuwa tumefanya dhambi!” mzee Ken alisema bila ya kumwangalia mkewe machoni.
“Kwa hiyo upo tayari mwanao ajiue?”

Mzee Ken akaduwaa na kumwangalia mkewe. “Lakini hajasema kama atajiua!” alisema.
“Anayetaka kujiua anasema? Naomba hili jambo uniachie mimi!”
Mzee Ken alishusha pumzi, akakosa la kusema.
“Hivi, kama Richard anataka kumuoa Dina, kwa nini ishindikane kumuoa?” mkewe mzee Ken alisema kwa sauti ya kiburi. “Marafiki zetu watatuelewaje wakisikia kuwa tumeshindwa kutumia uwezo wetu wa utajiri kuishawishi familia tuliyoizidi kipato kukubali binti yao aolewe na mtoto wetu? Mumewe yule mama sasa hivi hana kitu! Mafao yake ya kustaafu alikwenda kuyanunulia shamba, shamba limewashinda na nasikia wameliuza au wanataka kuliuza. Sasa hivi yule mama ndiye mlishaji wa nyumba kwa kutegemea hicho kibarua chake cha huko Ardhi, sijui ana kicheo gani! We si umeona baada ya kutufanikishia kuipata hati ya kiwanja cha Boko, mbona zile laki tatu tulizompa kama ahsante hakuzikataa?
Azikatae ana jeuri hiyo?”
Mzee Ken akabaki kuwa bubu.
“Na sitaki umwambie Richard lolote!” mkewe alionya. “Niwachie mimi mambo yote nitayaweka sawa.”

******

ILIKUWA usiku muda mfupi baada ya taarifa habari kutoka kwenye runinga kumalizika, mama yake Dina aliusikia mngurumo wa gari inayosimama nje ya nyumba yao, kisha akasikia mlio wa mlango wa gari uliofungwa. Akajua ni mgeni wa hapo nyumbani.
“Nadhani kuna mgeni,” mzee Nzasa alisema akiwa amekaa sebuleni kwenye sofa akiangalia runinga.
Mama yake Dina aliinuka kutoka kwenye sofa akaenda mlangoni.
“Hodi!” sauti ya mwanamke ilisikika kutoka nje akiwa amekwishaingia ndani ya uzio wa nyumba hiyo kupitia kwenye geti dogo lililokuwa wazi.
“Karibu,” mama yake Dina aliitikia akiwa ndani, akaufungua mlango wa mbele. “Oh, karibu mama Richard,” alisema.
“Ahsante mama Dina,” mke wa mzee Ken alisema na kuingia ndani.

“Karibu mama, karibu!” mzee Nzasa alisema alipomwona mke wa mzee Ken.
“Ahsante shemeji,” mama Richard alisema na kumpa mkono mzee Nzasa na kusalimiana naye kabla ya kukaa kwenye sofa.
“Gari umeiacha na mtu nje?” mama Dina aliuliza.
“Hapana.”
“Hakuna haja ya kutia wasiwasi, vibaka hawapitipiti kwenye mtaa huu,” mzee Nzasa alisema. “Wacha niwapisheni.”
“Ah, hapana shemeji, mbona nimekuja kwa mazungumzo ya kawaida
tu,” mama Richard alisema.
“Lakini si umekuja kwa ajili ya kumwona mwenzako?”
“Ni kweli, lakini sio faragha.”
“Usijali, nitaangalia TV ya chumbani, nyie endeleeni,” mzee Nzasa alisema na kuondoka.
“Ehee, za siku mbili, tatu mama Richard?” mama Dina aliuliza baada ya mzee Nzasa kuondoka.
“Nzuri tu, za kwenu?”
“Sisi hatujambo, karibu.”
“Dina yupo?” mama Richard aliuliza na kuangalia upande wenye korido ambako kuna vyumba.
“Yupo chumbani kwake anaangalia TV.”
“Kilichonileta kwako mama Dina,” mama Richard alisema.
“Nakumbuka uliwahi kuniambia unataka kumwozesha binti yako na ungeniletea kadi ya mchango. Nimeifuata hiyo kadi.”
“Kadi za mchango bado sijaanza kutoa mama Richard, nikitoa nitakupitishia. Wala usitie shaka.”
“Ukweli ni kwamba nilianza kutia shaka, nikasema mhh, huyu mama Dina si aliniambia anataka kumwozesha binti yake na angenipitishia kadi ya mchango? Mbona kimya? Ndio nimeamua kuja mwenzangu, pengine umenisahau.”
“Sijakusahau mama Richard, nasubiri tu mambo yaive ndio nikufuate.”
“Basi kumbe wasiwasi wangu ulikuwa wa bure.”
“Sijui nisemeje mama Richard, nakushukuru kwa kuyafuatilia haya mambo, si unajua yanavyochanganya kichwa?”
“Hayo ni ya kuyasema? Mhh, we haya mambo yaangalie kwa mwenzako tu, lakini yakija kwako lazima yakuchanganye!” mama Richard alisema, akanyamza na kujenga ukimya mfupi. Kisha akajiweka vizuri kuuliza swali lililomleta kwenye nyumba hiyo. “Kwani ni binti yako yupi anayeolewa?” aliuliza.
“Anayeolewa ni Dina!” mama Dina akajinasisha.
Mama Richard akamudu kuutengeneza mshangao wa bandia usoni kwake. “Haa! Dina ndiye anayeolewa?” alisema huku sauti yake ikionyesha kufanikiwa kushangaa.
“Dina mwenzangu!” mama Dina akazidi kujiingiza kichwa kichwa.
“Anaye rafiki yake, wenyewe wamekubaliana waoane, basi ndio ameleta
barua ya kumchumbia.”
“Kwa hiyo tayari mmemjibu?”
“Tumemjibu, sasa tunasubiri alete hayo mahari kisha nasi tuanze vikao.”
Mama Richard akaitumbukiza karata aliyoipanga kuanza kuicheza.
“Nakumbuka Dina aliwahi kuniambia kitu kama vile alikuwa akisubiri majibu yake ya kidato cha sita? Na majibu si tayari yametoka? Kwani hakuchaguliwa kwenda Chuo Kikuu?”
“Hakubahatika mwenzangu!” mama Dina alisema na kuguna.
“Imeniuma sana kutochaguliwa kwake!”
Hapo ndipo mama Richard alipoukamata usukani wa kumwongoza mama Dina!

“Sasa kwa nini mnakimbilia kumwozesha? Si mngemtafutia kwanza Chuo cha kusoma? Au hata awe na ajira yake kisha ndio aolewe?”
“Kuna mipango ya kazi tunayomfanyia.”
“Sasa kwa nini msisubiri kwanza aanze kazi kisha aolewe?”
“Hata wajomba zake walilizungumza hilo, na sisi tulimshauri hilo na hajakataa, lakini anauliza hiyo kazi itapatikana lini? Ili kama kuiahirisha harusi basi ijulikane itaahirishwa kwa muda gani.”
Mama Richard akajiona yupo karibu ya kumuua Tembo kwa ubua.
“Akipata kazi sehemu nyingine yoyote si anaweza akafanya? Au lazima apate huko mnakomtafutia?” alisema.
“Mwenzangu kokote kule! Je, huko tunakotegemea ikikosekana?”
Mama Richard akaitumbukiza karata yake ya mwisho.
“Basi mimi nitazungumza na baba Richard ili ampatie kazi kwenye kampuni yake. Nadhani sio vyema mkafanya haraka ya kumwozesha, bora aende kwa mumewe akiwa na kazi yake, maisha yenyewe haya ni ya kusaidiana. Tena nitamwambia baba Richard ampe mshahara mzuri.”
Kitanzi kikawa kimening’inizwa usoni kwa mama Dina, naye bila ya kusita akakitumbukiza kichwa chake.
“Mbona nitakushukuru mama Richard kama ukiweza kunifanyia hilo!” alisema.
“Kama mimi mwenyewe nimekuahidi, basi hilo usilitie shaka nalo. Nitahakikisha baba Richard anampatia Dina kazi yenye mshahara mzuri!”
Hali ikabadilika ghafla. Mama Dina alijikuta akiwa ananyenyekea kama kijakazi mbele ya nokoa na hata pale mama Richard alipoaga, ilibidi mama Dina kutaka kwenda kumuita Dina ili aje kumsalimia.
“Hapana usimsumbue mtoto, mwache apumzike. Lakini kitu kimoja mama Dina,” mama Richard alisema kwa utulivu. “Habari hizi za kazi usimgusie kabisa Dina, usimwambie kama kuna kazi ninayomtafutia. Na sitaki ajue kama ni mimi ndiye ninayemtafutia. Na endapo kama atajua, ama kwa kumwambia wewe mwenyewe au kuambiwa na mtu mwingine yeyote, mama Dina itabidi unisamehe, ujue sitohangaika kumtafutia kazi mwanao! Naomba hilo ulizingatie. Please usimwambie!”
“Kwa jina la Yesu Kristo Msalabani, sitamwambia!”
“Nitafurahi ukilizingatia hilo!”
“Sitomwambia, hilo nakuahidi!”

Kabla ya mama Richard hajatoka nje, aliombwa asubiri kidogo ili aitwe mzee Nzasa ambaye alitoka na kumsindikiza pamoja hadi nje. Huko nje mama yake Dina alionyesha unyenyekevu uliopitiliza kwa mama Richard na kumwombea kwa kumtaja Yesu kila baada ya muda kabla ya mama
Richard hajaingia kwenye gari.
Mama Richard alipokuwa akiondoka na gari lake, mama Dina aliipunga mikono yake yote miwili kwa furaha yenye unyenyekevu.

* * * * *

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA NNE

Hali ikabadilika ghafla. Mama Dina alijikuta akiwa ananyenyekea kama kijakazi mbele ya nokoa na hata pale mama Richard alipoaga, ilibidi mama Dina kutaka kwenda kumuita Dina ili aje kumsalimia.

“Hapana usimsumbue mtoto, mwache apumzike. Lakini kitu kimoja mama Dina,” mama Richard alisema kwa utulivu. “Habari hizi za kazi usimgusie kabisa Dina, usimwambie kama kuna kazi ninayomtafutia. Na sitaki ajue kama ni mimi ndiye ninayemtafutia. Na endapo kama atajua, ama kwa kumwambia wewe mwenyewe au kuambiwa na mtu mwingine yeyote, mama Dina itabidi unisamehe, ujue sitohangaika kumtafutia kazi mwanao! Naomba hilo ulizingatie. Please usimwambie!”

“Kwa jina la Yesu Kristo Msalabani, sitamwambia!” “Nitafurahi ukilizingatia hilo!”

“Sitomwambia, hilo nakuahidi!”

Kabla ya mama Richard hajatoka nje, aliombwa asubiri kidogo ili aitwe mzee Nzasa ambaye alitoka na kumsindikiza pamoja hadi nje. Huko nje mama yake Dina alionyesha unyenyekevu uliopitiliza kwa mama Richard na kumwombea kwa kumtaja Yesu kila baada ya muda kabla ya mama Richard hajaingia kwenye gari.

Mama Richard alipokuwa akiondoka na gari lake, mama Dina aliipunga mikono yake yote miwili kwa furaha yenye unyenyekevu.

* * * * *

“Nimekwisha kummaliza!” mama Richard alimwambia mzee Ken wakati alipokuwa akimwelezea kuhusu mazungumzo yake na mama Dina yalivyokwenda. “Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kumwajiri na kumpa kazi itakayomuweka karibu na Richard na Richard ataitumia nafasi hiyo kumshawishi Dina asiolewe na badala yake amuoe yeye!”

“Usitegemee jambo hilo litafanyika kwa haraka kama unavyozungumza!” mzee Ken alionya huku akiwa ndani ya vazi la pajama akiwa amelala kitandani kama ilivyokuwa kwa mkewe.

“Lipi? La kumwajiri? Au la kumshawishi?” mama Richard aliuliza kwa sauti iliyoonyesha kushituliwa na kauli ya mzee Ken.

“La kumshawishi Dina hadi akubali,” mzee Ken alijibu akiwa amelala chali. “Lazima litachukua muda hadi kufanikiwa. Na endapo itakuwa hivyo, ujue uwezekano wa Dina kuolewa na huyo mchumba wake mara tu baada ya kupata kazi utakuwepo. Utakuwepo kwa sababu kikwazo kilichokuwa kimeisimamisha ndoa yao

kitakuwa hakipo tena! Kwa hiyo, ipo hatari ya ndoa hiyo kufanyika wakati Richard akiwa bado hajafanikiwa kumshawishi Dina kuizuia ndoa hiyo!”
“Ken, lazima itumike mbinu kumzuia Dina asiolewe na huyo mchumba wake!” mama Richard alisema kwa sauti kavu.
“Kivipi?” mzee Ken aliuliza kwa sauti ya upole.
“Mbinu ni hii Ken; utakapomwajiri Dina, umpe barua itakayomuweka chini ya uangalizi wa miezi mitatu hadi ajira yake itakapothibitishwa,” mama Richard alisema. “Barua hiyo itatoa masharti atakayoyasaini, na moja ya masharti hayo ni kuwa, kwa kipindi hicho cha miezi mitatu atakachokuwa anaangaliwa utendaji wake, hakutakuwa na ruhusa ya dharura atakayopewa itakayozidi siku moja labda itokee kuwe na msiba wa kifo cha mmoja wa wazazi wake, kaka au dada wa kuzaliwa naye! Sharti hilo litambana ashindwe kuomba ruhusa kwa ajili ya kwenda kufunga ndoa!”

“Usisahau kuwa, umekwisha kujenga ukaribu na mama yake na anaweza akautumia ukaribu huo kuja kumwombea mwanae apatiwe ruhusa ya kwenda kuolewa!”

“Hapo ndipo atakapokosea! Nitaitumia nafasi hiyo kumweleza umuhimu wa kazi ya mwanae kimaisha, na nitamshawishi na lazima atashawishika kukubali kuliahirisha suala la ndoa hadi baada ya miezi mitatu aliyopewa mwanae imalizike. Nina hakika kwa mshahara utakaokuwa unampa Dina, kamwe hatokubali kuilaani bahati hiyo.”

“Kuna umuhimu wa Richard kuambiwa kusudio hilo?”

“Hapana, kwa sasa asiambiwe! Ataambiwa baada ya Dina kuajiriwa.” “Na ikimalizika miezi hiyo mitatu huku Dina akiendelea na msimamo wake wa kukataa kuolewa na Richard, hapo itakuwaje?” “Ikatishe ajira yake!”

* * * * *

Mawasiliano kati ya mama Richard na mama Dina yakaendelea bila ya watoto wao kufahamu, huku mmoja akiijua njama anayoifanya dhidi ya mwenzake, mwingine akiwa haijui njama anayofanyiwa na mwenzake!

Baada ya wiki moja, zengwe la mama Richard likawa limekamilika, na ulipofika usiku akampigia simu mama Dina!
“Mwambie Dina, kesho asubuhi saa nne awe ofisini kwa mzee Ken,” mama Richard alimwambia mama Dina kwenye simu na kumwelekeza ilipo ofisi yenyewe. “Aende na vyeti vyake vya shule. Akifika mapokezi aseme ameitwa na mzee Ken.”
“Nitamwambia usiku huu aanze kuvitafuta vyeti vyake!” mama Dina alisema kwa sauti iliyonyenyekea.
“Yeye akifika mwambie ajitambulishe kwa mzee Ken kuwa ni mtoto wa mzee Nzasa.”
“Nitamwambia dada, kwa kweli nakushukuru sana.” “Haina tabu. Haya usiku mwema.”
“Nawe pia. Yesu akubariki mama Richard!”
“Amen.”

****

RICHARD alikuwa amesimama, mgongo wake ukiwa umeelekezwa mlangoni wakati alipokuwa

akizungumza na msichana mfanyakazi anayefanya kazi idara ya mapokezi kwenye kampuni ya mzee Ken. Richard aliyekuwa amemsindikiza mgeni wake aliyemtoa hadi hapo mapokezi na kuagana naye sekunde chache zilizopita, lakini kabla hajarudi tena ofisini kwake, akakumbuka kuwa, asubuhi hiyo magazeti aliyokuwa ameletewa ofisini kwake yalikuwa pungufu.

“Leo sijaliona gazeti la Flames likiletwa ofisini kwangu, wewe unalo hapo kwako?” Richard alimwuliza msichana huyo wa mapokezi.
“Mtu wa magazeti leo kaleta hilo moja tu la Flames, na limepelekwa kwa Mkurugenzi,” msichana wa mapokezi alijibu.
Wakati msichana yule alipokuwa akijibu, mlango wa kuingilia hapo mapokezi uliotengenezwa kwa kioo ukasikika ukifunguliwa. Macho ya yule msichana yakavutika kuuangalia mlango huo, kitendo hicho nacho kikamvuta Richard aangalie mlangoni.

Wakamwona Dina akiingia!

Kitendo cha kuonana kati ya Dina na Richard kikawa kimewaletea mshituko wote wawili na kuonyesha dhahiri hakuna yeyote aliyetarajia kukutana na mwenzake eneo hilo huku Dina akionyesha wazi kabla ya hapo alikuwa hajui kama Richard alikuwa akifanya kazi kwenye kampuni hiyo!

Tukio la kumwona Dina akiingia kulimfanya Richard agande kwa sekunde chache huku akiwa hayaamini macho yake kama aliyekuwa akimwangalia alikuwa kweli ni Dina. Akili yake kwa sekunde hizo chache ilikuwa kama iliyokuwa imepooza, ikashindwa kuwaza kwa haraka. Akabaki akiwa ameduwaa huku akimwangalia Dina ambaye naye alikuwa akimwangalia. Ndipo Richard akakumbuka tukio lililoufanya moyo wake uzidi kupata pigo…

Aliikumbuka kauli aliyoambiwa na Dina mara ya mwisho walipokutana nje ya duka linalouzwa simu, kauli iliyomtaarifu kuwa, Dina na John Sailas wanatarajia kufunga ndoa wakati wowote!

* * * * *

Richard alikuwa akimfahamu John Sailas, wote waliwahi kusoma shule moja ya Azania, walikutana wakiwa kidato cha kwanza na wakawa darasa moja. Hawakuwa na ukaribu wa kuitwa marafiki, lakini walikuwa na ukaribu wa kuwa wanafunzi waliosoma darasa moja. Walisoma wakiwa pamoja kwa muhula mmoja pekee. Muhula wa pili, Richard alihamishiwa shule nyingine nchini Kenya.

Kwa upande mwingine ujuano wa kujuana kati ya Richard na Dina ulikuwa ni wa muda mrefu. Walijuana tokea wakiwa wadogo kutokana na kuishi eneo moja na mitaa yao ilikuwa jirani. Wakati Richard alipokuwa kidato cha kwanza, Dina alikuwa darasa la sita. Mwanzo wa Richard kuanza kumtongoza Dina kilikuwa ni kipindi Richard alichokuwa amerudi likizo kutoka nchini Kenya wakati huo akiwa kidato cha tatu na Dina akiwa ameingia kidato cha kwanza.

Kupoteana kwao kulikosababishwa na Richard kusoma nchini Kenya, kulimfanya Richard ayashangae mabadiliko ya ghafla ya kimwili yaliyomtokea Dina baada ya yeye Richard kurudi nchini kwa ajili ya likizo. Richard alimwona Dina kama aliyekua haraka kimaumbile. Umbile zuri la kike lililokuwa limejichomoza kwa kuvigawa viungo vya Dina kwenye hesabu sahihi, kulimfanya Richard aingiwe na hisia za matamanio ya

mapenzi dhidi ya jirani yake huyo.

Uzuri wa Dina na umbile lake hilo lililoanza kutatanisha wanaume wengine lilimfanya Richard awe na wakati mgumu wa kushindwa kuzificha hisia zake na kujikuta kama mtu anayepigwa na shambulizi la ghafla kila alipokuwa akikutana na Dina njiani. Akashindwa kujizuia, akaamua kumkabili Dina na kumpa yake kauli.

Dina akamkataa!

Richard hakukata tamaa. Akabuni mbinu mpya ambayo kwa upande mwingine ilikuwa kama ya kitoto; mbinu ya kulitumia jina la baba yake. Akawa anamwomba Dina aende naye nyumbani kwao na kumwambia kuwa, baba yake angefurahi sana kama angemwona naye. Richard alikuwa akiamini kama Dina angeukubali mwito huo wa kwenda nyumbani kwao, ule ufahari wa kimaisha ulioenea kila sehemu ya nyumba yao ungekuwa ni chachu kuu ya kumfanya Dina amkubali kirahisi. Hata hivyo, Dina hakulikubali karibisho hilo!

Si kwamba Dina alikuwa hamjui baba yake Richard, alikuwa akimjua vizuri sana mzee Ken kuwa ndiye baba yake Richard, na utajiri wa mzee huyo ulikuwa ukijulikana na kila mtu kwenye kila kona ya maeneo hayo wanayoishi. Hata hivyo, sababu iliyomfanya Dina kumkataa Richard ilitokana na Dina kujiona ndio kwanza ameanza masomo ya Sekondari na alikuwa amepania afike mbali kimasomo, hivyo hakuwa tayari kujiingiza katika mapenzi na mwanamume yeyote.

Hatimaye Richard aliondoka na kwenda masomoni Uingereza baada ya kufanikiwa kupata chuo, lakini aliondoka akijijua ana deni la kuja kuhitimisha dhamira yake aliyoiwekea nadhiri kuwa lazima aje kumpata Dina kimapenzi wakati atakaporudi likizo.

Likizo yake ya kwanza ilipowadia, Richard alirudi nchini akiwa na matumaini tele ya kumpata Dina. Alirudi akiwa amebadilika tabia. Akawa mtu wa kunata na kujisikia huku akionyesha kuuhusudu Uzungu kupitiliza. Katika siku za mwanzoni mwa likizo yake alidhani kule kusoma kwake nchini Uingereza kungemfanya Dina ampapatikie na angeweza kumpata kirahisi. Lakini Dina hakuwa hivyo! Dina aliendeleza msimamo wake uleule wa kuhakikisha Richard hampati!

Kengele ya hadhari ikalia kichwani mwa Richard, akagundua kumbe ujivuni ungemharibia mambo. Akajibadili kutoka kwenye tabia ya ujivuni na kuingia kwenye tabia ya kuwa mpole, akawa mnyenyekevu mbele ya Dina. Akaepuka kuzungumza stori za mapenzi kila alivyokuwa akikutana naye. Akaanza kuzungumza stori za matukio ya kusisimua yaliyopo na yaliyotokea nchini Uingereza. Stori hizo zenye mchanganyiko wa kutoka kwenye matukio halisi na historia nyingine za kuvutia alizokuwa akiziangalia kutoka kwenye dokumentari tofauti za vipindi vya kwenye runinga huku akimudu kuvielezea kwa ufasaha, vikaonekana kumwingia na kumvuta Dina.

Hali ikabadilika ghafla, Dina akaanza kuyafurahia mazungumzo hayo kila alipoonana na Richard. Ukaribu wao ukazidi, na Richard akajaribu kuitumia tena nafasi hiyo kumtaka Dina afike nyumbani kwao, lakini Dina hakuwa tayari kwa hilo. Hata hivyo, mkaa pamoja na waridi hunukia waridi. Ukaribu huo ukaanza kuleta mabadiliko, mwelekeo wa kuelekea kwenye mapenzi ukaanza kimya kimya. Ikafikia mahali ikawa halahala mti na macho! Richard akakaribia kidogo afanikiwe kumpata Dina kimapenzi.

Tukio hilo lilianzia usiku wakiwa pamoja nje ya nyumba ya akina Dina, walikuwa peke yao kwenye eneo hilo walilokuwa wakipenda kuonana na kuzungumza stori zao. Richard akazungumza neno lililomfurahisha Dina, Dina akajikuta akicheka na kukiegemeza kichwa chake kwenye bega la Richard. Ghafla Richard akapata akili ya kujaribu bahati yake, akauzungusha mkono wake kwenye shingo ya Dina na kumkumbatia. Akaunamia uso wa Dina na kuonyesha dhahiri alikuwa na lengo la kuubusu mdomo wa Dina. Mungu si Adam, akaishikia siku ya Richard kwa Richard kujikuta akinyonyana ndimi na Dina bila ya bishano la aina yoyote.

Siku hiyo Richard hakuiamini bahati hiyo! Hata alivyokwenda kulala, usingizi ulikataa kuja mapema, muda mrefu alijikuta akilifikiria tendo hilo na kuwa kama gurudumu la santuri ya video iliyokuwa ikijirudia wakati wote!

Lakini bahati hiyo ikaja kuharibiwa na marafiki zake ambao ni watoto wa matajiri kama alivyo yeye. Badala ya kuendelea na mkakati wa kutulia uliomletea matunda kwa Dina, Richard akaanza kukosa utulivu. Marafiki zake wakaanza kumyumbisha kwa kumfuata nyumbani kwao na kwenda naye kwenye madisko. Ikawa leo huko, kesho kule. Mara kwenye fukwe za bahari, mara wako na wasichana hawa, kesho wale. Dina akazishitukia tabia za Richard za kubadilisha wasichana, hata hivyo akaamua asimlalamikie Richard jambo hilo.

Aliamua asimlalamikie kwa sababu hakuuona ulazima huo! Ukaribu wao haukuwa mzito hivyo, hata kile kitendo cha faragha kilichofanyika kati yao cha kunyonyana ndimi zao hakikuwa kimemwumiza kutokana na kuwa, kilifanyika mara moja!

Dina hakukubali tena kukirudia kitendo hicho kila walipokuwa pamoja. Akawa amembadilikia ghafla Richard! Akaanza kumkwepa Richard kila Richard alivyokuwa akiomba kuonana naye na hata wakati walivyokuwa wakionana, Dina hakuwa tayari tena kukubali kusimama eneo lolote la faragha. Akawa anampa picha ya wazi Richard kumwonyesha kuwa, sasa ule ukaribu uliokuwa ukihitajiwa kati yao haukuwa na umuhimu tena! Richard akaanza kumlalamikia Dina kuwa amebadilika ghafla, hata hivyo Dina aliamua kutompa sababu ya kwa nini alikuwa akifanya hivyo!

Kugundua kuwa alikuwa hatakiwi na Dina kulianza kumchanganya Richard, lakini kilichomchanganya zaidi ni kule kutoijua sababu iliyomfanya Dina auchukue uamuzi huo wa ghafla wa kumkataa pasipo kumtamkia. Matumaini ya uhusiano wao baada ya tukio la kuzikutanisha ndimi zao akayaona yakiteleza mikononi mwake huku juhudi za kuzuia zikipoteza dalili zote.Hapo ukawa mwanzo wa Richard kugundua kile alichokuwa hakijui mwanzoni kuwa, kitendo cha kukataliwa na Dina kilikuwa ni jambo lisilokubalika kwake!

Mapenzi ya kumpenda Dina yalikwisha kumuingiza kichwa kichwa kiasi cha kujiona hawezi akajitoa! Ukawa ni mshituko ambao hakuutarajia, likawa ni pigo kwake kukataliwa baada ya kupenda! Akajaribu kuomba aina yote ya misamaha, lakini Dina hakuonyesha dalili ya kurudi nyuma kwenye uamuzi wake!

Wakati akiwa kwenye jitihada zote za kutaka kulirudisha tena penzi kwa Dina, likizo nayo iliyokuwa ikimuweka nchini ikaisha. Richard akarudi Uingereza bila ya mafanikio ya kuurudisha tena uhusiano wake na Dina!

* * * * *

****DINA ndani ya ofisi moja na RICHARD..mpenzi wake wa utotoni…nini kitaendelea??

****Je? Ile mbinu ya Mama Richard itazaa matunda.
***Ndoa ya John na Dina…na vipi hatma ya Judy???
**NI VITA KATI YA PESA, MAPENZI NA WIVU!!!

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA TANO

Mapenzi ya kumpenda Dina yalikwisha kumuingiza kichwa kichwa kiasi cha kujiona hawezi akajitoa! Ukawa ni mshituko ambao hakuutarajia, likawa ni pigo kwake kukataliwa baada ya kupenda! Akajaribu kuomba aina yote ya misamaha, lakini Dina hakuonyesha dalili ya kurudi nyuma kwenye uamuzi wake!

Wakati akiwa kwenye jitihada zote za kutaka kulirudisha tena penzi kwa Dina, likizo nayo iliyokuwa ikimuweka nchini ikaisha. Richard akarudi Uingereza bila ya mafanikio ya kuurudisha tena uhusiano wake na Dina!

* * * * *

Kurudi kwake Uingereza kukaonyesha ni namna gani alivyokuwa amechanganyikiwa na penzi lililovurugika. Tukio la kunyonyana ndimi na Dina likaendelea kuleta jinamizi lisiloisha kwake. Richard akaanza kupiga simu za mara kwa mara hasa usiku kutoka Uingereza kumpigia Dina. Alibembeleza na kulalamika huku akimsihi Dina amweleze sababu ya kumgeuzia kibao.

Dina hakuonyesha hasira wala kinyongo wakati wote alipokuwa akizipokea simu za Richard, alimsikiliza Richard alivyokuwa akihangaika na maneno, na mwisho wa mazungumzo yao Dina aling'ang'ania msimamo wake wa kutomwambia Richard sababu ya kumkataa, zaidi ya kumwambia, "Niliamua tu iwe basi!"

Ikawa ni kauli iliyomtesa Richard wakati wote. Umbali uliokuwepo kati yake na Dina ukawa ni kikwazo kingine, akawa anatamani arudi nchini angalau kungemuwezesha kuonana na Dina na kuyaweka mambo sawa na pengine fursa hiyo ingempa nafasi ya kukijua kile kilichomfanya Dina amkatae ghafla. Hata hivyo mawazo yake hayo yakabaki kuwa ni jambo lisilowezekana kutekelezeka kwa ukweli kuwa, asingeweza kurudi Tanzania na kuacha masomo.
Baada ya kukiri asingeweza kurudi nchini, ndipo Richard alipojaribu kuicheza karata yake ya mwisho kwa kumuahidi Dina pindi atakapomaliza masomo yake nchini Uingereza na kurudi nyumbani, jambo la kwanza ambalo angelifanya ni kumuoa!
Karata hiyo nayo, Dina akaitolea nje!

Richard akanyoosha mikono kusalimu amri akiwa London!

* * * * *

Baada ya kukaa Uingereza na kumaliza masomo yake, Richard alirudi nchini akiwa na Shahada yake. Ujio wake wa kurudi nchini, haukumshitua Dina. Richard akalielewa hilo, likamwumiza moyoni. Hata hivyo, akajaribu tena bahati yake kwa kuonana na Dina na kumlia kiapo kuwa ahadi ya kumuoa aliyoiahidi ilikuwa ni ya dhati na angekuwa tayari hata kwenda kujieleza kwa wazazi wake Dina kuhusu kusudio lake hilo. Dina akapangua tena!

Ndipo Richard alipoamua kuanzisha urafiki na Judi!

Aliuanzisha uhusiano na Judi kwa sababu alikuwa akijua Judi na Dina walikuwa wakifahamiana! Wasichana hao wawili walikuwa na historia iliyokuwa ikifanana kidogo na ile ya Richard na John. Hao nao waliwahi kusoma shule moja kama ilivyokuwa kwa John na Richard. Tofauti iliyokuwepo kati yao ni kuwa Judi na Dina wao walisoma pamoja kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kabla ya kuachana huku kila mmoja akienda kumalizia masomo ya kidato cha tano na cha sita kwenye shule tofauti. Kwa fikra za

Richard alizokuwanazo, alifikiri urafiki aliouanzisha na Judi ungeweza kumwumiza Dina na aliamini ingekuwa ni sehemu ya kulipiza kisasi chake kwa yale ambayo Dina alimfanyia!
Kwa upande wa Judi, pamoja na kukubali kuwa rafiki wa kike wa Richard, lakini yeye alikuwa haijui nasaba yoyote iliyokuwepo kati ya Richard na Dina. Hata hivyo, Dina alikuja kujua baadaye kuwa Richard ameanzisha uhusiano wa mapenzi na Judi. Ingawa taarifa hizo hazikumwumiza lakini kwa kiasi fulani zilimkera.

Kwa kuwa lengo lilikuwa ni kumwumiza Dina, Richard alipokuja kujua kuwa Dina alikuwa akiufahamu uhusiano uliopo kati yake na Judi, kinadharia akajiona tayari ni mshindi! Jambo hilo likamfanya Richard kuuimarisha uhusiano wake na Judi kwa kwenda naye kila mahali na kumtambulisha kwa kila mtu aliyekuwa akimfahamu huku akiamini uhusiano wao huo ungeleta gumzo jijini Dar na wangekuwa mfano wa watu wapendanao. Akawa na hakika sifa hizo zingemfikia Dina, na aliamini zingemchoma na kumwumiza kama alivyoumizwa yeye na Dina! Uamuzi wake huo wa kujenga uhusiano na Judi akategemea ingekuwa ni fimbo pekee ya kumwadhibu nayo Dina ili ajutie nafasi aliyoichezea!

Richard akaanza kuamini ushindi ulikuwa ukienda upande wake baada ya kubaini habari za uhusiano wake na Judi zilikuwa zipo kwenye kilele cha kuzungumzwa na watu tofauti na hasa wale wa daraja lao. Isitoshe, wengine wakawa wanazizidisha kwa kutia chumvi kwa kutangaza kuwa, wawili hao wangeoana!

Richard akaridhika kuwa amemkomoa Dina, lakini pia, akafanikiwa kumuondoa Dina kwenye fikra zake huku nafsi yake ikiridhika kuwa ameweza kulipiza kisasi. Pamoja na kuamini kuwa ameweza kuitimiza nadhiri ya kumwumiza Dina na yeye mwenyewe kuanza kuusahau ule ulazima wa kumwona Dina ni sehemu muhimu ya maisha yake, lakini bado alikiri kwenye moyo wake kuwa, adhabu aliyoipata na kuitumikia kutoka kwa msichana huyo ilikuwa kubwa na iliyomwumiza mno. Akajionya kuwa, mara nyingine asifikie kumpenda mwanamke mwingine kama alivyompenda Dina ambaye amemuachia kovu kwenye moyo wake lililosababishwa na jeraha la kupenda!

Lakini akiwa ndani ya imani hiyo ya kuwa ameweza kuitekeleza nadhiri yake, ghafla pasipo mategemeo Richard akajikuta akiingia kwenye mshituko mwingine asioutarajia pale alipobaini kuwa, kovu hilo lililoachwa na Dina moyoni mwake, kumbe kidonda chake kilikuwa bado kibichi na kilikuwa mbali na unafuu wa kupona.

Utambuzi huo ulikuja kama siku mbaya kwake, siku ya mwishoni mwa wiki aliyokuwa akiifurahia akiwa na Judi. Ilikuwa siku ya Jumapili!
Siku hiyo alikuwa akiisheherekea mapumziko ya juma la mwisho akiwa na Judi wakiwa kwenye hoteli ya BBH iliyopo nje ya jiji kandoni mwa fukwe ya bahari. Ilianzia wakati Richard akiwa anatoka chooni akimrudia Judi aliyekuwa amemuacha ufukoni akipunga upepo. Choo alichokuwa ametoka kukitumia kilikuwa karibu na bwawa la kuogelea, na alipokuwa akirudi aliamua kuitumia njia nyingine tofauti na ile aliyoitumia awali kuendea chooni. Njia hii aliyoamua kurudi nayo ilipita karibu na hilo bwawa, tofauti na ile ya mwanzo ambayo ilipita mbali na bwawa na pia ilikuwa ya mzunguko hadi kufika chooni.

Ghafla wakati alipokuwa akirudi kutoka chooni, Richard akamwona John Sailas! John alikuwa amevaa bukta pekee mwilini iliyolowa maji kuonyesha muda mfupi uliopita alikuwa akiogelea, alikuwa akitokea kwenye baa akiwa amezibeba glasi mbili za vinywaji vya aina moja vyenye rangi ya kijani ambavyo alihisi ni kinywaji aina ya Crème de Menthe vilivyotumbukizwa barafu iliyosagwa. Kitendo cha kumwona John

kikamfanya kutaka kumuita, na sababu ya kutaka kumuita ni kwamba walikuwa hawajaonana kwa kipindi kirefu kidogo. Akasita kuitekeleza dhamira yake hiyo ya kumuita baada ya kumwona msichana aliyekuwa hatua kadhaa mbele huku mgongo wa msichana huyo ukiwa umeelekea kwake akiwa amekaa kwenye kingo za bwawa la kuogelea na nywele zake zikiwa zimelowa huku miguu yake ameitumbukiza kwenye maji. Msichana huyo alikuwa amevaa bikini ya kuogelea ambayo ni chupi na sidiria akiwa amegeuka kuangalia nyuma na kutabasamu baada ya kumwona John.

Richard alisimama ghafla baada ya kugundua msichana aliyekuwa akimwangalia alikuwa ni Dina! Bila ya kukusudia kuufanya uamuzi huo, Richard alijikuta akirudi kinyume nyume kama aliyekuwa ameona jambo la hatari. Akabadili njia huku akiendelea kumwangalia Dina alivyokuwa akimpokea John glasi yenye kinywaji, kisha John akajiunga kukaa pembeni mwa alipokaa Dina, naye miguu yake akaitumbukiza majini kuwakabili kuwaangalia watu waliokuwa wakiogelea. Kitendo cha John kukaa karibu na Dina kukayafanya mabega yao yagusane, Dina akatumia bega lake kuligonga bega la John kiushikaji. Kitendo hicho hakikuwa na nguvu iliyotumika, lakini John akafanya igizo kama aliyekuwa amesukumwa kwa nguvu. Akayumba kidogo kuonyesha ameyumbishwa na msukumo wa bega la Dina, kisha akamwangalia Dina aliyekuwa akimwangalia kwa ncha za macho yake huku akitabasamu. John naye akatabasamu, kisha wote wawili wakazikutanisha papi za midomo yao na kubusana kwa mara moja.
Tukio hilo likamuacha Richard kwenye maumivu yaliyomchanganya kichwa. Ilikuwa ni vigumu kwake kusadikisha yanayotokea ni sehemu ya mkanganyiko wa mawazo yanayomjengea taswira zisizokuwepo kutokana na jinamizi la kuachwa na Dina, au yupo ndotoni akiiota ndoto hiyo!
Yote aliyoyaona aliyapinga kwa kuamini hayakuwa kwenye ithibati ya matukio ya kweli. Hakukubali kukiri kama aliyemwona ni John Sailas na yule aliyekuwa naye ni Dina. Pili, hakukiamini kile kilichokuwa kinamdhihirishia kichwani mwake kuwa, endapo ni kweli hao aliowaona ni John Sailas na Dina, basi kinachomdhihirishia hapo ni kwamba watu hao ni wapenzi, tena ni wapenzi wa muda mrefu!

Akakubali kujiondoa kwenye uhayawani wa kuukataa ukweli unaotokea mbele yake, akakiri hayuko ndotoni na anayoyaona ni ya kweli! Lakini pia hakujua kilichokuwa kikimwumiza. Ni kule kumwona Dina akiwa na bwana mwingine? Au ni kumwona Dina akiwa na John Sailas? Akagundua kilichokuwa kikimwumiza ni kugundua John Sailas ni bwana wake Dina! Awali alitarajia kitendo chake cha kumchukua Judi na kumfanya rafiki yake wa kike kingemfanya Dina alipize kisasi kwa kumtafuta bwana wa uhakika na mwenye uwezo kama aliokuwa nao yeye. Kamwe hakutarajia Dina na uzuri aliokuwa nao angeweza kumkubali mtu kama John Sailas mwenye maisha ya kawaida yanayoendeshwa kwa kutegemea ajira yenye kipato cha wastani! Richard aliishiwa nguvu, akashusha pumzi na kusikitika
peke yake. Akarudi alipokuwa amemuacha Judi.

Kero la aina ya maisha aliyonayo John bado liliendelea kumsulubu Richard. Alimshangaa Dina kumkubali mtu mwenye kumiliki usafiri wa pikipiki. Akailinganisha tofauti iliyokuwepo kati yake na John. Yeye alikuwa ni mtoto wa tajiri mwenye kuuchezea utajiri wa baba yake unaompa umiliki wa kubadilisha magari ya kifahari muda wowote anaotaka. Isitoshe pia, ni mrithi mtarajiwa wa mali za baba yake pindi akifariki. Alikwisha kuonana na John Sailas barabarani zaidi ya mara tatu wakati yeye akiwa anaendesha gari lake la kifahari na John akiwa na pikipiki yake akiwa amekifunika kichwa chake kwa kofia ngumu ya helmeti. Utofauti huo wa kimaisha, Richard aliuona ungempa moja kwa moja turufu ya ushindi kwenye vita hiyo ya mapenzi, lakini haikuwa hivyo! Ni John Sailas ndiye aliyeonekana ni mshindi!

Lilikuwa pigo kwa Richard, pigo lililomuanzishia kumchukia John na kumwona ni adui yake namba moja.

Hakuamini mtu mwenye maisha aina ya John Sailas anaweza akamshinda. Fikra hizo zikamuweka kwenye ubishi wa kutokubali kushindwa. Akaamini, endapo safari hii kama ataianzisha tena vita ya kumrudisha Dina mikononi mwake angeweza akafanikiwa nayo. Alihisi kulikuwa na dosari ndogo aliyokuwa ameifanya kwenye kumwongoza Dina wakati mtafaruku wao ulipotokea. Hakuijua dosari hiyo, lakini aliamini ilikuwa ni ndogo ambayo anaweza akaisawazisha. Vinginevyo, Dina asingeweza amuache yeye aliyezungukwa na utajiri, kisha akamfuata mtu kama John Sailas ambaye alimwona kama mbabaishaji wa maisha!

Tukio hilo la kumwona John Sailas akiwa na Dina, Richard alilichukulia kama tusi na fedheha kwake, lakini pia akalifanya ni changamoto kwake. Hakutaka kuamini mtu kama John anaweza akawa na ubavu wa kumnyang'anya msichana kama Dina! Akajiapiza lazima arudi kwenye vita ya kumrudisha Dina mikononi mwake! Tukio hilo likaendelea kumtesa, akakosa amani. Kwa mara ya kwanza alijikuta akikiri kuwa, uamuzi wake wa kumchukua Judi kama njia ya kumkomoa Dina ilikuwa sawa na hakuna alichokifanya!

Richard akaapa, piga ua lazima amrudishe tena Dina mikononi mwake kwa gharama yoyote!

Siku chache baada ya tukio hilo kutokea, ndipo Judi alipomwuliza Richard kuhusu kufunga ndoa kwao. Likawa ombi lililokwishachelewa kutolewa! Akili ya Richard ilikuwa imetekwa upya na penzi la Dina huku akijitangazia vita dhidi ya John Sailas!

* * * * *

Richard akaingia rasmi vitani kumsaka Dina, lakini haikuwa rahisi kwa kumvizia barabarani. Kwa mara ya kwanza alijikuta akijilaumu kwa uamuzi wake wa awali wa kuifuta namba ya simu ya Dina siku chache baada ya kuanzisha urafiki na Judi. Kukosekana kwa namba ya simu ya Dina kukawa ni tatizo jipya kwake. Richard akawa hana mtu wa karibu ambaye angemwezesha kuipata namba hiyo kwa urahisi.

Uwezekano pekee ambao ungemwezesha kuonana na Dina kirahisi ni kwenda nyumbani kwao Dina. Wazo hilo alilipinga moja kwa moja, aliuona ni uamuzi wa kujirahisisha na ungetoa nafasi kwa Dina kujiweka kwenye ujivuni usio na lazima pale ambapo angemwona amekuja nyumbani kwao kwa ajili ya kubembeleza penzi. Kikwazo hicho kikamuweka Richard kwenye wakati mgumu wa kuweza kuonana na Dina. Siku zikaanza kupotea huku kila siku Richard akihaha kutafuta njia ya kuonana na Dina.

Mara nyingi ukiomba kwa dhati huwa unapewa. Mungu akampa Richard bahati hiyo ya kuonana na Dina. Walionana bila ya kutarajiana. Ilikuwa wakati Richard akikatiza kwa nje kwenye duka linalouzwa simu lililopo katikati ya jiji. Akiwa anaukaribia mlango wa duka hilo kwa nia ya kuupita ili aendelee na safari yake, ndipo Dina akawa anatoka kutoka kwenye duka hilo. Wote wawili wakashituka.

"Dina!" Richard aliita kwa uchangamfu uliokuwa hauna nguvu sana. Aliogopa kujiamini moja kwa moja.
Dina alitabasamu na kusema, "Hai, Richard!"
"Za siku nyingi?"
"Poa. Zako?"
"Zangu mbaya."
"Kwa nini?"
"Sikutarajia kunikataa kwako kukufanye unichukie hivi Dina. Umekuwa sio mtu wa kunitafuta kwa simu japo

kwa kusema heloh?”

“Unanilaumu mimi wakati wewe mwenyewe unafanya kitu hicho hicho?”

“Mimi nataka sana kukupigia Dina, lakini naogopa kutonesha jeraha ulilonialachia moyoni. Ukweli ni kwamba bado nakupenda Dina.”

“Sio vizuri Judi akikusikia ukisema kauli kama hiyo kwangu.”
“Judi siko naye tena!”

“Eti unasemaje Richard?”
“Tumeachana!”
“Kwa nini?
“Ukweli ni kwamba bado hajapatikana mtu wa kuiziba nafasi yako. Bado nakupenda Dina!”
Kauli hiyo ikamfanya Dina atoe kicheko cha kama aliyeguna.
“Ina maana huna habari?” alisema.

Richard akaonyesha kushangaa kidogo.
“Habari ipi?” aliuliza.

Ndipo Dina alipomweleza Richard kuwa, anatarajiwa kuolewa na John Sailas siku chache zijazo! Taarifa hizo zikawa zimemmaliza Richard!
Akiwa bado hajayaponya majeraha yaliyotoneshwa upya, wiki mbili baadaye Richard anashangaa kumwona Dina akiwasili kwenye ofisi za kampuni ya baba yake!.....

**RICHARD amegundua kuwa kulipiza kisasi katika mapenzi hakusaidii bali kunaumiza zaidi…ameaamua kupigania moyo wake unapomuelekeza….moyo unamtaka DINA!!!

***Dina yupo katika hatua za mwisho za kutolewa mahali na JOHN SAILAS….je mpango huu utafanikiwa???

**RICHARD kijana wa kitajiri ametangaza rasmi vita ya mapenzi dhidi ya John SAILAS.

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA SITA

Akiwa bado hajayaponya majeraha yaliyotoneshwa upya, wiki mbili baadaye Richard anashangaa kumwona Dina akiwasili kwenye ofisi za kampuni ya baba yake!

LILIKUWA kama shambulizi la ghafla walilofanyiana. Wote wawili, Dina na Richard walitumia takriban sekunde mbili au tatu kushangaana huku wakitazamana bila yeyote kati yao kutamka neno.

“Dada karibu,” msichana wa mapokezi alisema huku akimwangalia Dina na wakati huo huo akiiba kumwangalia Richard aliyekuwa bado ameduwaa akimwangalia Dina.

“Ahsante,” Dina alisema na kuonyesha kuondoka kwenye mshangao uliompata.
“Nadhani ni mgeni wangu!” Richard alimwambia msichana wa mapokezi kabla ya msichana huyo hajaanza kumhoji Dina.
“Karibu Dina.”
“Nimekuja kumwona mzee Ken,” Dina alisema huku akimwangalia Richard.
Richard akaonyesha kidogo kupigwa na butwaaa.
“Karibu yupo,” alisema kabla hajatekwa na butwaa lake.
“Anajua kama utakuja?”
“Anajua,” Dina alijibu.

“Twende nikupeleke ofisini kwake,” Richard alisema na kuuweka mkono wake mgongoni mwa Dina na kuondoka naye.
Walifika ofisini kwa Katibu Muhtasi na Richard alimtambulisha Dina kuwa ni mgeni wa Mzee Ken, kisha akamwongoza Dina hadi mlangoni mwa ofisi ya mzee Ken. Aliugonga mlango na kuufungua, akamwingiza Dina na kusema huku akimwangalia mzee Ken, “Mgeni wako!” kisha baada ya kusema hivyo alitoka na kuufunga mlango.

Mazungumzo kati ya mzee Ken na Dina yalichukua takribani dakika kumi na tano hadi ishirini. Dina akafahamishwa kazi ambayo angeajiriwa, akaikubali.

“Nitakulipa mshahara wa shilingi laki nane na nusu ukiwa chini ya uangalizi wa miezi mitatu, na ikifika miezi sita, nitakupandishia mshahara wako na kufikia shilingi milioni moja na elfu sabini na tano,” mzee Ken alisema.
Dina hakuamini alichokuwa akiambiwa, alihisi kulikuwa na makosa kwenye matamshi ya mzee Ken. Akatamani amwambie mzee huyo arudie kauli yake, lakini hakuweza.

“Upo tayari kwa mshahara huo?” mzee Ken aliuliza huku akili yake
ikicheza na akili ya Dina na kugundua binti huyo alikuwa tayari amekimeza chambo.
“Nipo tayari,” Dina alisema kwa sauti hafifu ambayo ilibaki kidogo ikatae kutoka kutokana na kutoamini bahati iliyomwangukia ya kuajiriwa kwa kulipwa mshahara mkubwa.

“Subiri hapo nje,” mzee Ken alisema.
“Ukitoka niitie huyo mama.” Dina alisimama kwa nidhamu kabla hajaondoka, na hatua zake alivyoanza kutoka alikuwa akitembea kwa woga na miguu yake alihisi kama iliyokuwa ikitetemeka na kutembea kwa tahadhari kama vile alionywa sakafu ya humo ofisini ingevunjika kama angeikanyaga kwa nguvu. Alitoka na kuyapeleka maagizo aliyotumwa kumpelekea Katibu Muhtasi.

Baada ya Katibu Muhtasi kuingia ofisini kwa mzee Ken alikokuwa ameitwa, ikamchukua muda mfupi akatoka. Alipotoka alimchukua Dina hadi kwenye ofisi iliyokuwa jirani na ilipo ofisi ya Richard. Huko walimkuta kijana aliyeonekana kuwa na umri wa takribani miaka thelathini anayeitwa Mohamed Hussein, lakini alikuwa akiitwa kwa jina la mkato, Mohsein.

“Mohsein,” Katibu Muhtasi alimuita kijana huyo.
“Huyu binti ni mfanyakazi wetu mpya, anaitwa Dina. Utamfundisha kazi unazozifanya ili akusaidie na muwe pamoja,” baada ya kusema hivyo, akamgeukia Dina na kusema, “Dina, huyu anaitwa Mohamed Hussein, wengi tunamuita Mohsein. Utakuwa naye pamoja na atakufundisha kazi zote unazotakiwa kuzijua,” baada ya kusema hivyo akamgeukia tena Mohsein.
“Mohsein, utamwonyesha Dina bosi wenu ni nani.”

Baada ya kumtambulisha Dina, Katibu Muhtasi alitoka, akaenda ofisini kwa Richard ambako alimhabarisha Richard kuhusu ujio wa Dina.
Siku hiyo hiyo Dina akaanza kazi rasmi!

* * * * *

“Eti nini?” John Sailasi aling’aka akiwa na butwaa usoni mwake kuonyesha kutokiamini kile alichokisikia kutoka kwa Dina. Akazunguka chumbani mwake kama mnyama mkali aliyejeruhiwa. Akiwa amejikamata kiuno, John alimwangalia Dina huku uso wake ukionekana kama anayetatizwa na kitu. Akacheka kicheko kilichoonyesha kumwumiza. “Usiniambie barua uliipeleka leo, na kazi ukaianza leo hii!” alisema.
“Isitoshe, umeahidiwa kulipwa shilingi laki nane na nusu kama mshahara wako na baada ya miezi sita utaongezewa hadi kufikia milioni na ushee!

Huoni kama kuna sintofahamu katikati yake? Hujiulizi inakuwaje huna ujuzi wowote, lakini bado utalipwa shilingi laki nane na nusu kama mshahara wako wa kuanzia? Za nini zote hizo wakati hauna umaalumu wowote kwenye kazi hiyo? Halafu kitu cha ajabu ni kuwa umetakiwa uripoti kazi zako kwa Richard, huu ni mzaha, Dina!"

"Mzaha ki-vipi?" Dina aliuliza kwa utulivu.

"Wakati ulivyoambiwa uandike barua, ulijua ni kazi gani unayokwenda kuifanya?"

"Sikuijua!" Dina alisema na kuinua juu mabega yake kama mtu asiye na hatia. "Nilichotakiwa niandike ni barua ya kuomba kazi na niambatanishe na vyeti vyangu vya shule."

"Uliwahi kumwambia mama yako akutafutie kazi kwenye kampuni ya baba yake Richard?"

"Sikuwahi kuongea naye. Lakini hiyo sio sababu ya kutonitafutia kazi."

"Ninavyoshangaa hivi, sina maana sitaki ufanye kazi! Lakini huwa najiuliza, imekuwaje ukapata kazi ghafla na kirahisi hivyo? Hiyo barua uliyoiandika, ulikuwa umeomba nafasi kazi gani? Au walikuwa wakimuhitaji mtu kwa haraka sana kwenye nafasi hiyo waliyokupa?"

"Niliandika kazi yoyote, nadhani elimu yangu ya kidato cha sita labda ndio iliyonifanya wakubali kunipa mshahara huo."
John akacheka kicheko cha dhihaka na kusikitika.
"Mshahara huo waliokuahidi kukupa haupishani sana na wa mhitimu wa Chuo Kikuu aliyeondoka na shahada yake! Sembuse kidato chako cha sita ukiwa umekosa hata alama za kukupeleka chuoni? Tuachane na hilo, lakini pia bado huna ujuzi wowote wa kazi unayoijua zaidi ya kuhitimu na kupata cheti cha kidato cha sita, halafu ulipwe mshahara huo? Huo ni mzaha Dina, lazima hapa kuna namna!"

Uso wa Dina ukiwa kama uliogwaya, alimwangalia John na kusema kwa sauti ya utetezi, "Labda ni kwa vile mama yangu na mke wa mzee Ken ni marafiki."

"Nina muda gani tokea nianze na wewe Dina?" John aliuliza kwa aina ya kusuta. "Kipindi chote hicho hujawahi kuniambia kama mama yako na mama yake Richard..," hapa alisita, kisha akasema kwa mkazo, "Mimi simuiti mke wa mzee Ken…namuita mama yake Richard! Sioni sababu ya kuzunguka! Hujawahi hata siku moja kunitamkia kama wao ni marafiki! Nakumbuka uliwahi kuniambia kuna wakati mama yako aliwasaidia wao kupata hati ya kiwanja kutoka Wizara ya Ardhi, basi! Leo unaniambia wao ni marafiki? Dina! Au kwa sababu ya kupata hiyo kazi?"

"Kwa hiyo unafikiri hii kazi nimeipata kwa sababu ya Richard?" "Kuna sababu nyingine?"

Dina akacheka kicheko cha karaha, kifupi na kilichoudhi.
"Yaani John unamaanisha nini?" Dina alisema kwa sauti iliyokereka.
"Yaani mimi kukubali kufanya kazi kwenye kampuni ya mzee Ken maana yake kazi hiyo kanifanyia mipango Richard? Au kufanya kazi chini yake ndio nitakuwa demu wake?"

“Nakijua unachokiwaza wewe! Unahisi mimi nalia wivu, lakini wacha ionekane hivyo..!” John akasita, akacheka kicheko kidogo kilichoonyesha kumwumiza ndani kwa ndani.
“Sitaki kusema zaidi, lakini nakwambia kitu kimoja, mimi siridhiki wewe ufanye kazi pale!”

“Kwa hiyo ina maana huniamini? Umekwishaniona kuwa nakusaliti?” Dina alisema kwa sauti ya kulalamika na iliyoonyesha lawama ndani yake.

“Wewe umepelekwa pale kama chambo, nakwambia Dina!”
“Kwa hiyo mama yangu ameshiriki kwenye njama za kuniuza?”
“Sina maana hiyo!”

“Sasa una maana gani ukisema nimepelekwa pale kama chambo wakati ni mama yangu ndiye aliyenifanyia mipango hii ya kazi?”
“Tuyaache hayo Dina,” John alisema na kuonyesha kukata tamaa. “Fanya nikusindikize nyumbani!”
Dina alishusha pumzi kwa nguvu, kisha akaunamisha chini uso wake na kuubana mdomo wake. Akazama kwenye fikra.
Ilikuwa ni siku ya kwanza Dina akiwa ameanza kazi, lakini pia ikawa siku ya kwanza kazi hiyo kumwingiza kwenye mgogoro na John!

* * * * *

Ajira hiyo ya Dina ilimkosesha amani John Sailas. Taarifa alizopewa na Dina kuwa ameanza kazi kwenye kampuni ya mzee Ken na kazi hiyo akiwa anaifanya chini ya usimamizi wa Richard, hali kadhalika na kiwango cha mshahara alichoahidiwa kupewa, ulimkamilishia jawabu kuwa, kuna zengwe lililosukwa dhidi ya Dina!

John alikuwa akijua Richard na Dina waliwahi kuwa na mahusiano
kabla ya kufarakana, na pia alikuwa akizijua juhudi alizozifanya Richard kumwomba Dina waurudishe uhusiano huo na Dina alikataa. Taarifa hizo, John alikuwa ameambiwa na Dina mwenyewe kwenye mazungumzo yao ya kawaida huku Dina akiapa kuwa hajawahi kutembea na Richard, lakini alikiri uhusiano wao ulikuwa ni wa aina ya mapenzi. Tukio la kuambiwa taarifa hizo lilitokea siku za mwanzoni za urafiki wao baada ya John kujua pahali ilipo nyumba ya akina Dina ni jirani na anapoishi Richard. John akamwambia Dina kuwa, yeye na Richard waliwahi kusoma shule moja na darasa moja walipokuwa kidato cha kwanza kabla ya Richard kuhamia nchini Kenya kwa masomo, ndipo Dina naye alipomweleza John uhusiano uliokuwepo kati yake na Richard kabla hawajafarakana.

Kwa kipindi chote hicho, ingawa John baadhi ya wakati alikuwa akionana na Richard hususan baada ya Richard kurudi kutoka Uingereza, lakini John hakudiriki kumtamkia Richard kuwa ana mahusiano na Dina. Na sababu iliyomfanya John asimwambie Richard ni kutokana na kutokuwa watu wa karibu kiurafiki zaidi ya kule kujuana kuwa waliwahi kusoma shule moja, kidato kimoja, na kwa mwaka mmoja! Pamoja na kutomwambia kutokana na sababu hiyo, lakini sababu nyingine iliyomfanya asimgusie lolote linalohusu uhusiano wake na Dina, ni kwamba John hakutaka Richard aujue uhusiano huo kati yake na Dina kwa kuhofia endapo Richard angejua, angeweza kuianzisha vita ya kumgombea Dina na yeye John alihisi angeshindwa vita hiyo kutokana na kuwa Richard ni mtoto wa tajiri mwenye uwezo wa vishawishi vyote

ambavyo vingemfanya Dina arudi tena kwake!

Tokea wakati huo, John alipokuwa akimsikia Dina akilalamika kuwa Richard alikuwa bado akimsumbua kwa kumfuata fuata, alijikuta akiingiwa na homa ya wasiwasi huenda siku moja Richard angeweza kufanikiwa kumgeuza mawazo Dina na Dina angeurudisha tena uhusiano wake na Richard na yeye akitoswa!

Mawazo hayo yalikuwa yakimtesa na kumkosesha amani. Faraja pekee aliyokuwa akiipata ambayo hakuiwekea asilimia mia moja ni kule kupewa moyo na Dina kuwa aondoe wasiwasi, huku Dina akimhakikishia kuwa kamwe asingeweza kurudisha uhusiano wake na Richard hata ingetokea wakiachana yeye na John! Huo ulikuwa upande mmoja wa faraja.

Lakini upande wa pili wa faraja aliyokuwa akiipata John ni kule kusoma kwa Richard Uingereza. Akawa anajaribu kuitumia nafasi ya kutokuwepo kwa Richard nchini kuuimarisha uhusiano wake na Dina. Akahisi amefanikiwa kulitimiza hilo! Lakini wakati akifikiri hivyo, siku chache baadaye akapata habari kuwa Richard amerudi nchini, tena moja kwa moja!
Habari hizo zilimsumbua kwa sababu ya kumpenda sana Dina. Usumbufu huo ukamfanya ajikute akifanya mambo ya kibwege yaliyotawaliwa na wivu, akaanza kuzifuatilia nyendo za Dina kwa siri kuchunguza kama angeziona dalili za watu hao wawili kuurudisha uhusiano. Lakini kabla ya matokeo ya upelelezi wake hayajampa picha yoyote, ndipo alipojikuta akipata faraja baada ya kusikia Richard ameanzisha mahusiano na Judi!

Unjema wa habari hizo ulikuja pale Dina alipomhabarisha kuwa, msichana aliyeingia kwenye mahusiano na Richard ni msichana aliyesoma naye pamoja sekondari na walikuwa wakifahamiana vizuri ingawa hawakuwa na urafiki wa karibu sana, lakini walikuwa na aina ya urafiki. Tukio hilo likampa John imani kuwa, isingekuwa rahisi kwa Dina kumkubali tena Richard wakati akijua ana mahusiano na Judi ambaye alisoma naye shule moja kwa miaka minne huku wakiwa na urafiki fulani.

Hatimaye John akaja kuzisikia habari zilizokuwa zimeanza kuenea kuwa, Richard na Judi wanataka kuoana! Taarifa hizo zikamchanganya akili kutokana na furaha aliyoipata na iliyomhakikishia kuwa, ndoa hiyo kati ya Richard na Judi itasababisha kutokuwepo tena na uwezekano wa Richard na Dina kurudiana! Furaha yake hiyo ikamlazimisha na yeye ajibu mapigo kwa haraka kama jibu la kumfurahisha Dina; akaamua kupeleka posa kwa wazazi wake Dina! Aliamini hilo lilikuwa jibu kwa Dina asije akajisikia unyonge atakapomwona mwenzake anaolewa!

Lakini siku chache baada ya kujibiwa posa yake kuwa imekubaliwa, John akaambiwa na Dina kuwa, mahusiano kati ya Richard na Judi yamefikia tamati! Ni taarifa ambazo kidogo zilimshitua, lakini hazikumuweka roho juu hasa kutokana na kule kukubaliwa posa yake, akaamini ndoa atakayoifunga na Dina itamfanya ammiliki msichana huyo anayempenda kuliko kitu kingine chochote kile, kwa haki zote. Hata hivyo faraja hiyo haikudumu, kabla ya ndoa yake kufanyika mashaka mapya yakapandikizwa moyoni mwake, baada ya Dina kumfahamisha kuwa amepata ajira kwenye kampuni ya baba yake Richard!

Akiwa ametoka kumsindikiza Dina na kumfikisha nyumbani kwao huku kiza kikiwa kimeishaingia, alipokuwa anarudi nyumbani kwake akiwa ndani ya daladala na akiwa ameiacha pikipiki yake nyumbani kutokana na Dina kuapa kuwa hapandi pikipiki, John alikuwa amejawa na hofu ya wazi iliyomkosesha

amani kufuatia kitendo cha Dina kukubali kuajiriwa kwenye kampuni ya baba yake Richard! Zilikuwa ni habari zilizomjia kama shambulizi la ghafla ambalo hakujiandaa nalo, na laiti angekuwa anazifahamu kabla, angeweza kuweka pingamizi kwa kumshawishi Dina asikubali.

Aliamini Richard alikuwa amepania kutaka kumrudisha Dina kwenye himaya yake ya mapenzi baada ya harusi yake na Judi kuvunjika, na akawa na dhana kuwa Richard ameamua kufanya hivyo kama eneo la kumlipizia kisasi Judi. John akakiri kuwa, endapo Richard atafanikiwa kuurudisha uhusiano wake na Dina ni wazi kitendo hicho kitakuwa kinaitishia ndoa yake isifanyike! Hakuwa na uhakika ni mbinu za aina gani zilizotumiwa na Richard hadi kufanikisha Dina aajiriwe kwenye kampuni ya baba yake, lakini aliamini, ama Richard alimtumia mama yake kwenda kumwambia mama yake Dina kumwambia kuna nafasi ya kazi inayomfaa Dina, au Richard mwenyewe alimkabili mama yake Dina na kumwambia kuna kazi anayotaka kumwajiri Dina huku akijua mama yake Dina asingeweza kuilaani bahati hiyo kutokana na binti yake kutokuwa na ajira.

Mzunguko wa ajira hiyo ulivyopatikana bado uliendelea kumtia mashaka baada ya kukifikiria kiwango cha mshahara atakacholipwa Dina, ni kiwango kilichoonyesha mazingira aliyoyaamini yana ushawishi wa kumshawishi Dina aikubali ajira hiyo na kisha pia, aione familia hiyo ya mzee Ken kuwa ni wakarimu. Alizikumbuka tuhuma alizowahi kuzisikia kuwa, Richard hudekezwa sana na wazazi wake. Alijikuta akizipa nguvu tuhuma hizo kwa kuihusisha familia hiyo kujiingiza kikamilifu kwenye kuitengeneza njama ya kumsaidia Richard ili afanikiwe kumpata Dina! John alihisi Richard atakuwa amewaambia wazazi wake jinsi anavyomuhitaji Dina na huenda baba yake alimpa hakikisho la kumsaidia kuliondoa tatizo hilo kwa kukubali kumpa ajira Dina kwenye kampuni hiyo, vinginevyo, mzee huyo asingekuwa tayari kumwajiri Dina kwa kupoteza pesa nyingi kumlipa mshahara mkubwa wa aina hiyo!

John hakuona mantiki nyingine yoyote iliyotumika kumfanya Dina alipwe mshahara mkubwa kama huo wakati ni mbumbumbu asiyekuwa na ujuzi wowote wa kazi anayoijua. Aliamini hakuna mwajiri yeyote duniani anayeweza kumwaga pesa kwa ajili kulipa mshahara mkubwa bila ya kuwepo faida. Aliamini Dina hakuwa na faida yoyote kwa mzee huyo kibiashara na wala hakuwa na thamani ya kulipwa mshahara kama huo, isipokuwa amelifanya hilo kwa ajili ya kumsaidia mwanae!

Kumfanya Dina awe chini ya uongozi wa Richard kikazi, John aliamini ni sehemu ya mkakati utakaoimarisha kuurudisha uhusiano uliopotea kati ya Richard na Dina. Hali hiyo ikamfanya John ajiulize kama taarifa za kuolewa kwa Dina zilikuwa zikifahamika na familia ya mzee Ken? Na kama zitakuwa zinafahamika, inakuwaje wafanye maamuzi ya kuhatarisha kuivunja ndoa ya Dina? Na kama watakuwa hawana habari hizo je, urafiki wa mama Dina na mama Richard unaodaiwa na Dina, inakuwaje mama yake asimfahamishe mama Richard kuwa Dina anatarajiwa kuolewa hivi karibuni?

John akaanza kuingiwa na wasiwasi kuwa huenda Dina alimdanganya alipodai kuwa, hakuwa aliijua mipango hiyo ya kazi tokea mapema! Lakini hata kama ni kweli alikuwa haijui, John aliwaza, ina maana ajira ile ya kuwekwa karibu na Richard haikumshitua? Akaifikiria kauli ya Dina ya kujiamini aliposema, asingeweza kukubali kuwa demu wa Richard hata kama wangeshirikiana na Richard ofisi moja! John alishindwa kujipanga auegemee upande upi kati ya kuiamini kauli ya Dina au Dina alisema vile kumwondoa njiani?

Katika kufikiri huko, John alikiri kitu kimoja kuwa, yeye na Richard wapo kwenye mpambano wa

kumgombea Dina! Ingawa aliingiwa tena na ile hofu ya kuwa anapambana na mtu mwenye uwezo wa kipesa, lakini kulijua hilo hakukumkatisha tamaa, aliamini Dina angekuwa upande wake kwenye vita hivyo. John akaiona njia pekee ya kupambana na Richard ni kuhakikisha anaharakisha ulipaji wa mahari aliyotakiwa atoe na kisha afanye haraka ya kutangaza siku ya kufunga ndoa.

John akajikuta akiwa na ari mpya iliyompatia nguvu mpya ya kuhakikisha anafanikiwa kuikamilisha mahari hiyo ndani ya wiki mbili zijazo!

***DINA ameanza kazi rasmi, John SAILAS kwa roho upande anakubaliana na hali huku akiamini kuwa DINA amewekwa pale kama chambo.
LAITI kama John angekuwa na pesa huenda angemzuia DINA asifanye kazi lakini JOHN ni maskini.
***JE? Richard atafanikiwa kumrejesha DINA katika himaya yake????

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA NANE

“Nimekupa uisome ili ujue haitawezekana kufunga ndoa, hadi miezi mitatu ipite! Hukuyaona masharti niliyoandikiwa? Si umeona siruhusiwi kuchukua ruhusa zaidi ya siku moja? Ndoa inahitaji uwe huru, ikibidi uwe na ruhusa ya zaidi ya wiki moja, wengine huchukua hadi likizo. Kwa hiyo tarehe uliyoitaja haitowezekana. Itabidi tusubiri hadi baada ya miezi mitatu ndio tufunge ndoa!”

Kauli hiyo ikamnyong’onyesha John, ikamchanganya kwa muda huku akiuona mpango wake ukielekea kushindwa.

Hakukubali!

“Tunaweza tukaoana bila sherehe!” John alisema kama aliyekurupuka huku akionekana kukosa umakini.

“Usinichekeshe John! Tuoane bila ya sherehe kisa nini?” Dina aliuliza katika hali inayomshushua John.

John akaanza kuueleza uwongo wake, Dina akausikiliza mwanzo hadi mwisho.

“Muda wa wewe kwenda kusoma na muda niliopewa kazini hautatofautiana sana,” Dina alisema kwa utulivu baada ya kumsikiliza John.
“Mimi nitakuwa tayari kukusubiri hadi urudi! Kwani kuna haraka gani mpaka tufunge ndoa kwenye mazingira kama hayo yasiyo na sherehe? Nitasubiri hadi utakaporudi ili tuweze kufanya kitu cha uhakika. Hata hivyo, unadhani upande wetu utalikubali wazo lako? Eti tuoane kwanza halafu sherehe baadaye? Najua nao watakujibu kama hivi ninavyojibu. Mimi nakuomba usisumbuke kuwapa ushauri huo upande wa kwetu. Nakushauri kitu kimoja,” Dina akanyamaza na kumwangalia John aliyekuwa amesimama kama aliyeumbuliwa huku akionekana kukosa hoja.
“Fanya hiyo mahari iletwe kama ulivyopanga. Itakuwa vizuri ukiilipa kabla hujaondoka nchini ili uonekane kweli una dhamira ya kunioa!”

Pigano la kwanza dhidi ya Richard, John akakiri amekwishalipoteza!

***

RICHARD akiwa amekiegesha kidevu juu ya vidole alivyovifumbata pamoja huku mikono yake ikiwa imeegemea juu ya meza ya ofisini kwake, alikuwa ametulia katika hali hiyo kwa muda mrefu na kuonekana kutekwa mawazo na kitu alichokuwa akikifikiri. Ilikuwa kama fumbo mfumbie mjinga! Alikuwa akikifikiria kitendo cha kuajiriwa Dina hapo ofisini kilivyokuwa kimemshitua, kilimshitua kutokana na kitendo hicho kufanyika siku chache baada ya kutoka kuzungumza na baba yake kuhusu msichana huyo huyo ambaye alikiri anampenda na yupo tayari kumuoa.

Kuajiriwa kwa Dina katika mazingira aliyoyachukulia kuwa ni ya kumshitukizia ambayo yalifanyika kimya kimya kisha akakabidhiwa awe chini ya uongozi wake, Richard aliwaza jinsi baba yake alivyokuwa

hakufanya tena rejea ya mazungumzo yaliyomhusu msichana huyo tokea pale mara ya mwisho walivyolizungumzia suala lake na matokeo yake ni kumleta hapo akiwa amekwisha ajiriwa.

Richard alidhani kuajiriwa kwa Dina hapo ofisini kungekuwa ni sababu tosha ya kumfanya baba yake alirejeshe tena suala la msichana huyo kwenye mjadala wao uliokuwa haujamalizika kuhusu kumuoa, lakini alishangaa kumwona baba yake hakufanya hivyo! Ukimya huo wa baba yake ulimshangaza, lakini pia, alishangaa na kujiuliza kwa nini baba yake hakutaka kumshauri au kumdokeza kama alikuwa na mipango ya kumwajiri Dina?

Awali katika siku za mwanzoni, ajira hiyo ya Dina ilimsumbua kichwa kutokana na kumchukulia Dina kuwa ni adui yake baada ya kumkataa na kisha kukubali kuposwa na John. Tukio hilo la Dina kuajiriwa na kisha kuletwa kwenye idara yake kufanya kazi; tena bila ya barua ya ujulisho, lilimfanya apigwe na butwaa na kutomwelewa baba yake kwa uamuzi huo. Akawa anajiuliza mara kwa mara, ni nini kilichomfanya baba yake amwajiri msichana huyo wakati alikwishamfahamisha kuwa, alikataa kuolewa naye?

Lakini wingu la uteguzi wa kitendawili hicho kilichokuwa kimemuweka kwa siku kadhaa kwenye sintofahamu iliyokuwepo kati yake na baba yake kuhusu ajira hiyo ya Dina, Richard alianza kukitegua kitendawili hicho baada ya baba yake kumwandikia barua ya kiofisi zikiwa zimepita takribani siku tano tokea Dina kuajiriwa. Aliikumbuka barua hiyo iliyomjulisha kuwa, Dina atakuwa chini ya uongozi wake na ikamjulisha kiwango cha mshahara ambacho angelipwa.

Kiwango cha mshahara ndicho kilichokuwa chachu ya kumzindua akili! Mara ya kwanza alipokuwa akikisoma kiwango hicho alijikuta akiamini kuna makosa ya kisarufi yaliyofanyika kwenye barua hiyo, lakini baada ya kuona kiwango hicho kilikuwa kimeenda sambamba kwa kurudiwa kimaandishi, akawa amepigwa na butwaa baada ya kuona hakukuwa na maantiki yoyote iliyostahilisha Dina alipwe mshahara mkubwa kama huo wakati hana ujuzi wowote wa kazi!

Richard alikumbuka jinsi alivyoingiwa na ushawishi wa kwenda kumkabili baba yake mara baada ya kuletewa barua hiyo ili amwulize ni kwa nini alimwajiri Dina bila ya kushauriana na yeye hali akijua kuwa yeye na Dina hawaelewani? Isitoshe, pia alikusudia kumwuliza ni kwa nini ameamua kumlipa mshahara mkubwa kama huo wakati wapo wafanyakazi walioajiriwa wakiwa na ujuzi wao ambao hawapati mshahara kama huo? Akakumbuka kabla ya kuuchukua uamuzi huo wa kumkabili baba yake, alijiwa na wazo lililomfanya asite kuuchukua uamuzi huo baada ya kujiuliza kuwa, huenda kuna sababu iliyomlazimisha baba yake kumwajiri Dina na kuamua kumlipa mshahara wa aina hiyo. Wazo hilo ndilo lililompa nafasi ya kuufikiria uamuzi huo wa baba yake na kabla hajaenda mbali kifikra ndipo alipoweza kukitegua kitendawili hicho alichotegwa na baba yake!

Chachu ya kukitegua kitendawili hicho ilimjia Richard baada ya kuuwazia mshahara ambao angepewa Dina na kuyawekea mashaka maamuzi hayo. Akahisi lazima kungekuwa na sababu nyuma ya maamuzi hayo yaliyolazimisha Dina aanze kazi na mshahara kama huo. Ndipo alipogundua kuwa kiwango hicho cha mshahara kilikuwa ni aina ya chambo kilichovikwa kwenye ndoana alichotegeshewa Dina ili kumlainisha na aione familia ya mzee Ken ipo karibu naye. Ulikuwa mtego! Richard aliwaza. Mtego ambao ulikusudiwa kwa Dina ili aulegeze msimamo wake wa kukataa kuolewa na familia hiyo! Richard alitabasamu peke yake baada ya kugundua kuwa, Dina amechezwa shere kwa kutengenezewa wigo asioweza kuutoka; wigo utakaomfanya amkubali ili asiupoteze mshahara huo!

Richard akakiri kwa mtaji huo, isingekuwa ajabu kumwona Dina akiurudisha uhusiano uliokuwa umetoweka kati yao!

Ghafla akamkumbuka John! Akakumbuka kuwa, Dina yupo karibu kuolewa na John! Badala ya wazo hilo kumwingiza kwenye unyonge kama ilivyokuwa awali kila alipokuwa akikumbuka jambo hilo, safari hii Richard alijikuta akiliwazia jambo hilo kwa mtazamo tofauti. Kilichomfanya awe na mtazamo huo tofauti ni kule kuajiriwa kwa Dina hapo ofisini. Aliamini kuletwa kwa Dina na kuwekwa karibu yake kungemwezesha kuua Tembo kwa ubua. Richard alitengeneza tabasamu la ushari baada ya kujiona safari hii ana nafasi kubwa ya kumpata Dina hata kama ataolewa na John! Aliamini bado angekuwa na nafasi ya kumchukua na kutembea naye kwa siri akiwa ameolewa!

Wazo hilo la kuja kutembea na Dina akiwa ameolewa na John lilimfariji mno na kujisikia burudiko kwenye moyo wake. Aliuona huo ndio ungekuwa wakati mwafaka wa kulipiza kisasi kwa John! Na kwake ingekuwa ni furaha ilioje kama angefanikiwa kukifanya kitendo hicho katika mazingira hayo Dina akiwa ameolewa! Kitendo hicho kingemfurahisha zaidi moyo wake kwani angejiona angekuwa analipiza kisasi katika njia inayostahili, na ingekuwa ni nafasi yake ya kumdhihirishia John kuwa alifanya makosa kumpora Dina akiwa mikononi mwake! Alitaka liwe fundisho kwa John ili mara nyingine asivamie maeneo yanayomilikiwa na watu wenye pesa kama yeye!

Kisasi chake alitaka kisiishie kwa kumchukulia John mke wake halafu iwe basi; lakini pia, alitaka John aje atambue kuwa yeye anatembea na mke wake! Na sio tu John ajue kuwa mkewe anatembea na yeye, lakini pia, aliapa kuitumia nafasi hiyo kuhakikisha anamdhibiti Dina kimapenzi hadi awe chizi kwa ajili yake na John alifahamu hilo! Alipenda amwone John akitesekea penzi kama alivyoteseka yeye wakati alipokuwa akimbembeleza Dina warudiane. Alitaka kusiwepo maelewano kati ya John na Dina kwenye ndoa yao. Alipania kuisambaratisha ndoa hiyo, alitaka amshuhudie John akihangaika kwenda kuomba msaada kwa Padri ili kuiokoa ndoa yake bila ya mafanikio! Alitaka Kanisa lifikie mahali likubali kuvunjwa kwa ndoa hiyo, kisha yeye ndiye aje kumuoa Dina!

Lakini wakati akiifikiria mikakati hiyo ya kumsulubisha John na kumrudisha Dina kwenye himaya yake ya mapenzi, Richard alikiri bado kulikuwa na tatizo mbele yake ambalo alikiri kuwa ni kubwa na linalohitaji aina nyingine ya maamuzi! Tatizo hilo aliliangalia kama vile Mwanasayansi anavyokiangalia kirusi cha hatari kinachotaka kujipenyeza kwenye mfumo mzima wa mawasiliano ya chombo muhimu.
Alikuwa Mohsein!

Alimwona Mohsein kama mtu aliyekuwa akihatarisha harakati zake ziingie kwenye ugumu usio wa lazima. Na tatizo halikuwa kwa Mohsein mwenyewe, bali lilikuwa ni Dina! Aligundua Dina alikuwa akimpenda Mohsein. Kulikuwa na dalili za wazi zilizokuwa zikionyeshwa na Dina kuwa amekwisha kimahaba kwa Mohsein na akalikumbuka tukio la kuwafumania wakiwa wamevigusisha pamoja vichwa vyao kwa aina fulani ya mahaba wakati alipokuwa amewaingilia ghafla ofisini.

Tukio hilo lilikuwa likimtafuna Richard, wivu na chuki ya kumchukia Mohsein ikawa imejijenga, na hakutaka kujidanganya; kwa sababu dalili zote zilikuwa ziko wazi zikionyesha kuwa, kama kuna mtu anayeweza kumpata Dina kirahisi bila ya kujali kikwazo cha uchumba uliopo kwa John basi Mohsein ndiye mwenye nafasi hiyo! Richard akajionya endapo hatochukua hatua za haraka, uwezekano wa Mohsein kumchukua

Dina mbele ya macho yake usingezuilika!

Richard alikiri hilo ni tatizo na akaliona ni kubwa na la hatari! Asingekubali litokee huku akiliona! Afanye nini? alijiuliza. Amfanyie fitna Mohsein afukuzwe kazi? Aliiona hiyo ndio njia pekee itakayomuweka kwenye amani, lakini pia, aliogopa kitendo hicho kingeweza kigandulika na Mohsein kuwa, amefukuzwa kazi kwa ajili ya kuonewa wivu dhidi ya Dina! Hilo lingeweza kumchochea Mohsein kufanya juhudi za ziada kuhakikisha anatembea na Dina kama sehemu ya kulipiza kisasi! Richard alipolifikiria hilo, mchomo wa wivu ukapenya moyoni mwake! Akajionya kuwa, maamuzi yoyote ya kumfukuza kazi Mohsein yangeleta janga badala ya suluhisho.

Akajaribu kujituliza na kufikiri kwa kutumia uwezo wa akili badala ya akili za nguvu. Akajiuliza, ni njia ipi ya kuitumia ili Mohsein aachane na fikra za kumtaka Dina kimapenzi? Njia pekee aliyoiona kuwa inaweza ikamsaidia, ni kufanya kila njia ili Mohsein ajue kuwa, yeye ndiye aliyemwajiri Dina na Dina yuko hapo kwa ajili yake. Alikuwa na uhakika endapo Mohsein atalifahamu hilo, basi angeogopa kujihusisha kimapenzi na Dina kwani angeelewa, Dina ni mali za bosi wake!

Kwa kuwa alikuwa na safari ya kikazi ya kwenda Morogoro, Richard akapanga mara atakaporudi kutoka Morogoro ndipo angeyaonyesha makucha yake kuwa yeye ndiye bosi na mmoja wa wamiliki wa kampuni hiyo. Akaamini, mwelekeo wa uelewa huo ungemtisha Mohsein!

Laiti angelijua kosa analolifanya, kamwe Richard asingeenda safari hiyo ya Morogoro!

* * * * *

Ilikuwa siku ya pili tokea Richard alivyokuwa amekwenda Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa ndani wa mahesabu kwenye kituo chao cha mafuta ambacho ni kikubwa kuliko vingine vyote mkoani humo. Mohsein akawa amekaimu nafasi yake kiofisi.

Ilikuwa ni kawaida kwa kila inapokuwa Richard hayupo ofisini kikazi, Mohsein ndiye anayekaimu madaraka yake, labda itokee wote wasafiri safari moja ya kikazi. Siku ambayo Richard aliondoka kwenda Morogoro aliacha maagizo kwa Mohsein kuwa, kukahesabiwe vifaa alivyokuwa ameviorodhesha kwenye nyaraka aliyomkabidhi Mohsein ili vikahesabiwe upya baada ya kutokea utata wa orodha kamili ya mahesabu kuhusu vifaa hivyo vilivyokuwa vimehifadhiwa stoo na alitaka shughuli hiyo ifanyike siku hiyo hiyo aliyokuwa akisafiri ili akirudi akute majibu.

Lakini baada ya Richard kuondoka, Mohsein akazembea kuianza kazi siku hiyo kama alivyokuwa ameagizwa, akasubiri hadi siku ya pili asubuhi ndipo alipoikabidhi kazi hiyo kwa kumpa Dina akaifanye badala ya kuifanya yeye.

Ilikuwa ni kazi ya siku moja, lakini Dina akaingia nayo siku ya pili akiwa bado hajaimaliza!

Ikiwa ndani ya siku ya pili kazi hiyo haijamalizwa, na ikiwa ni siku ya tatu tokea Richard alivyoondoka kwenda Morogoro, ilipofika saa tano asubuhi, Mohsein akaanza kuingiwa na mashaka kuwa, huenda

Richard angerudi siku hiyo na kuikuta kazi ikiwa haijamalizika. Kwa kumhofia Richard asije akaja kumbwatukia atakapoikuta kazi hiyo haijamalizika na wakati jukumu hilo alipewa yeye, Mohsein aliamua kumfuatilia Dina ili ajue amefikia wapi na endapo ikibidi amsaidie.

Alimfuata Dina aliyekuwa peke yake kwenye hiyo stoo ambayo haikuwa kubwa ya kutosha na iliyozungukwa na makabati ya chuma yaliyokuwa wazi ambayo yalibeba vifaa mbalimbali vya kampuni, akamkuta yupo katikati ya kuhesabu.

“Bado hujamaliza?” Mohsein alimwuliza Dina.

“Ungenikuta nimekwishamaliza,” Dina alijitetea.
“Lakini kulikuwa na baadhi ya maboksi ilibidi niyapangue kwanza kisha ndio nikaendelea kuhesabu.”
“Kwani bado sana?”

“Kama utanisaidia, tutamaliza mapema.”
“Umebakiza upande upi?”

Dina akamwonyesha Mohsein upande wa makabati yaliyokuwa na vifaa hivyo. Mohsein akaenda kuhesabu. Iliwachukua dakika arobaini na tano hadi kuimaliza kazi hiyo.

“Chukua hesabu nilizozipata ili uingize kwenye mahesabu yako,” Mohsein alisema huku akimpa Dina karatasi aliyokuwa akiingizia nukuu za hesabu zake alizozipata.

Dina aliichukua karatasi hiyo na kusogea kwenye mwanga zaidi ambako alikwenda kuegemea kwenye kabati lililokuwa na uwazi na kuutumia uwazi huo kama meza ya kurekebishia hesabu zake huku akiwa amesimama. Mohsein akajiunga naye. Wakasaidiana kuzifanya pamoja hesabu hizo.

Wakati walipokuwa wakiendelea kuzifanya hesabu hizo, mabega yao yalikuwa yakigusana mara kwa mara na hali hiyo kuonekana ni ya kawaida kwao hadi walipomaliza na kupata uhakika wa hesabu walizozirekebisha.

“Nakushukuru kwa msaada wako,” Dina alisema, akiwa amegeuka kumwangalia Mohsein.

Mohsein akamwangalia Dina. “Usijali,” alisema.

“Lazima nijali bwana…” Dina alisema na kutabasamu huku akiendelea kumwangalia Mohsein.
“Ningekuwa sijaimaliza hii kazi kama sio wewe kuja na kunisaidia!”

Mohsein naye akatengeneza tabasamu na kusema, “Poa.”

Ghafla kukajenga ukimya kati yao ulioleta faragha humo ndani huku kila mmoja akishindwa kujisogeza alipokuwa amesimama. Wakatekwa na ukimya, kisaikolojia wakajiona wapo kwenye faragha iliyojitokeza huku kila mmoja akikiri nafsini mwake kuwa ilikuwa na jambo mbele yao linalohitaji kufanywa kati yao. Wakaangaliana, wakawa mabubu kwenye vinywa vyao, lakini macho yao yakawa yanazungumza lugha ya ukimya ambayo kila mmoja aliielewa maana yake. Mapigo ya mioyo yao ikaanza kwenda kasi. Mohsein

akawa wa kwanza kuonyesha kusudio lake kwa kuuangalia mdomo wa Dina, akauinamisha uso wake na kuusogeza usoni kwa Dina na mdomo wake kuulengasha mdomoni mwa Dina!

Mohsein akasita kuupeleka moja kwa moja mdomo wake kinywani kwa Dina, akasikilizia marejesho ya Dina yatakuwaje. Dina akawa ameganda kama aliyepigwa na shoti ya umeme, naye akajikuta akiuangalia mdomo wa Mohsein kwa macho yaliyoonyesha haiba ya kukubali kitendo kinachofuatia, kisha akafumba macho. Mohsein akaupeleka mdomo wake kinywani kwa Dina na papi zao za midomo kugusana. Mohsein akaupitisha ulimi wake..!

Dina akaupokea!

Kila mmoja alilihisi joto la ulimi wa mwenzake wakati ndimi zao zikinyonyana. Dina akauhisi mkono wa Mohsein ukianza kumpapasa kwenye paja lake ukiwa umeipandisha juu nguo yake, akawahi kuuzuia alipouhisi ukitaka kuingia ndani zaidi. Akaendelea kukaza msuli wake wa mkono kuuzuia mkono wa Mohsein uliokuwa ukitaka uende zaidi ya hapo.

Vita ya kuzuiana mikono iliendelea huku ndimi zao zikiendelea kunyonyana!

*****

HAIKUWA wiki njema kwa John tokea alivyojibiwa na Dina kuwa hakukuwa na uwezekano wa wao kuoana mapema kama alivyokuwa amekusudia. Sababu iliyokuwa imetolewa na Dina, John aliiafiki kuwa ni ya msingi, lakini alilaani kipengele kilichotumika kwenye barua ile kilichomnyima Dina kupata ruhusa ya kupumzika kikazi hadi miezi mitatu ikatike! Kipengele hicho alikiona kama vile kilikusudiwa kuingia kwenye dhamira yake ya kumuoa Dina isifanikiwe.

Hofu dhidi ya Richard iliendelea kujikita kila alipoifikiria miezi hiyo mitatu ipite bure bila ya kufunga ndoa na Dina, lakini wakati huo huo miezi hiyo ikitumika akimwona Dina akiwa karibu na Richard! Kihoro hicho ndicho kilichokuwa kikimtesa kwa wivu! Hakuamini kama Dina angekuwa na ubavu wa kuendelea kuhimili vishawishi vitakavyofanywa na Richard kwa wakati wote huo, hali hiyo ilimfanya awe na wingi wa hisia kuwa, Dina atamsaliti!

Hofu ilikuwa ikimtawala na kumuweka kwenye hali ngumu kila alivyokumbuka kuwashuhudia wanawake wengi wakiwaacha wanaume waliokuwa wakiwapenda na kuwafuata wanaume wenye pesa! John alizidi kuumia moyoni jinsi wanawake hao walivyokuwa hawajali maumivu yaliyowakuta wanaume waliokuwa nao baada ya kuwaacha, na wakati mwingine walidiriki hata kuwatolea maneno ya kebehi wakati wanaume hao walipokuwa wakiwabembeleza warudiane.

Fedha! John alinyong’onyea baada ya kuikiri nguvu ya chombo hicho. Awali kabla ya Dina kuajiriwa na kampuni ya mzee Ken, John aliwahi kujisifia kuwa ni mwenye bahati ya kumpata msichana aliyeumbika kama Dina aliyekuwa tayari kumkataa mwanamume mwenye pesa kwa ajili yake na kukichukulia kitendo cha Dina kumkataa Richard kama kigezo chake cha kupendwa. Alikuwa akijiona ni shujaa na kuhisi burudiko moyoni mwake kila alipokuwa akionana na Richard na kumcheka moyoni. Na wakati Richard alipokuwa akijaribu kumbembeleza Dina ili warudiane, John alifikia hali ya kumshangaa na kumwona kama aliyepungukiwa na akili!

Hakutaka kuamini Dina angeweza kumsaliti kupitia kwa mtu aliyekwisha kumkataa tokea awali. Lakini kwa upande wa pili hisia zilikuwa zikiendelea kumuonya mara kwa mara kuwa, ukaribu wa kikazi kati ya Dina na Richard ungewalazimisha watu hao wawili wajenge maelewano kati yao ambayo Richard angeyatumia kurejesha tena uhusiano wa mapenzi uliotoweka! John aliuhisi moyo wake ukienda mbio na dalili za kupandwa na shinikizo la damu zilikuwa zikimwashiria kutokana na wivu ulioitawala akili yake. Akakiri moyoni kuwa, kitendo cha kurudiana kwa Dina na Richard kama kitafanyika kingemwumiza mno!

Akaingiwa na akili ya kutaka kumshawishi Dina aache kazi, lakini alijikuta akijijibu mwenyewe kuwa hilo lisingewezekana! Aliamini hilo lisingewezekana kutokana na ukweli alioukiri mwenyewe kuwa, nyota yake ya mapenzi ilikuwa imefunikwa na nyota ya Dina! Dina alikuwa na sauti dhidi yake, alilolitaka ndilo litakalofanyika na aliamini Dina angelikataa wazo lake hilo na asingekuwa na ubavu wa kumlazimisha!

Ndani ya nafsi yake alikuwa akiandamwa na hatia iliyokuwa ikimsuta kutokana na ukweli kuwa alikuwa akimpenda mno Dina. Hatia hiyo ikawa inamuingiza kwenye hofu ya kuachwa na hata kudiriki kutawaliwa na mawazo ya kijinga kuwa kusingekuwa na mbadala wa maisha mengine bila ya Dina! Akauhisi ule unyonge wa kutokuwa na ushawishi wa kumuweka Dina chini ya himaya ya amri yake ukimzomea.

Mawazo yake yakarudi kule kule kwenye kuwahi kumuoa Dina mapema kabla ya Richard hajafanikiwa kurudisha uhusiano na Dina, aliamini hatua hiyo angalau ingemuweka kwenye haki ya kummiliki Dina kuwa mkewe, haki ambayo angeitumia kukabiliana na Richard kama angediriki au hata kujihusisha na Dina kimapenzi. Lakini ukweli huo ulikuwa mbali!

Alijua asingeweza kumshawishi Dina aache kazi kwa sababu Dina asingemsikiliza. Lakini pia asingeweza kumkabili Richard na kumuonya dhidi ya Dina kwa sababu Dina bado hajawa mkewe, na asingeweza kumvaa Richard kwa mkwara wowote kwa sababu mwenzake ana pesa inayoweza kutumika kwenye vyombo vya sheria na vyombo hivyo kumgeukia yeye na akajikuta akiswekwa mahabusu au pengine hata gerezani!

Akili yake ikajiwa na wazo la kimbilio la wanyonge; kwenda kwa waganga kwa ajili ya ushirikina! Angalau kwa kiasi fulani wazo hilo lilianza kumfariji baada ya kuifikiria hatua hiyo. Hakuwa ni mtu aliyependa kujihusisha na vitendo vya ushirikina, lakini aliamini ushirikina upo. Alishawahi kuzisikia sifa za mara kwa mara walizokuwa wakisifiwa waganga waliopo kijijini kwao, sifa ambazo zilikuwa zikitolewa na watu wa mkoa wao. Hatua ya kuwafuata waganga kama hao aliamini kama ataichukua ingemsaidia kupambana na Richard. Fikra za kujipa matumaini kuwa dawa ya mtu mwenye pesa ni kupambana naye kwa kutumia njia za kishirikina ikaanza kumtawala kichwani.

Kwa upande huo aliamini angemwendea fundi wa shughuli hizo na kumtaka afanye uchawi wake ili Dina anapomwona Richard aingiwe na hisia kama vile ameona kinyesi! Pili, angemtaka fundi huyo afanye utaalamu wake wa kuifanya nyota yake iitawale nyota ya Dina ili aweze kumdhibiti kimapenzi. Aliamini kitendo hicho kingemfanya awe na sauti mbele ya Dina na Dina angegeuzwa kuwa kama Kondoo kwa kutii kila ambalo angelizungumza. Fikra hizo zikamrudisha John kwenye Ukamanda wa kujiona yupo tayari kurudi tena kwenye uwanja wa vita kupambana na Richard! Kwa mtazamo huo, John akaisifia akili yake kupata wazo la kishirikina!

Akaipanga siku maalumu ya kwenda kumwona mganga kijijini kwao!

* * * * *

***JOHN SAILAS anasukumwa na wivu na kuamua kuwakimbilia waganga wa jadi.
**DINA amejikuta katika mapenzi na MOHSEIN…..
****RICHARD bado hajafanikiwa kumrejesha DINA katika himaya yake.
***Ni vita ya kimyakimya kati ya MOHSEIN, RICHARD NA JOHN SAILAS

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA TISA

Kwa upande huo aliamini angemwendea fundi wa shughuli hizo na kumtaka afanye uchawi wake ili Dina anapomwona Richard aingiwe na hisia kama vile ameona kinyesi! Pili, angemtaka fundi huyo afanye utaalamu wake wa kuifanya nyota yake iitawale nyota ya Dina ili aweze kumdhibiti kimapenzi. Aliamini kitendo hicho kingemfanya awe na sauti mbele ya Dina na Dina angegeuzwa kuwa kama Kondoo kwa kutii

kila ambalo angelizungumza. Fikra hizo zikamrudisha John kwenye Ukamanda wa kujiona yupo tayari kurudi tena kwenye uwanja wa vita kupambana na Richard! Kwa mtazamo huo, John akaisifia akili yake kupata wazo la kishirikina!

Akaipanga siku maalumu ya kwenda kumwona mganga kijijini kwao!

* * * * *

Usiku, Dina alichelewa kupata usingizi kutokana na fikra zilizokuwa zimemtawala karibu kutwa nzima ya siku hiyo; fikra za kumfikiria Mohsein na tukio lilitokea siku hiyo kati yao kwenye stoo ya kazini kwao! Ni tukio lililomlazimisha awafikirie watu wawili kwa wakati mmoja, Mohsein na John! Alikiri tukio la kufanya mapenzi na Mohsein siku hiyo lilikuwa limedhihirisha jinsi lilivyoishinda ile dhamira yake aliyojipa awali ya kuchukua hadhari na maamuzi yake pindi anapokuwa na Mohsein. Alikuwa ameshindwa kuitekeleza! Alikiri kushindwa huko kulitokana na ukweli kuwa, akiwa mbele ya Mohsein alikuwa akijisikia raha wakati wote kama vile alirogwa naye!

Kumruhusu Mohsein afanya naye mapenzi kulimdhirishia ni namna gani moyo wake ulivyotekwa na jamaa huyo. Hakutaka kuamini kama ametokea kumpenda, kwa sababu aliamini ni John pekee ndiye aliyetokea kumpenda. Alikubali kuwepo kwa hisia fulani zilizokuwa zikimfanya afarijike kila anapokuwa yuko na Mohsein, lakini alipingana na nafsi yake kuwa amempenda Mohsein. Aliamini mapenzi yake yapo kwa John na kukiri John ndiye kila kitu kwake. Lakini hata hivyo, nafsi yake iliendelea kumsuta kwa kukataa kuungama kuwa, kitendo cha kufanya mapenzi na Mohsein kilishatia ufa kwenye msimamo wake huo wa kuwa, John ni kila kitu kwake!

Ufa huo ulioutikisa msimamo wake ulimfanya akiri kwa mara ya kwanza kuwa, binadamu ana udhaifu ndani ya nafsi yake. Ni udhaifu wenye msukumo mkubwa wa ushawishi pale unapojikuta umezungukwa kwa ukaribu na ushawishi huo. Alikiri njia pekee ya kuepusha kuingia kwenye majaribu ni kukaa mbali na ushawishi wa aina hiyo; vinginevyo ni kushawishika kama alivyojikuta akishawishika kwa Mohsein! Yeye na Mohsein walikuwa na ukaribu, ukaribu uliokuja baada ya nafsi yake kukiri mapema kuwa Mohsein ni mwenye haiba ya kupendeza, jamali wa sura na umbile! Kukiri huko kukawa kama aliyeiruhusu sumu imwingie kwenye mishipa yake ya damu! Huo ndio ukawa udhaifu wa kwanza uliomwingiza kwenye ushawishi ambao ulikuja kuchochewa na ukaribu wao wa kila siku. Sumu ikaanza kumtafuna!

Akamruhusu Mohsein afanye naye mapenzi katika mazingira ambayo mwenyewe alikiri kuwa, alikubali mwenyewe kwa hiari yake. Kukubali kuwa alikifanya kitendo hicho kwa hiari yake kuna kipindi akawa anakijutia kiaina, lakini pia majuto hayo yakawa hayamwumizi sana kichwa kwa sababu alichokifanya ulikuwa ni uamuzi wake mwenyewe! Kuyumba huko kimawazo kukamdhihirishia jinsi alivyomkubali Mohsein kwenye nafsi yake na hakutaka kujidanganya kwa hilo, kwa kuwa alishakiri alikuwa akiufurahia ukaribu uliopo kati yake na Mohsein!

Kukiri huko kulimfanya kila alipokuwa akimfikiria Mohsein na kile kitendo kilichofanyika stoo kulimletea msisimko fulani, lakini pamoja na kuwaza hivyo, fikra za kumfikiria John nazo zikawa zinajipenyeza muda huo huo. Alimfikiria John kwa sababu aliamini ndiye anayempenda na aliamini pia, hata ndoa yao nayo ingefanyika kama walivyopanga. Lakini pia akakiri moyoni kuwa, bado angeendelea kumruhusu Mohsein

kuwa mtu wake wa karibu kuiba kufanya naye ngono!

Katika hali ya kujipanga kisaikolojia, Dina alikiri upo uwezekano wa kuiratibu mihimili yenye uzito tofauti ya kupenda watu wawili kwa wakati mmoja. Alijua mambo hayo huwa yanafanyika na huendelea kufanyika kila kukicha kwa wanandoa kufanya mapenzi nje ya ndoa. Dina aliamini matendo hayo huwa yanajulikana ndani ya jamii na wakati mwingine huchukuliwa kama ni matukio ya kawaida, lakini hugeuka kutokuwa ya kawaida, pale fumanizi linapotokea.

Ni matukio yanaohusisha kada tofauti, wake na waume. Wapo waheshimiwa wenye heshima zao, wapo wenye elimu zao, wapo wenye madaraka makubwa na wakati mwingine hata kwa viongozi wa kidini, wote hao hujihusisha na vitendo hivyo. Udhaifu wa mwanadamu! Dina aliwaza. Lakini kwa upande mwingine hisia za kupingana na mawazo hayo zilimjia. Akazitazama katika mtazamo wa Kishetani, lakini akakiri ni mtazamo uliokaa kifalsafa zaidi kuliko Kibaolojia. Akakubali kuwa, inapotokea binadamu akatawaliwa na udhaifu huo huwa ni vigumu kuuondoa kirahisi kama mahubiri ya dini yalivyo. Akakiri kuwa, hata yaliyomtokea kati yake na Mohsein yalitokana na udhaifu wa kibinadamu na sio Ushetani!

Jambo pekee ambalo aliliona lingemuweka kwenye utulivu na amani katika kukabiliana na hali hiyo ni kujipanga kuitunza siri hiyo isijulikane na John! Siri ndio ingetumika kuliendesha zoezi hilo la kumtumikia John na Mohsein, kwa sababu kwa upande wa John ni kuwa alimpenda, na kwa upande wa Mohsein ni kwamba nafsi yake ilitaka awe naye. Hata hivyo, ili kuitunza siri hiyo alikiri mmoja alipaswa amjue mwingine na sio wote kutojuana! Alimwona Mohsein ndiye mwenye haki ya kutakiwa kumjua John, ili ajue ni mchumba wake na anahitaji kuheshimiwa.

Hisia za Shetani! alijiambia wakati akiyawaza hayo. Lakini akazipuuza kwa kujiweka kibaolojia zaidi kuwa yeye ni binadamu wakati mwingine huendeshwa na nafsi yake inavyomshawishi! Akauona huo ndio ukweli wenyewe na anapaswa akabiliane nao!

Richard! Tukio la kumkumbuka lilikuja kama onyo asilolitarajia, onyo lililomkumbusha kuwa kuna mtu muhimu aliyekuwa amesahauliwa. Dina aliiona hatari iliyopo mbele yake endapo Richard atagundua mahusiano ya mapenzi yaliyopo kati yake na Mohsein! Alijua ugunduzi huo ungemletea Richard wivu wa mapenzi ambao aliamini ungeweza kuleta kizaaza cha kumpotezea kazi mmoja wao, ama yeye au Mohsein! Au wote kwa pamoja! Dina alikuwa na uhakika Richard alikuwa bado hajaachana na nia yake ya kutaka kumuoa, na alijua lazima angekuja kumwomba ili warudiane. Dalili zilikuwa za wazi zilizokuwa zikimuashiria kuwa Richard alikuwa bado akimuhitaji, kuanzia uangaliaji wake hadi uzungumzaji. Kila kitu kilijidhihirisha kwa Dina kuwa, Richard alikuwa bado akiendelea kuteseka na penzi lake!

Tokea awali, baada ya kuajiriwa na kufahamu kumbe Richard naye anafanya kazi kampuni hiyo hiyo, Dina alijipanga mapema kuwa, endapo Richard atamwomba waurudishe uhusiano wao, asingemkubalia! Na alijiandaa kuitumia sababu ya kuchumbiwa na John kuwa ni kigezo cha kumkatalia. Alijua uamuzi huo ungeendeleza uadui kati yao, lakini aliamini Richard asingeweza kumfukuza kazi kwa sababu sio yeye aliyemwajiri, bali ni baba yake!

Lakini ni hili tatizo jipya lililojitokeza ndilo lililokuwa likiichachafya akili yake. Mahusiano yake na Mohsein! Hakutaka kujidanganya na tatizo hilo. Alijua ni tatizo kubwa na lingeleta balaa endapo Richard atagundua kuwa yeye na Mohsein wana uhusiano wa mapenzi. Alikuwa na uhakika tatizo hilo litawasha moto wa

kutisha hapo ofisini kati ya watu hao wawili; Richard na Mohsein! Pengine hata kufikia kupigana au kufanyiana visa vya kuudhi. Hofu ikaanza kumuumiza Dina na kichwa kikamuuma, mashaka yakamwingia kuwa anaweza akasababisha mtafaruku utakaoivuruga ofisi nzima na kusambaa hadi kwa mzee Ken na mzee Ken angemwambia mama Richard na mama Richard angemwambia mama Dina, na mama Dina angemwambia baba Dina na baadaye taarifa hizo zingemfikia John!

Wote hao wangemwona yeye ndiye chanzo cha matatizo na mzigo wote wa lawama ungemwangukia. Uamuzi wa kufukuzwa kazi alikuwa na uhakika ungefanyika, na aliamini kusingetokea mtu yeyote kati ya hao ambaye angemwonea huruma, isitoshe hata wazazi wake wasingesita kumlaani kwa kupoteza kazi iliyokuwa ikimpatia kipato kizuri ambacho kingekuwa msaada mkubwa kwa wazazi wake hao.

Akiwa amechanganyikiwa na kuzinduka kwake huko, Dina alikurupuka kitandani na kuichukua simu iliyokuwa pembeni yake, akampigia Mohsein.

“Sema Dina,” sauti ya Mohsein ilisikika baada ya kuipokea simu. Ilikuwa nzito yenye kujiamini na iliyotulia, ikionekana kama aliyekuwa ametoka usingizini.

“Ulikuwa umelala?” Dina aliuliza kwa tahadhari, hakutaka kuingia moja kwa moja kwenye hoja.

“Siwezi nikasema hivyo, lakini nilikuwa nimepitiwa na usingizi nikiwa kwenye kochi.”

“Ulikuwa ukifanya nini hapo kwenye kochi?”

“Nilikuwa naangalia runinga nikapitiwa na usingizi. Vipi?” “Mohsein, kuna jambo muhimu nataka nikwambie,” Dina alisema kwa sauti iliyokuwa na umakini.

“Niambie mpenzi,” Mohsein alisema kwa kujiamini na kiburi cha ujivuni kikawepo ndani yake huku sauti yake ikiendelea kujenga kujiamini.
“Nakuomba uhusiano wetu asiujue mtu yeyote pale ofisini!”

Kimya kidogo kikapita, kisha Mohsein akasema, “Kwa nini unasema hivyo? Au unadhani mimi ni mropokaji?”
“Sina maana hiyo, lakini sitaki watu wajue!”

“Ni hilo tu?” Mohsein aliuliza kiwepesi.
“Hofu ondoa, labda uje utamke wewe mwenyewe kwa watu!”

Dina akagundua jinsi Mohsein alivyoijibu hoja hiyo kiwepesi. Akaingiwa na wasiwasi.
“Mohsein please, niko serious!” alisema kwa sauti yenye kusisitiza.

“Mbona unaonekana kama una hofu fulani?”

“Ni kweli nina hofu Mohsein…stori yake ni ndefu, lakini nataka ujue kuwa, yeyote atakayeufahamu uhusiano wetu na habari hizo zikamfikia Richard, ujue ama sote kwa pamoja au mmoja wetu, kibarua kitaota nyasi!”

“Mbona sikuelewi Dina?” Mohsein aliuliza na safari hii sauti yake iliondoka kwenye kujiamini na kutwaliwa na wasiwasi.

“Ni stori ndefu kama nilivyokwambia, kesho asubuhi tutakapokutana ofisini nitakuelezea.”

Siku ya pili walipokutana, Dina alimpa ukweli wote Mohsein!

Ikawa ni mara ya kwanza Mohsein kutambua kuwa, Dina ana mchumba na harusi ingefanyika baada ya miezi mitatu ijayo. Akatajiwa jina la mchumbiaji na kukiri alikuwa hamjui. Lakini kibaya zaidi ni pale alipoupata mshituko uliomwogopesha, aliposikia kuwa, hata Richard ni mmoja kati ya watu wanaowania kumuoa Dina!

* * * * *

Richard alirudi kutoka Morogoro baada ya siku tatu akaenda ofisini moja kwa moja. Alifika ofisini saa sita mchana, akawasalimu baadhi ya wafanyakazi aliojisikia kusalimiana nao. Aliwakuta Mohsein na Dina wakijiandaa kutaka kwenda kula chakula cha mchana. Tukio hilo la kuwaona Mohsein na Dina wakitaka kutoka pamoja likapenyeza mchomo mkali wa wivu moyoni mwake.

“Dina nisubiri!” Richard alimwambia Dina kwa sauti iliyoonyesha ana jambo muhimu analotaka kulizungumza kwake. Kisha akatoka ofisini humo bila ya kusubiri jibu.

Dina na Mohsein wakaangaliana kwa macho yaliyoingiwa na wasiwasi, hofu ikaingia kwenye mioyo yao na kila mmoja akaingiwa na sintofahamu ya agizo hilo.

“Kwani vipi?” Mohsein aliuliza kwa sauti ya chini kama vile alikuwa akiogopa Richard asisikie huko alipo.

Dina akayainua na kuyashusha mabega yake. “Sijui!” alijibu. Mohsein akauangalia mlango wa ofisi yao kama vile alitarajia Richar angerudi tena. Kila mmoja akawa ameingiwa na hofu kuwa, Richard amekwishapata habari ya mahusiano yao, lakini kila mmoja akashindwa kumwuliza mwenzake swali hilo.

“Kwa hiyo nikusubiri?” Mohsein aliuliza huku sauti yake ikionyesha kujiamini kwake kulishaondoka.

“Sio vizuri akituona tukiondoka pamoja!” Dina alisema kwa sauti ya kuonya.
“Wewe nenda kale!”

Mohsein akawa kama aliyepigwa butwaa na jibu la Dina.
“Kwa hiyo hutokuja?” aliuliza huku akionyesha kutoridhishwa na uamuzi wa Dina.

Dina akaonekana kidogo kama amechanganyikiwa.
“Agh, Mohsein we nenda!” alisema huku sauti yake ikiwa na hasira. Hakutaka Richard awakute wakiwa bado wako pamoja humo ofisini ingawa ni ofisi yao kikazi. Hatia ilikuwa imemjenga. Kwa mara ya kwanza alijitambua kuwa, alianza kumwogopa Richard!

Mohsein akamwangalia Dina kwa uso uliohamanika, akasema kwa unyonge, “Poa.” Kisha akatoka na hali ile ile ya unyonge.

Kila mmoja alikiri moyoni kuwa, ujio wa Richard umekuja kutibua fungate yao ya siku mbili iliyokuwa imewapa uhuru humo ofisini kwa kuonyeshana kuwa ni wapenzi wapendanao huku wakifanyiana dalili zote za kimahaba na wakati mwingine walifikia hadi kujiamini kwa kuitumia nafasi ya kuwepo kwao wawili ofisini kunyonyana ndimi zao.

Ilikuwa kama vile Paka akiondoka… Ndivyo ilivyokuwa kwao!

Dina akiwa amebaki peke yake humo ofisini baada ya Mohsein kutoka, alijikuta akishindwa kuendelea na kazi. Akili ilikuwa imekwama kuwaza jambo lolote, agizo alilopewa na Richard lilikuwa kama lililoitia akili yake ugonjwa wa kiharusi.

Laiti isingekuwa mahusiano ya mapenzi aliyoyaanzisha na Mohsein, kamwe agizo hilo lisingemshitua! alijiambia moyoni. Angejiamini kama alivyokuwa akijiamini siku za nyuma wakati alivyokuwa akiitwa na Richard ofisini na alikuwa hamwogopi hata pale walivyokuwa wakizungumza ana kwa ana. Lakini tukio hilo la kuanzisha mahusiano ya mapenzi na Mohsein, ghafla kukawa kumeibadilisha hali hiyo. Sasa alianza kumwogopa Richard tena kwa kasi kubwa kuliko alivyotarajia. Ikawa kama vile alikuwa amejitengenezea mwenyewe Shetani wa kuja kumtisha!

Maswali yaliyotawaliwa na hofu kuwa huenda taarifa za mahusiano yake na Mohsein zimekwisha kumfikia Richard yalikuwa yakirindima kichwani mwake na kuhisi hicho ndicho alichokuwa akiitiwa. Akajiuliza, ni kipi hasa alichokuwa akikihofia? Ni ile hofu ya kugundulika mahusiano yake na Mohsein? Au ni kufukuzwa kazi baada ya kugundulika mahusiano hayo? Dina akakosa utulivu wa akili wa kuchanganua mchanganuo huo!

Richard akaufungua mlango wa humo ofisini bila kupiga hodi. Hakuingia moja kwa moja, alisimama mlangoni na kuuzuia mlango usijifunge. Kitendo hicho kikamshitua Dina, lakini kibaya zaidi ni pale alipoonyesha dalili zote za kumwogopa Richard! Bahati iliyoje, Richard akawa hakuuona woga uliokuwepo usoni mwa Dina.

“Njoo ofisini!” Richard alisema kwa sauti kavu, kisha bila ya kupoteza muda wala kuhangaika kumchanganya machoni Dina, akatoka.

Dina akashusha pumzi, akajizoa kitini na kusimama, kisha akatoka ofisini. Alimkuta Richard amekaa nyuma ya meza akiandika, Dina akaenda kukaa kwenye kiti kilichopo mbele ya meza ya Richard kwa nidhamu ambayo hajawahi kuifanya tokea siku aliyoanza kuingia kwenye ofisi hiyo.

Uingiaji wa Dina humo ofisini haukumfanya Richard auinue uso wake kumwangalia ingawa alijua kuwa ni Dina ndiye aliyeingia. Aliendelea kuandika kama vile hakuna mtu aliyeingia. Dina akaenda kukaa kwenye kiti cha wageni kilichopo mbele ya meza ya Richard. Kitendo hicho nacho hakikumshitua Richard kuinua macho yake kumwangalia mtu aliyekaa. Dakika kadhaa zilipita huku akiendelea kuandika na bila ya kumsemesha Dina. Hali hiyo ikawa inamtesa Dina Kisaikolojia na kujikuta akihofia hata kujikohoza. Ilikuwa ni kama vile ni zamu ya Richard kumtesa Dina!

Hatimaye Richard aliacha kuandika, akauegemea mgongo wa kiti kwa aina fulani ya ujivuni na kumtazama Dina kwa mara ya kwanza tokea alivyokuwa ameingia.

“Dina,” Richard aliita kwa sauti ya kuonyesha yeye ni bosi. Dina aliitikia kwa sauti iliyokwama kusikika vizuri.

Kabla ya kuendelea kuzungumza, Richard akaonekana kama vile ameigundua hali aliyokuwa nayo Dina, akaonyesha dalili ya kutaka kumwuliza kama alikuwa anaumwa.

“Jumatatu tunakwenda Arusha kikazi!” Richard alisema ghafla. Ule mwonekano aliouonyesha kutaka kuiulizia afya ya Dina ukawa umetoweka usoni mwake. “Tunakwenda kufanya ukaguzi wa ndani wa mahesabu. Huenda ikatuchukua wiki moja au zaidi,” akanyamaza na kumwangalia Dina machoni.

Dina akayakwepesha macho yake. Kauli ya Richard ilikuwa shambulio alilokuwa hakujiandaa nalo.

“Ni moja ya utaratibu wa kazi zetu ulivyo,” Richard akaendelea bila ya kusubiri jibu la Dina. “Huwa ni kawaida kwenda mikoani kufanya ukaguzi wa ndani wa mahesabu kila baada ya muda fulani, hutegemea na mkoa wenyewe. Juzi na jana nilikuwa Mororgoro kwa shughuli kama hiyo. Kwa hiyo mkoa unaofuata ni Arusha. Jiandae kwa safari hiyo!”
“Tunakwenda wangapi?” Dina aliuliza.

“Wawili, mimi na wewe!” Richard alijibu kisha akamwangalia Dina kwa macho ya kuuliza kama ana swali jingine.

Dina akabaki kimya.

“Sawa?” Richard aliuliza na kumwangalia Dina kwa mtazamo wa kumsanifu.

Dina alionyesha kusita, kisha akajibu kwa sauti ndogo yenye unyonge kwa kusema, “Sawa.”

* * * * *

Mohsein alirudi ofisini baada ya kuutumia muda wa kula mchana kwa kunywa soda na keki, hamu ya kula ilikuwa imemtoka! Alimkuta Dina akiwa amejiinamia ofisini. Kumwona Dina akiwa kwenye hali hiyo, moja kwa moja akajua Dina amepata tatizo na bila ya kujiuliza, akahisi tatizo hilo litakuwa limesababishwa na Richard!

“Vipi?” Mohsein aliuliza akiwa ameinama huku akijaribu kukiinua kichwa cha Dina aliyekuwa amekilalisha juu ya meza.

Dina akakitikisa kichwa chake kumtaka Mohsein amuachie. Mohsein akahisi kuna tatizo kubwa kuliko alivyolichukulia awali.

“Dina!” Mohsein aliita akiwa ameuondoa mkono wake kichwani kwa Dina na kuufanya mhimili wake wa kuegemea kwa kuukita juu ya meza.

“Mhh,” Dina aliitikia bila ya kuuinua uso wake.

Mohsein akahisi Dina alikuwa akilia. Hali hiyo ikamchanganya! Akapatwa na kihere, “Kwani vipi?” aliuliza. Badala ya kujibu, Dina akashusha pumzi kwa nguvu huku akijiinua na kukaa vizuri. Hakuwa alikuwa akilia, lakini alionekana kuikaribia hali hiyo. Akaangalia juu ya meza kisha asiseme lolote.

“Richard amekwambiaje?” Mohsein aliuliza huku akiwa na uhakika ni Richard ndiye aliyemfikisha Dina kwenye hali hiyo.

“Amenitaka niende naye Arusha kikazi!” Dina alisema bila kuondoa macho yake mezani. Sauti yake ilikuwa imenyongea na uso wake kuonekana kuzidiwa na mawazo.

“Ahh!” Mohsein aliguna kwa sauti iliyotaharuki.
“Lini?” aliuliza.
“Jumatatu!”

“Amekwambia mnaenda wangapi?” Mohsein aliuliza kwa kihoro cha kuogopa jibu atakalopewa.

“Mimi na yeye!”

Mohsein akatoa tusi la kumtukana mzazi wa Richard!

Mchomo wa wivu ulikuwa umepenya moyoni mwa Mohsein, akaonekana kuchoka kama aliyeibuliwa kutoka kwenye msukule, akaongoza taratibu hadi kwenye meza yake na kukaa. Nguvu zilikuwa zimemuishia!

“Jamaa amepania!” Mohsein alisema kwa sauti ndogo na kuonekana kama aliyekuwa akiongea peke yake.
“Umemjibu nini?” safari hii aliipandisha juu sauti yake kutaka Dina asikie.

Dina akamwangalia Mohsein kwa mara ya kwanza tokea alivyokuwa ameingia.
“Ulitaka nimwambieje?” naye aliuliza kwa sauti ya taratibu huku akionekana hana cha kujitetea.

“Mwambie unaumwa huwezi ukaenda!” Mohsein alibwata na kuonyesha wivu ulikuwa ukichukua nafasi yake kumchanganya.

Dina hakujibu. Kimya kikapita kati yao.

Kwa mara ya kwanza, Mohsein akagundua ni kwa kiasi gani alikuwa akimpenda Dina na kwa wigo gani aliokuwa akimhitaji awe naye karibu. Wivu ulikuwa ukirindima na kumtafuna. Alihofu safari hiyo Richard aliipanga kwa kuikusudia kwa lengo la kupata faragha atakayoitumia kumbembeleza Dina ili atembee naye kimwili.

“Kwa hiyo?” Mohsein aliuliza kama mpumbavu aliyechanganyikiwa huku akimwangalia Dina.

“Kwa hiyo?” Dina alirudishia swali kwa sauti ile ile ya taratibu huku akionyesha kushangaa kwa

kutomwelewa Mohsein.

“Nenda kamfahamishe kuwa unaumwa na hutoweza kwenda safari hiyo!” Mohsein alisema kwa msisitizo.

“Wacha tu, niende!” Dina alisema kwa mkato.

“Uende naye Arusha?” Mohsein aliuliza kama vile hakuamini alichokisia.

“Ghafla nimwambie kuwa naumwa?” Dina alisema.
“Atanishangaa kumlalamikia hivyo baada ya kutajiwa safari!”

“Yeye si alikuwa Morogoro! Utamwambia una karibu siku mbili ulikuwa unaumwa!”

“Atataka kujua kwa nini sikumwambia palepale? Na atataka kujua kama kazini nilikuwa nakuja siku zote. Akijua kama nilikuwa nakuja siku zote, atajua siumwi bali nasingizia ugonjwa kwa kuikataa safari!”

Mohsein akanywea! Akaonekana kushindwa kuendelea kumshawishi Dina aikatae safari hiyo.

“Kwanza wewe kazi yenyewe hujaijua vizuri, kwa nini asinichukue mimi?” Mohsein alilalamika na kuuonyesha dhahiri kuumizwa na wivu aliokuwa nao. “Kwani wewe Arusha huna ndugu?”

Uso wa Dina ukaonyesha mshangao kutokana na swali aliloulizwa. Akatingisha kichwa kukataa.
“Sina!” alisema.
“Kwa nini unaniuliza hivyo?”

“Kama ungekuwa na ndugu yeyote ningekushauri ukalale kwake baada ya kufika Arusha.”

Dina akatingisha tena kichwa na kusema, “Sina!”

“Mimi ninaye dada yangu, anaishi Kaloleni. Unaonaje nikiongea naye?”

“Ili nifikie kwake?” Dina aliuliza, akaonekana kumshangaa Mohsein. “Bila ya kufanya hivyo huyu mshamba atakusumbua mkifika Arusha!

Atataka mfikie hoteli moja na pengine hata kukodi chumba kimoja!”
“Hilo halitawezekana!” Dina alisema na sauti yake ilijenga ubishi. “Eti nini, achukue chumba kimoja? Hawezi akaniburuza kirahisi hivyo! Si bora niache hiyo kazi yenyewe!”

Kauli hiyo ikamfanya Mohsein kutaka kuiteka nyara hoja hiyo ili amshawishi Dina bora aache kazi kuliko kwenda Arusha! Mtazamo wa wivu ndio uliokuwa ukimtesa, kwa sababu alihofu endapo Dina atakubali kwenda Arusha, ni wazi kuwa Richard atakuwa na nafasi kubwa ya kumpata Dina! Lakini moyo wake haukumpa ushujaa wa kuyatamka hayo. Alijua ungekuwa ni ushauri wa kijinga uliotokana na wivu, alihofu Dina angemdharau. Badala yake akaongea kwa kujitetea huku sauti yake ikinyongea. “Nina hakika mkifika Arusha atakuletea upuuzi wa kukutaka kimapenzi, ukimchekea shauri yako!”

Dina akafanya tabasamu dogo kumwonyesha Mohsein kuwa amemuelewa. “Mimi sio mtoto mdogo, hawezi akanilazimisha!”

“Hata hivyo, bado ukifika unayo haki ya kukataa kukaa naye hoteli moja! Hakuna sheria itakayokulazimisha kukaa naye hoteli moja!”

“Mohsein,” Dina aliita kwa utulivu, kisha akaendelea, “Pamoja na kwamba mimi na Richard tuna uadui wetu, lakini bado ni bosi wangu. Kuna mambo ambayo naweza kumkatalia, lakini sio ya kikazi! Safari tunayokwenda ni ya kikazi na hata kama tutakaa hoteli moja bado litakuwa ni suala la kikazi. Lakini pale atakapotaka kunilazimisha kukaa chumba kimoja na yeye, hilo litakuwa sio suala la kikazi tena na nitakuwa na haki ya kumkatalia!”

***RICHARD ameamua kuvunja ukimya katika vita hii anataka kusafiri na DINA kikazi…je? Kitatokea nini huko mbeleni……MOHSEIN ana wasiwasi mkubwa sana juu ya jambo hili…..WIVU umemtawala bila kutarajia…….
***VIPI harakati za John na waganga wa jadi!!

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI

“Hata hivyo, bado ukifika unayo haki ya kukataa kukaa naye hoteli moja! Hakuna sheria itakayokulazimisha kukaa naye hoteli moja!”

“Mohsein,” Dina aliita kwa utulivu, kisha akaendelea, “Pamoja na kwamba mimi na Richard tuna uadui wetu, lakini bado ni bosi wangu. Kuna mambo ambayo naweza kumkatalia, lakini sio ya kikazi! Safari tunayokwenda ni ya kikazi na hata kama tutakaa hoteli moja bado litakuwa ni suala la kikazi. Lakini pale atakapotaka kunilazimisha kukaa chumba kimoja na yeye, hilo litakuwa sio suala la kikazi tena na nitakuwa na haki ya kumkatalia!”

Kauli hiyo angalau ikampa matumaini Mohsein, wivu wake ukashuka kwa asilimia fulani, lakini kitendo hicho cha Richard kutaka kusafiri na Dina bado kilikuwa kikimteketeza! Akatamani achukue ruhusa ya dharura ili naye aende Arusha kivyake vyake, akiamini kuwa karibu na Dina ndio njia pekee ya kumlinda.

Hadhari aliyopewa na Dina kuwa amechumbiwa, ikaonekana kusahaliwa na Mohsein, akajiona yeye ndiye mwenye haki ya kummiliki Dina kuliko mtu mwingine yeyote!

***

JOHN aliwasiliana na baba yake na kumtaarifu kuwa, lile kusudio lake la awali la kutaka ndoa yake na Dina ifungwe mapema, sasa halipo tena. Sababu ile ile ya barua ambayo Dina alimwonyesha kama kikwazo kinachozuia kufunga ndoa mapema, ndio aliyoitumia kumwambia baba yake.
“Kwa hiyo mmekubaliana?” baba yake alimwuliza.

“Alikuwa tayari tufunge ndoa mapema, lakini ni sababu hiyo ya barua ndio imeleta kikwazo,” John alijitetea.
“Kwa hiyo sikumwambia tena kama ulikuwa ukimhitaji.”

“Hakukuwa tena na ulazima, hata mimi nilitaka kuzungumza naye kwa suala hilo hilo. Lakini vipi kuhusu suala la upelekaji mahari, si bado liko pale pale?”
Kuulizwa swali hilo kukamkumbusha John kusudio lake la kutaka kwenda kijijini kwao kwa ajili ya kumfanyia ushirikina Dina. Akahofu pesa ambazo angekwenda nazo zisingetosha baada ya kuambiwa mganga atakayekwenda kumwona huwa anatoza gharama kubwa kutokana na sifa kuwa, wateja wake wengi ni vigogo wa Serikali. Taarifa hizo zikamuweka kwenye hitaji la kuongeza pesa ili aweze kuikabili gharama atakayotajiwa. Kwa kuwa hakuwa na pesa nyingine za ziada ya akiba zaidi ya zile za mahari zilizokuwa zikisubiri kupelekwa kwa wazazi wake Dina, John akaamua alisimamishe kwanza zoezi la kupeleka mahari na pesa hizo zikafanye kazi ya ushirikina!

“Kwa kuwa ndoa yenyewe itafanyika baada ya miezi mitatu, nadhani hakuna haraka ya kupeleka mahari mapema,” John alimwambia baba yake.

“Ni wewe tu, hata ukisema zipelekwe leo au kesho ni wewe mwenyewe na maamuzi yako!” baba yake alimjibu.

Safari ya kupelekwa mahari ikaahirishwa! Umuhimu wa kutaka kumdhibiti Dina kwa kumfanyia ushirikina ukachukua nafasi.

Kuchelewa kuyapeleka mahari hayo hakukuisumbua akili yake kwani aliamini, endapo Dina atatengenezwa na kuinamishwa kwa imani za kishirikina, basi kutampa uwezo wa kumwambia Dina waanze maisha ya kuishi pamoja kama mtu na kimada wake kisha ndoa ingefuata baadaye.

Aliamini hilo lingewezekana kwa sababu madawa yangemdhibiti Dina na atakuwa akizipokea amri zake kwa kila atakachomwambia.
Huo ungekuwa ni ushindi mkubwa kwake wa kumsambaratisha Richard!

Siku ya pili, John alionana na Dina, akamuaga kwa kumwongopea kuwa anatarajia kusafiri kwenda kijijini mwishoni mwa juma kwa ajili kuwapelekea taarifa za harusi wazee wake wengine walioko huko na kuahidi angerudi Jumatatu.

Jumatatu hiyo ikamkumbusha Dina kuwa ndio siku ambayo yeye na Richard watasafiri kwenda Arusha!

Awali, Dina alikuwa amepanga amtaarifu John safari yake hiyo ya kwenda Arusha. Alipanga amwambie siku ya Jumapili asubuhi, siku ambayo ni kawaida yake kuitumia akiwa nyumbani kwa John hadi jioni kabla ya kurudi nyumbani kwao. Lakini hakupanga kumwambia kuwa angesafiri na Richard, alijua kauli hiyo ingemchanganya John. Badala yake angemwambia kuwa anasafiri kwenda Arusha kikazi kwa muda wa wiki moja. Lakini baada ya John naye kumwambia alikuwa akitarajia kusafiri, Dina akabadili azma yake ya kutaka kuaga. Akaamua asubiri hadi John atakaposafiri, kisha ampigie simu huko kijijini atakakokuwa amekwenda amfahamishe kuwa na yeye amepata safari ya ghafla ya kikazi kwenda Arusha! Alijua kwa kufanya hivyo angekuwa ameondoa bugudha ambayo ingempata kutoka kwa John kama angemuaga wakiwa Dar es Salaam, aliamini John angeleta ligi ya kuuliza maswali lukuki yenye mrengo wa wivu ambayo yangemhusisha Richard na kutaka kujua kama naye angesafiri, lakini kwa kupitia kwenye simu aliyaona maswali hayo yasingempa wakati mgumu kuliko kama ingekuwa ni ana kwa ana!

Alikwishaanza kukerwa na tabia za wivu zilizoanza kuonyeshwa na John alizokuwa akizielekeza kwa Richard dhidi yake tokea aanze kazi kwenye kampuni ya mzee Ken!

* * * * *

Hadi ilipofika siku ya Ijumaa mchana, Dina alikuwa hajaambiwa lolote kuhusu kujiandaa na safari aliyoambiwa. Alitarajia kuambiwa mapema mipango ya kujiandaa na safari itakavyokuwa, lakini hadi kufika siku hiyo hakukuwa na dalili zozote kutoka kwa Richard zilizoonyesha kuwa angelizungumzia jambo hilo.

Alishangaa kuona, tangu Richard alipomzungumzia kuhusu safari hiyo, hajawahi tena kulizungumza jambo hilo japo kwa kumdokeza muda wa kuondoka au safari hiyo itaanzia kituo gani. Ukimya wa kutoambiwa ulimuweka njia panda kwa sababu siku hiyo ya Ijumaa ndio siku ya mwisho ya wiki kufanya kazi, siku zinazofuata za Jumamosi na Jumapili ni siku za mapumziko. Aliamini hata kama wangeondoka siku hiyo ya Jumatatu kama alivyokuwa ameambiwa na Richard, pengine kwa kuondokea ofisini kwa gari la ofisi au la Richard mwenyewe, bado alistahili kuarifiwa mapema ili hiyo Jumatatu aweze kuja kisafari.

Ukimya huo wa Richard haukuwa ukimsumbua Dina peke yake, lakini hata Mohsein ulikuwa ukimgusa, tena kwa kiasi kikubwa kutokana na kuteswa na wivu. Safari ya Dina kuondoka akiwa na Richard ilikuwa ikimuuma kila alipokuwa akiifikiria. Mawazo ya wivu yalikuwa yakimteketeza kila alipokuwa akiijenga picha ya uwepo wa peke yao kwa watu hao wawili watakapokuwa Arusha. Sononeko la kuchukuliwa kwa Dina kwenye mikono yake na kutenganishwa naye lilikuwa likimwadhibu. Bila ya kujijua, hali hiyo ikamfanya Mohsein apoteze uzito ndani ya siku hizo chache za kusubiri Dina na Richard waondoke kwenda Arusha.

Safari hiyo ya Dina na Richard kwenda Arusha ilikuwa kama chachu iliyomzindua Mohsein kuujua uzito wa penzi lake lilivyozama kwa Dina. Awali alivyokuwa ameambiwa na Dina kuwa awe mwangalifu ili Richard asiyajue mahusiano yao kutokana na sababu zilizoelezwa, fikra za Mohsein zikamuweka kujiona kama shujaa aliyebahatika kumpata Dina na kuhisi burudiko la kumuwazia bosi wake anavyohangaika kupapata mahali alipopata yeye kiulaini na kumwona Richard kama fala fulani aliyekuwa hatakiwi kimapenzi na Dina!

Lakini tokea Richard alivyorudi kutoka Morogoro na kumjulisha Dina kuwa atasafiri naye kikazi kwenda Arusha, upepo wa kumwona Richard kuwa ni 'fala fulani' ukawa umegeuka! Wivu ukajitengeneza, ufala ukamgeukia yeye! Akaanza kumlalamikia Dina kwa kumtuhumu Richard kuwa anatumia madaraka yake kumlazimisha kusafiri naye kama njia ya kwenda kumlazimisha kufanya naye mapenzi! Ingawa Dina alimpa moyo na kumhakikishia kitu kama hicho hakiwezi kutokea kwake, bado Mohsein alikosa imani. Lolote linaweza likatokea kati yao! Fikra hizo zikaendelea kumtafuna Mohsein.

Lakini ukimya uliokuwa ukiendelea kujitokeza kuhusu safari hiyo huku Dina akidai kuwa, Richard hajamwambia lolote jingine linalohusiana na maandalizi ya safari hiyo huku wiki ikiishia kukatika, Mohsein akaanza kupata aina fulani ya faraja kuwa huenda safari hiyo haipo tena. Yeye kwa upande wake na kama ilivyokuwa kwa Dina, wote kwa pamoja walitaka safari hiyo ivunjike, na ukimya huo ulivyokuwa ukiendelea wakaanza kupata matumaini kuwa, pengine upo uwezekano wa safari hiyo kutokuwepo tena na huenda ikawa ndio chanzo cha ukimya huo!

Wivu, chuki na husda, Mohsein alikuwa amemuwekea Richard, akawa anaomba Richard afikwe na mabaya, kama vile kuumwa ghafla au kutokee jambo lolote litakalomzuia asiweze kusafiri safari hiyo na badala yake safari hiyo imwangukie yeye! Wakati akiwa na mtafaruku wa msongo mkali wa mawazo na kukiri kumpenda Dina kwa kasi ya ajabu na kujiona ndiye mwenye uhalali wa kummiliki, Mohsein akawaza kuwa, endapo safari hiyo itakuwepo kama Richard alivyopanga, basi ni vyema akafanya mpango kati ya Jumamosi au Jumapili amwombe Dina aje nyumbani kwake ili awahi kufanya naye mapenzi angalau kuondoa usongo aliokuwa nao kabla ya Dina hajasafiri. Aliamini kufanya mapenzi na Dina kungekuwa ni aina ya faraja ambayo ingempunguzia kukabiliana na machungu wakati Dina atakapokuwa hayupo, na angeitumia nafasi hiyo wakati wa kufanya naye mapenzi kumsisitiza Dina asikubali kabisa kumpa penzi Richard watakavyokuwa wapo Arusha!

Wakiwa ofisini mchana huo katika hali ile ya sintofahamu ya uwepo wa safari hiyo ya Arusha, Mohsein akaona bora autumie wakati huo kumshawishi Dina aje nyumbani kwake siku inayofuata kwa kusudio alilokuwa amelipanga la kufanya naye mapenzi.

"Dina," John aliita kwa kujiamini.
"Unaonaje kesho…" akasita kuendelea baada ya kuusikia mlango wa ofisini kwao ukigongwa. Akaonekana kuchukizwa, "Karibu!" alisema kwa hasira.

Akaingia msichana ambaye ni mfanya usafi na mpika chai wa ofisini. Akasimama na kumwangalia Dina.
"Dada Dina," alisema. "Bosi Richard anakuita ofisini kwake!"

Mohsein akahisi mfano wa kisu kikali kikichana katikati ya moyo wake! Akashindwa hata kumwangalia Dina wakati Dina alipoinuka. Dina akaiona hali iliyomkuta Mohsein, akaamua kuondoka bila ya kusema lolote kwa Mohsein. Mohsein akamwangalia Dina alipokuwa anauvuta mlango wa ofisini kwa ajili ya kuufunga

wakati akitoka, akatamani kumuita na kumwambia asiende!

Dina akaufunga mlango nyuma yake baada ya kutoka, Mohsein akabaki anasaga meno huku akiuangalia mlango huo ukimsuta!
Dina alimkuta Richard akizungumza kwenye simu wakati alipokuwa akiingia ofisini kwake. Safari hii Richard aliupunga mkono wake kumkaribisha kwenye kiti huku akiendelea kuzungumza na simu. Dina akaenda kukaa na kubaki kimya huku akijiangalia kucha zake za mikono na wakati mwingine kuyazungusha macho yake kuziangalia kuta za ofisi hiyo kama kwamba ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuingia ofisini humo.

Richard alimaliza kuzungumza kwenye simu na kumwangalia Dina huku akiirudisha simu juu ya meza. Akafanya tabasamu dogo. “Nilikwambia safari ni Jumatatu vile?” alisema.
Dina aliitikia.

“Ulishawahi kufika Arusha?”

“Bado,” Dina alijibu kwa sauti ya chini. Ghafla alijiona anazungumza na mtu aliyemzoea.

“Tiketi yako,” Richard alisema huku akimpa Dina bahasha yenye rangi mchanganyiko buluu na nyeupe iliyokuwa na nembo ya kampuni yao.
Dina aliipokea na kuiweka mapajani mwake bila ya kuifungua.

“Na hizi pesa ni za teksi,” Richard alisema tena na kumpa Dina bahasha nyingine iliyofanana na ile ya kwanza.
Bahasha hiyo nayo, Dina aliipokea na kuiunganisha na ile ya kwanza kwa kuiweka pale pale mapajani mwake, nayo hakuifungua.

“Hakikisha unawasili Uwanja wa Ndege saa kumi na mbili na nusu asubuhi, utanikuta nikikusubiri.”
Lilikuwea ni shambulio jingine ambalo Dina alikuwa hakujiandaa nalo!

Alikuwa hajawahi kupanda ndege! Uelewa wa kuwa atasafiri kwa ndege ulimyumbisha akili yake. Kila kitu alikiona ni kigeni kwake, alikuwa hajui teksi itakayompeleka Uwanja wa Ndege itamgharimu kiasi gani na atakapofika uwanjani hangejua angeanzia wapi. Akili yake ikawa tegemezi kwa wazazi wake ambao walikuwa na uzoefu wa kusafiri kwa ndege miaka ya nyuma kabla ya kustaafu kazi kwa baba yake aliyekuwa akisafiri kikazi kwa usafiri huo ambapo wakati mwingine alikuwa akisafiri na mama yake.

Lakini pia kuwepo kwa Richard katika safari hiyo na uwepo wake wa kutangulia kufika Uwanja wa Ndege kwa ajili ya kumsubiri yeye nako kulimpa matumaini ya kuwa atakuwa na mtu mzoefu kwenye safari hiyo. Wazo la kumuwazia Richard kuwa ni sehemu ya msaada atakaokuwa akiuhitaji wakati wa kuingia na kuwepo kwake kisafari ndani ya ndege, likamfanya akiri kuwa lingeuleta tena ukaribu wa mahusiano yao binafsi yaliyoasiana kwa muda mrefu.
Wazo hilo likamfanya alikumbuke onyo la Mohsein!

* * * * *

Kujua kuwa Dina atasafiri kwa ndege kulimtia wazimu Mohsein! Bao la kisigino! Alikiri kufungwa bao hilo. Aliiona kete iliyotumiwa na Richard ilikuwa ni ya aina yake, kete yenye ushawishi kwa mtu kama mwanamke, au mwingine yeyote mwenye kupatiwa huduma kama hiyo! Yeye mwenyewe alishawahi kusafiri na Richard kwa safari za kikazi kama hizo na kwa mikoa tofauti, lakini hakuna hata safari moja aliyowahi kusafiri kwa ndege. Safari zote Richard alizowahi kusafiri kwa ndege za ndani au nje ya nchi, alisafiri peke yake.

Kwa mara ya kwanza uelewa ukaanza kumjia kuwa, vita aliyokuwa akijaribu kupigana ilianza kumuelemea mapema. Mwanzo huo uliofanywa na Richard kwa kumkabidhi Dina tiketi ya ndege, zilikuwa dalili za wazi zinazomthibitishia kuwa, alikuwa anashindana na mtu mwenye fedha na aliyepania kuitumia kuhakikisha anaununua ushindi kwa hali yoyote ile! Hali hiyo ilimchanganya na kujikuta akishindwa kujizuia.

“Unaona!” Mohsein alibwata mbele ya Dina na kuonekana kupoteza kabisa mhimili wa akili kichwani mwake na kujikuta akisimama. “Mimi nimeshasafiri naye mara kibao, hakuna hata siku moja aliyowahi kunisafirisha kwa ndege! Mi nakwambia hii safari sio ya kikazi, ina lengo lake! We utaniambia!” akamwangalia Dina kwa sura iliyojenga wasiwasi. “Kwa nyie wanawake..!” akasita, kisha akasema. “Sijui!”

“Nakuomba uondoe presha Mohsein,” Dina alisema kwa utulivu. “Unajipa presha za bure, mimi nimekwishakwambia atakuwa anajisumbua! Au huniamini?”

“Kukuamini nakuamini,” Mohsein alisema kwa sauti yenye kujitilia mashaka na kauli yake mwenyewe. Alikuwa hamwangalii Dina usoni, hasira ilikuwa bado ikitawala usoni mwake na alikuwa amenuna!

“Sasa kwa nini unapandisha presha?”

Mohsein akasikitika. “Inauma, Dina!” alisema kwa sauti iliyomwonyesha ni kweli alikuwa akiumizwa na maumivu aliyokuwa akiyasikia. Kisha akakiangalia kiambaza cha ukuta wa ofisini, akaganda kama aliyezubaa, na kubaki hivyo.

Dina akakosa la kuzungumza, alikwisha kumwona Mohsein akiwa kwenye kiwango cha juu cha wivu.

“Nataka kesho uje nyumbani!” Mohsein alisema ghafla huku akimwangalia Dina. “Saa ngapi utakuja?”

Dina akaonyesha mshangao usoni mwake.
“Kuna nini?” aliuliza.
“Uje tuagane!”

Dina akawa mwepesi kukijua kilichomo kichwani mwa Mohsein. “Kesho sitokuja!” alisema bila ya kumwangalia usoni Mohsein.

“Basi fanya Jumapili!”

“Nayo pia itakuwa ngumu kuja!”

Mohsein akajenga ndita kwenye paji lake la uso.

“Kwa nini?” aliuliza akionekana kuwa na aina ya kisirani.

“Nitakuwa bize na kujiandaa kwa safari!”

Jibu hilo likamrudisha Mohsein kwenye kiti, akakaa kwa unyonge na kujiinamia. Akapiga kite huku akitingisha miguu yake. Akauinua uso wake na kumwangalia Dina usoni.
“Unajua kuwa nakupenda?” alisema.
“Najua,” Dina alijibu kwa sauti ya chini.

“Sidhani!” Mohsein alisema kulikana jibu la Dina. Nadhani unahisi kama nakupenda, lakini hujui ni kwa kiasi gani nakupenda Dina, labda pengine sijawahi kukutamkia neno hilo na ndio sababu ya kutoujua uzito wa mapenzi yangu kwako. Lakini, laiti ungeingia kwenye moyo wangu na kuujua uzito wa kukupenda kwangu, usingenifanyia hivi!”

Dina akaonyesha aina ya mshangao huku akimwangalia Mohsein. “Kwani nimekufanyia nini?”

“Usingenikatalia!”

Dina akafumba macho. Akataka kutamka neno, lakini akaishia kutanua papi za mdomo bila ya kuongea lolote.

Mohsein akaonekana kuwa mnyonge ghafla na mwenye kukata tamaa. “Ungekuwa unanipenda, ungekuja nyumbani tukaagana. Lakini huoni umuhimu huo kwa sababu bado hujanikubali!”

Imeshakuwa kero! Dina aliwaza. Ghafla akamfikiria John na safari yake ya kwenda kijijini kwao kwa ajili ya kutoa taarifa za harusi yao. Akapanga jioni baada ya kutoka kazini, aende kwake kwa ajili ya kuagana naye na mengine yatakayofuatia!

****

JOHN alikuwa amekaa upande wenye dirisha kwenye basi alilopanda asubuhi hiyo ya siku ya Jumamosi akielekea kwao kijijini. Upepo uliokuwa ukiingia kupitia dirisha alilokuwepo ulimfanya alirudishe kwa kulifunga kidogo kwa lengo la kuupunguza upepo unaoingia. Akatulia kwa kujiegemeza kwenye kiti na kufumba macho kama aliyekuwa akihitaji kulala. Akaanza kuyakumbuka mapenzi aliyofanya na Dina jana jioni baada ya Dina kuja nyumbani kuagana naye. Kisha akaifikiria hiyo safari yake…

Alijikuta akimlaani Richard na kumwona ndio chanzo cha safari hiyo, lakini pia akaamini safari hiyo ndio ya kukata mzizi wa fitina wa vita iliyopo kati yao. Kuifikiria vita hiyo kukamfanya amuwazie mganga anayemfuata huko kijijini ambaye kwake alikuwa kama silaha ya maangamizi anayoiendea. Akajenga matumaini jinsi mganga huyo atakavyolishughulikia tatizo lake kwa ukamilifu, na aliamini matunda ya safari hiyo ni kurudi na ushindi wa kuja kumdhibiti Dina kwa kumuweka kwenye kiganja chake! Aliyawazia madawa yenye nguvu za ajabu atakayopewa na mganga jinsi yatakavyoweza kumdhibiti Dina na kumfanya asiwe anavutiwa na mwanamume mwingine yeyote zaidi yake yeye!

Alikuwa na uhakika baada ya kurudi kutoka huko anakokwenda, juhudi za Richard za kutaka kurejeana na

Dina zitakuwa zimefikia ukingoni! Dina angekuwa haoni wala kusikia la mtu; wa kuonekana angekuwa ni yeye na wa kusikilizwa angekuwa ni yeye! Wengine wote wangeonekana ni wajinga fulani, mmoja wao akiwa ni Richard! Richard asingekuwa tena mwiba wa kuwa tishio la ndoa yake, na utajiri wake usingekuwa mali kitu kwa Dina!

Akalikumbuka tukio la kusindikizwa na Dina asubuhi ya siku hiyo hadi Kituo cha Mabasi yaendayo Mikoani cha Ubungo. Akaamini alikuwa akipendwa na Dina kwa dhati, lakini pia akakiri Richard alikuwa kidudu mtu anayetaka kuliharibu penzi hilo!

Aliiona safari hiyo ilikuwa na umuhimu kuliko hata ile ndoa aliyotaka kuiwahisha. Uamuzi wa kwenda kumwona mganga kwa lengo la kujihami ulikuwa wa maana na wenye manufaa kwake, kwa sababu lengo ni kumdhibiti na kummiliki Dina. Alitaka awe mmiliki pekee wa kummiliki, hakuhitaji mshirika kwenye umiliki huo. Hiyo ndio ilikuwa dhamira yake ambayo endapo itafanikiwa, suala la kufunga ndoa na Dina lisingekuwa na haraka tena. Angeweza kuichelewesha kidogo ili ajipange upya endapo pesa aliyokuwanayo mfukoni itaishia kwa mganga anayemwendea. Alikuwa na uhakika Dina asingeulalamikia uamuzi huo wa kuichelewesha ndoa kwa sababu angekuwa hana kauli ya kuipinga kauli yake!

Matumaini hayo yalimpa furaha wakati akiwa ndani ya basi, akaihisi furaha ya ushindi wa kumdhibiti msichana mzuri kama Dina ikielekea kwake!

John alijikuta akitabasamu peke yake; tabasamu la ushindi!

* * * * *

John baada ya kuwapa taarifa baadhi ya wazee wake wanaoishi kijijini kuwa anatarajia kufunga ndoa, akawaomba siku inayofuata wampeleke kwa mganga aliyewatajia jina ambalo alipewa na jamaa zake wa Dar es Salaam. Aliwadanganya wazee hao kuwa anataka akafanyiwe tiba ya kuimarisha mwili wake kwa kuogeshwa na kufukizwa madawa kabla ya kufunga ndoa. Wazee hao wakamhadharisha kuwa, mganga anayemtaka ana gharama kubwa kwa sababu haishi kwa kutegemea uganga kama waganga wengine walivyo, mganga huyu ni mfanyabiashara mwenye biashara zake. Wakamshauri wampeleke kwa mganga mwingine ambaye hayupo mbali na eneo wanaloishi.

“Lakini huyu niliyemtaja si ndio yule anayewashughulikia hadi Mawaziri waliopo Serikalini?” John aliuliza kwa lengo la kutaka kuupinga ushauri aliopewa.

“Hizo ni habari tunazosikia juu juu kuwa, anapokwenda Dar es Salaam huwa anakwenda kuwafanyia Mawaziri, lakini kwa hapa kijijini hatujawahi kumwona Waziri yeyote aliyewahi kuja kwa ajili yake. Labda ndio sababu inayomfanya atoze gharama kubwa kwa wateja wanaomwendea. Lakini kwa sisi wakazi wa hapa kijijini huwa hatumtumii, wote tunakwenda kwa mganga tuliyekwambia,” ulikuwa moja ya ushauri alioambiwa.

John hakukubaliana na ushauri aliopewa, akamg’ang’ania mganga aliyesifiwa na watu wa Dar es Salaam. Akapelekwa!

Gharama alizoambiwa zikawa kubwa mara mbili ya vile alivyofikiria baada ya kuelezea shida yake.

Akahakikishiwa kazi atakayofanyiwa ni ya uhakika na yeye mwenyewe atarudi hapo kijijini kuja kutoa mkono wa pongezi kwa mganga huyo. Ikamlazimu John alitumie fungu la mahari alilokuwa amelichukua kama akiba endapo pesa alizokwenda nazo zisingetosha. Akafanyiwa shughuli aliyoihitaji ambayo ilichukua siku mbili, akapewa masharti ya kufanya, mengine aliyaanzia hapo hapo kijijini na mengine akatakiwa aende akayamalizie akifika Dar es Salaam.

Ilipofika usiku wa Jumapili akijiandaa kutaka kulala ili asubuhi asafiri kurudi Dar es Salaam, akamfikiria Dina, akaona ni vyema amjulishe kuhusu safari yake hiyo ya kurudi Dar es Salaam, lakini badala ya kupiga, John akawahiwa kupigiwa na Dina!

Dina akamfahamisha John kuwa anaondoka kesho asubuhi kwenda Arusha kikazi itakayomchukua wiki moja huku akiilalamikia safari hiyo ilikuwa ni ya ghafla ambayo hakuitarajia.

Habari hizo zilimshitua John na kumchanganya baada ya kumkumbuka Richard!
“Unakwenda na Richard?” aliuliza.

“Bado sijajua, lakini sidhani kama na yeye atakwenda!” Jibu hilo likashusha presha za John.

“Kwa hiyo unasafiri peke yako?” John aliuliza.

“Bado sijajua. Nilichoambiwa, kesho asubuhi niwahi kufika ofisini kuna safari ya kwenda Arusha!”

* * * * *

***MOHSEIN amechomolewa na DINA kuhusu kuagana....RICHARD anamchanganya DINA kwa kumweleza kuwa atasafiri na ndege...je atamnasa???
*** JOHN ameenda kwa mganga ....vipi atafanikiwa shida zake??

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Dina akamfahamisha John kuwa anaondoka kesho asubuhi kwenda Arusha kikazi itakayomchukua wiki moja huku akiilalamikia safari hiyo ilikuwa ni ya ghafla ambayo hakuitarajia.

Habari hizo zilimshitua John na kumchanganya baada ya kumkumbuka Richard! “Unakwenda na Richard?” aliuliza.

“Bado sijajua, lakini sidhani kama na yeye atakwenda!” Jibu hilo likashusha presha za John.

“Kwa hiyo unasafiri peke yako?” John aliuliza.

“Bado sijajua. Nilichoambiwa, kesho asubuhi niwahi kufika ofisini kuna safari ya kwenda Arusha!”

* * * * *

Dina aliwasili Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere akiwa kwenye teksi na alisindikizwa na mama yake. Walimkuta Richard akiwa amekwishafika kama alivyokuwa ameahidi.

Kitendo cha kuwepo kwa Richard mapema hapo uwanjani kwa ajili ya kumsubiri Dina kilionekana kumfurahisha mama yake Dina na kuamini Dina alikuwa kwenye mikono salama. Alimchukulia Richard kama mwanae na alimwona Dina kama yuko na kaka yake. Kwenye maamkizi kati ya mama huyo na Richard, mama yake Dina alionyesha upendo kwa kijana huyo. Dina na Richard wakamuaga, akawaombea heri kwenye safari yao. Baada ya mama huyo kuondoka, Dina na Richard wakajikuta kwenye muunganiko wa pamoja na wakawa karibu kama vile hawakuwa na tofauti zao.

“Ulishawahi kusafiri kwa ndege?” Richard alimwuliza Dina mara tu baada ya mizigo yao kukaguliwa kwenye mashine za usalama wakati walipoingia ndani ya jengo la Uwanja wa Ndege.

“Bado,” Dina alijibu na kucheka kicheko kidogo cha kuondoa aibu kutokana na swali aliloulizwa. Kilikuwa kicheko cha kwanza na cha wazi kumchekea Richard baada ya kipindi kirefu cha uhasama wao!

Richard akamfahamisha Dina kinachotakiwa kufanywa hatua inayofuata wakati walipokuwa wakikaribia kujiunga na moja ya foleni inayoelekea kaunta ambako kulikuwa na vitenganishi vya majina ya mashirika tofauti ya ndege yenye kuashiria utoaji huduma wa wasafiri wa ndege zao.

“Watakuwekea namba ya kiti, kwa hiyo unatakaje? Tuchague kukaa pamoja au tukae viti tofauti?” Richard aliuliza wakiwa wanaikaribia kaunta.

Dina akafumba macho na kujenga tabasamu.
“Mi sijui chochote, mambo yote nakuachia wewe!” alijibu na kumtazama Richard.

“Basi tukae pamoja au unasemaje?”

“Yaani bado unaniuliza mimi?” Dina alisema na kumwangalia Richard kwa ncha za macho yake.

“Poa, nitamwambia karani atuweke pamoja.”

Walipoingia ndani ya ndege kabla ya kukaa kwenye viti vyenye namba walizoandikiwa, Richard akamwuliza Dina, “Utapenda kukaa dirishani?”
“Mi naogopa kuangalia nje!” Dina alisema kwa sauti ndogo ambayo hakutaka asikiwe na abiria waliosimama jirani ambao walikuwa wakihangaikia kuiingiza mizigo yao kwenye majaluba ya kuhifadhi mizigo ya ndani ya ndege.

Richard akakaa sehemu ya dirishani, Dina akakaa kando yake.

Dina alikuwa mwepesi kuiangalia hali iliyomo kwenye ndege na kuwaangalia baadhi ya abiria waliokuwa wakiendelea kuhangaika kupandisha mizigo yao kwenye majaluba na wakati huo huo wahudumu wa ndani ya ndege wakiwasaidia kuwaonyesha abiria mahali vilipo viti vyao. Akakumbuka kujifunga mkanda. Akadhani angeufunga mkanda huo kama vile ajifungavyo kwenye gari. Akaukamata mkanda uliopo kwenye kiti chake na kutaka kujifunga, akagundua uko tofauti na ule wa kwenye gari, hali hiyo ikamfanya aanze kubabaika kujifunga.

“Niangalie mimi ninavyojifunga mkanda!” Richard alisema ghafla baada ya kumwona Dina akijaribu bila mafanikio kuufunga mkanda huo.
Dina akamwangalia Richard alivyokuwa akijifunga, kisha na yeye akajaribu kuiga. Akapatia!

Richard akatabasamu na kumwangalia Dina. Dina akalirudisha tabasamu na kumwangalia Richard kwa ncha za macho yake.

“Itabidi uzime simu yako, hawaruhusu matumizi ya simu kwenye ndege!” Richard alisema huku tabasamu likiwa bado lipo mdomoni mwake.
Dina akaizima simu yake!

* * * * *

Upweke uliosababishwa na kutokuwepo kwa Dina ofisini ulianza kumtesa Mohsein baada ya kuwasili kazini. Tokea Dina alivyoanza kazi, hii ilikuwa ni mara ya kwanza kutokuwepo pamoja. Kutokuwepo kwake kulikuwa kama kipimo kilichompa jawabu kuwa Dina alikuwa ni sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku hapo ofisini. Aligundua Dina alikuwa akimwongezea furaha ya kuipenda kazi yake kila alipokuwa naye.

Kutokuwepo kwa Dina kulimfanya ashindwe kuifanya kazi yake ipasavyo asubuhi hiyo na kujikuta mnyonge wakati wote. Ule uelewa wa kujua Dina hatokuja kazini kutokana na kusafiri kulimpa wakati mgumu na kuiona asubuhi iwe chungu kwake. Penzi lilikuwa likimuadhibu na wivu ulikuwa ukimwandama.

Kadri muda ulivyosogea kwenda mbele hali ya kujiona ni mgonjwa iliongezeka, kila kitu humo ofisini kikawa kinamkumbusha uwepo wa Dina. Tafakuri za mazoea ya kumwona Dina akifanya hiki au kile humo ofisini zilimwelemea. Alikikumbuka kicheko cha Dina chenye maringo, na uangaliaji wake wa kupenda kumtazama mtu kwa kutumia ncha za macho yake. Hali hiyo ilimfanya awe na hisia zilizomwumiza na kuhofu kama vile, Dina asingerudi tena! Akili yake haikuwepo kabisa ofisini, ilikuwa imetekwa na fikra za kumuwaza Dina na kumfanya atumie muda mwingi wa kuduwaa kuliko kufanya kazi. Dina alikuwa amemkaa akilini mwake kama muhuri wa moto ukaavyo kwenye nyaraka!

Siku hiyo pia, ilitumika kama mzani wa kugundua jinsi alivyotokea kumpenda msichana huyo kwa kasi ya ajabu. Alijishangaa kujiona akimlilia wivu hali akijua msichana huyo yuko njiani kuolewa! Lakini, alijishangaa zaidi kujiona akimwona Richard kuwa ndiye adui yake namba moja badala ya John ambaye ndiye mume mtarajiwa wa Dina!

Mohsein alijaribu mara kadhaa kujipa ujasiri wa kuachana na fikra za kumuwaza Dina na kumwonea wivu Richard, hasa akizingatia hata yeye ana rafiki yake wa kike wa muda mrefu wanaoheshimiana na kupendana na pengine wakaja kufunga ndoa! Alikiri huyo ndiye aliyestahili kupewa upendo wote badala ya kubabaishwa na Dina aliyejipenyeza ghafla kati kati ya penzi lao. Ushawishi wa kujipa ujasiri huo wa kumwondoa Dina mawazoni mwake aliuona ukikubalika akilini, lakini ukikataa moyoni.

Akiwa mwenye kujihurumia, Mohsein alijionya kuwa, upendaji aliojiachia nao wa kumpenda Dina kwa nguvu kiasi hicho unaweza ukaja kumzindua rafiki yake wa kike kugundua kuwa anamsaliti. Mawazo yake yakarudi nyuma na kukiri kuwa, siku ambayo moyo wake ulipenyezwa sumu ya kumpenda Dina na kumuingiza kwenye ufala wa kupenda kibwege uliomkuta hapo alipo, ni ile siku ambayo alifanya mapenzi

na Dina wakiwa stoo. Kitendo hicho ndicho kiliingiza sumu kwenye mfumo mzima wa mzunguko wake wa damu na kuivuruga sehemu kubwa ya ubongo wake. Lakini pia, baada ya kitendo hicho ukawepo mwendelezo wa vitendo vya kuonyeshana kuwa wanapendana kila walipokuwa pamoja ofisini.

Siku ambayo Richard alirudi kutoka Morogoro ndio ikawa siku ya kuihitimisha fungate yao na furaha ya penzi lao kusambaratishwa baada ya Richard kumpa Dina taarifa ya safari!

Siku hizo ndizo ambazo zilikuwa na sumu iliyomwangamiza kiakili, sasa aliziona akizitumikia kwa kifungo cha mateso yanayomtesa huku akitawaliwa na donge la kumwonea wivu Richard kwa kuondoka na Dina. Akakiri kuwa, amezama kichwa kichwa kwenye penzi la Dina.

Nimekwisha! alijisikitikia peke yake!

* * * * *

Waliwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro na Dina alishangaa pale alipokuwa kwenye gari lililowachukua kutoka uwanjani kugundua kuwa, uwanja huo wa Kimataifa ulikuwa mbugani na ukiwa mbali kabisa na jiji la Arusha ikiwa ni tofauti na Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam ambao haukuwa mbali kutoka katikati ya jiji.

Waliwasili Arusha, gari walilopanda likawapeleka moja kwa moja kwenye hoteli kubwa ya kimataifa na ya kifahari ya Masai Shield iliyokuwepo kando kidogo kwa kilomita chache kutoka katikati ya jiji la Arusha. Wakiwa mapokezi, Richard alijiandikisha, hali kadhalika kwa Dina naye ikawa ni hivyo hivyo, na walipokuwa wakijaza maelezo yao kwenye kadi ya hoteli ya kujisajili upangaji, kuna maeneo ambayo Richard alimwelekeza Dina namna ya kujaza kwenye kadi yake.

“Tungependa kwenda kustafutahi kabla hatujakwenda vyumbani kwetu,” Richard aliyeonekana sio mara yake ya kwanza kuwepo kwenye hoteli hiyo alimwambia mtumishi wa mapokezi.

“Mnakaribishwa. Restaurant yetu bado inahudumia kifungua kinywa,” mtu wa mapokezi alisema huku akiiangalia saa yake ya mkononi.

Waliruhusiwa kwenda kwenye mgahawa wa hoteli wakiwa na mizigo yao. Huko Richard alimsaidia Dina kuagiza kifungua kinywa kwa kumchagulia baadhi ya vitafunio kutokana na uzoefu wake. Wakati walipokuwa wakistafutahi, Richard aligundua Dina alikuwa na tatizo linalowakabili wasichana wengi warembo wa kutokuwa na uzoefu wa namna ya kukamata uma. Dina alikuwa akiikumbatia badala ya kuikamata wakati akikita kuchoma kitu anachotaka kula. Richard hakusema lolote! Baada ya kumaliza kustafutahi, walikwenda kwenye vyumba vyao na Richard akamwonyesha Dina chumba chake kilipo. Kilikuwa jirani na chake.

“Kesho ndio tutakwenda kuanza kazi, vipi baadaye utapenda kuuzunguka mji wa Arusha na kuujua?” Richard aliyekuwa amemsindikiza Dina hadi mlangoni mwa chumba alichopangiwa kukaa alimwuliza Dina kabla hajaingia chumbani humo.

“Mi nakusikiliza wewe!” Dina alijibu na kumwangalia Richard kwa ncha za macho yake.

“Basi pumzika, baada ya masaa mawili nitakuja kukugongea mlango ili ukatembee kuuona mji.”

“Sawa,” Dina alijibu kwa upole.

Richard akamsaidia Dina kumfungulia mlango wa chumbani kwake kwa kutumia kadi na kumwelekeza matumizi ya kadi hiyo ambayo hutumika badala ya funguo ya kawaida.

Akiwa chumbani peke yake na kushangazwa na uzuri wa chumba alichomo huku akijiona kama yuko ndotoni akiwa haamini yale yanayomtokea, Dina alikuwa tayari amechanganyikiwa! Hadhi ya kusafiri kwa ndege kikazi, kulala kwenye hoteli ya kifahari kama hiyo, kilikuwa ni kitu ambacho hakikuwahi kumtokea kwenye fikra zake. Alikiri huduma anayopewa haikuwa hadhi yake kikazi, ilikuwa ni hadhi ya mtu mwenye elimu inayoanzia na Shahada! Hakutaka kujidanganya kuwa alikuwa na bahati ya mtende kupewa hadhi hiyo kutokana na kazi aliyokuwa nayo. Hakuwa na elimu ya kazi wala ujuzi wa kazi hiyo! Alitambua yote hayo yalikuwa yakifanywa na Richard kwa sababu moja ya wazi; Richard alikuwa akimpenda na alikuwa akiuonyesha upendo wake kwake!

Aliwazia jinsi alivyokuwa akimkataa Richard kwa kipindi kirefu, kipindi ambacho Richard alikuwa akimbembeleza kwa kila hali ili warudiane. Akafikiria jinsi alivyomkatisha tamaa baada ya kumchagua John kuwa chaguo lake na kumteua kuwa mchumba wake! Alikuwa na uhakika maamuzi hayo yalimwumiza Richard, lakini yeye hakujali wakati huo; kwa sababu aliamini ni John pekee ndiye aliye moyoni mwake na ndiye mwenye haki ya kuutumia mwili wake. Lakini bila ya kutarajia, alijikuta akimsaliti John kwa kutembea na Mohsein, tena kwa hiari yake! Ulikuwa ni kama uamuzi wa ajabu kukubali kufanya kitendo hicho cha kumsaliti John, lakini aliukiri udhaifu uliomkuta wa kuvutwa na mvuto wa Mohsein, udhaifu ambao unaweza kumkuta yeyote! Sasa amejikuta akiwa na mabwana wawili, na kuwa tayari kila mmoja ampende kwa sababu yake. John kwa ajili ya ku-make love, na Mohsein kwa ajili ya ku-make sex!

Lakini sasa hapo alipo kwenye chumba cha hoteli ya kifahari, Dina alikiri yupo kwenye mtihani mwingine aliokuwa akipewa na Richard. Mtihani aliouona ukimchanganya kichwa, ulimchanganya kwa sababu ni mtihani ulioingia takrima ya mapenzi. Alikuwa na uhakika matendo aliyofanyiwa hadi sasa na Richard kama angeyaeleza kwa rafiki yake yeyote wa kike, rafiki yake huyo asingesita kumshauri kumkubali Richard! Na angemshawishi kuwa, takrima anayofanyiwa na Richard ni yenye upendo wa dhati kwa sababu Richard alishamuahidi kutaka kumuoa!

Aliyafikiria matendo yote aliyotendewa na Richard na kuamini hata ule mshahara aliopangiwa ulitokana na juhudi za Richard kumshawishi baba yake, na kwa mara ya kwanza alijikuta akiamini, hata kazi aliyoajiriwa ilitokana na Richard! Akaifikiria safari iliyofanyika asubuhi hiyo kutoka Dar es Salaam hadi hapo Arusha, matendo yaliyotokea kati yake na Richard katika safari nzima hakutaka kujidanganya nayo, alikiri yalikuwa ni matendo yaliyowezesha kuwaweka tena karibu na kujikuta wakiurudisha uhusiano wao kwa njia moja au nyingine. Alitakiwa airudishe fadhila hiyo ili kuonyesha uungwana wake!
Mtihani ulikuwa kwake!

****

SIMU yake ndio iliyomshitua, alijishangaa kujikuta kumbe alikuwa amepitiwa na usingizi akiwa amelala na suruali yake ya jeans iliyomshika vema mapajani. Awali kabla ya kupitiwa na usingizi alizungumza kwa simu na wazazi wake wote wawili, akawajulisha kuwa alikwishafika salama mjini Arusha. Pamoja na kuwakumbuka John na Mohsein lakini hakuwapigia simu kuwajulisha kuhusu kuwasili kwake jijini Arusha. Akiwa ameshituliwa na simu ambayo ilikuwa ikiendelea kuita akaiweka dhana ya kuwa huenda simu hiyo ilikuwa inapigwa na mmoja wapo kati ya John au Mohsein. Akaichomoa simu yake iliyojibana kutoka kwenye mfuko wa mbele wa jeans alikokuwa ameiweka. Akashangaa kuziona namba za mpigaji badala ya jina la mmoja wao kati ya John au Mohsein. Akashindwa kuijua simu hiyo ilikuwa ikipigwa na nani.

“Haloh,” alisema kivivu.

“Mimi Richard, nifungulie!” sauti kutoka kwenye simu ilisema. Akashituka baada ya kutambua ni Richard ndiye aliyekuwa akiipiga
simu hiyo, akakumbuka namba ya Richard alikwishaifuta muda mrefu kwenye simu yake, lakini pia akakumbuka siku chache zilizopita Richard aliiomba namba yake wakiwa ofisini na alimpa. Akakurupuka kutoka kitandani, akajifuta uso haraka haraka na kwenda kuufungua mlango. Akamkuta Richard amesimama mlangoni.

“Karibu,” Dina alisema.

“Siingii,” Richard alisema kwa upole.
“Nakusubiri Mapokezi, gari limeshafika.”

Dina akaikumbuka safari ya kwenda kuzunguka kuliangalia jiji la Arusha.

“Nakuja!” Dina alisema.

Walitumia muda mwingi kuzunguka mjini, Richard alimwonyesha Dina baadhi ya maeneo yenye umaarufu hapo Arusha, waliingia kwenye maduka tofauti na Richard akaitumia nafasi hiyo kumnunulia Dina zawadi mbalimbali, kisha alimuagiza dereva wa gari walilokuwemo ambalo ni mali ya kampuni yao kuwapitisha kwenye kituo cha mafuta kinachomilikiwa na kampuni ya baba yake. Walipofika hawakuteremka, Dina akaonyeshwa kituo hicho cha mafuta kuwa ni hapo ndipo ambapo kesho watakuja kufanya kazi. Dina akakiangalia kituo hicho ambacho kilikuwa kikubwa chenye Super Market pamoja na mgahawa wa Kimataifa.

Waliporudi hotelini, walikuwa wamechoka na njaa zilikuwa zikiwauma.

Richard alimsaidia Dina kubeba baadhi ya mizigo aliyomnunulia hadi chumbani kwa Dina.

“Richard,” Dina alisema wakiwa chumbani kwake baada ya kuiweka mizigo waliyoiingiza. “Mungu akubariki!”

“Amen,” Richard alijibu na kuunganisha alilokuwa anataka kulisema. “Unaonaje ukiagiza chakula kiletwe humu chumbani? Kuna kitu nataka kukuonyesha.”

Dina akamwangalia Richard kwa ncha za macho yake.
“Kuna kitu unataka kunionyesha?” aliuliza huku akionyesha kushangaa.

“Ndiyo. Nitakuonyesha wakati chakula kitakapoletwa,” Richard alisema na kuifuata kadi yenye orodha ya vyakula kwa ajili ya huduma maalumu ya chumbani huku akimuacha Dina akiwa bado yupo kwenye mshangao. Alirudi alipomuacha Dina, akamkabidhi kadi hiyo.
“Chagua, chakula gani utapenda uletewe?” alisema.

“Samaki,” Dina alisema alipokuwa akiitazama kadi hiyo.
“Naona kuna aina tofauti ya mapishi, unaweza ukanichagulia?”

“Nakuchagulia Poached fish, naamini utafurahia.”
“Wewe huagizi?”
“Kama utaniruhusu nile chumbani kwako, nitaagiza.”

Dina akamwangalia Richard. “Agiza!” alisema kwa sauti ya chini yenye maringo.

Richard akaagiza kwa kutumia simu ya humo humo chumbani, naye pia aliagizia samaki kama aliomchagulia Dina. “Itachukua sio chini ya dakika ishirini hadi kutuletea, wacha niende chumbani kwangu kuna kazi kidogo nakwenda kuifanya, nitarudi kabla ya chakula hakijaletwa,” Richard alimwambia Dina. Wakaagana.

Ni kweli aliwahi kurudi kabla ya chakula kuletwa! Dakika tano baada ya kufika, chakula nacho kikaletwa. Richard akasaini kwenye stakabadhi ya malipo, kisha alitumbukiza mkono mfukoni na kutoa noti aliyompa mhudumu aliyeleta chakula ikiwa sehemu ya bakshishi. Mhudumu akashukuru na kutoka.

“Nionyeshe ulichotaka kunionyesha!” Dina alisema kabla ya kuanza kula.

“Kula kwanza…” Richard alisema huku akitabasamu.

Dina akagoma kula. “Sili mpaka unionyeshe hicho kitu!” alisema. Ikawa kama sehemu ya utani kwao ambao haukuwa rasmi. “Nitakuonyesha,” Richard alisema huku akiinuka kivivu kwa kujishika magoti wakati akisimama, akaenda kumsimamia Dina mgongoni.
“Nataka kukufundisha namna ya kukamata uma,” alisema huku akimuinamia Dina juu ya mabega yake.

“Khaa!” Dina alishituka.
“Yaani mimi sijui kushika uma?”
“Hujui kuushika wakati unapokula!”

“Haya makubwa!”

Richard akauchukua uma uliovingirishwa na kisu kwenye karatasi ya kujifuta mdomo iliyokuwa pembeni mwa sahani ya chakula, akaukamata kama alivyokuwa ameukamata Dina asubuhi walipokuwa wakistafutahi.
“Wewe unashika uma hivi,” akamwonyesha Dina.

“Uma haukamatwi hivi, unakamatwa hivi. Hebu jaribu,” akaurudisha kwa Dina.
Dina akasikitika kisha akafanya alivyoambiwa.

“Na kisu kikamate kama ulivyoukamata uma. Ukite uma juu ya samaki, kisha kata kwa kisu.”

Dina akafanya vile alivyoambiwa.

“Sasa endelea kula. Huo ndio ukamataji wa uma na kisu. Tatizo hili sio lako peke yako, nimeshuhudia vijana wengi, pamoja na kuupenda Uzungu, lakini wengi wanashindwa namna ya kukamata uma unavyotakiwa wakati wa kula.”

Walipokuwa wakiendelea kula, ghafla Richard alichukua kipande cha samaki alichokikata na kukiinua kwa uma.

“Nataka kukulisha,” Richard alisema huku akimwangalia Dina usoni. Dina akawa kama aliyeshangaa, akamwangalia Richard usoni bila ya kutoa jibu la haraka. Wakaangaliana kwa makini kama waliokuwa wakisomana akili zao. Hatimaye Dina akaufungua mdomo bila ya kutamka
lolote, akamruhusu Richard amlishe!

* * * * *

***DINA mtegoni AMEFUNDISHWA KUTUMIA UMA na sasa anataka kulishwa…..je atanasa????
**Nini hatma ya wivu wa JOHN SAILAS na MOHSEIN

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Walpokuwa wakiendelea kula, ghafla Richard alichukua kipande cha samaki alichokikata na kukiinua kwa uma.

“Nataka kukulisha,” Richard alisema huku akimwangalia Dina usoni. Dina akawa kama aliyeshangaa, akamwangalia Richard usoni bila ya kutoa jibu la haraka. Wakaangaliana kwa makini kama waliokuwa wakisomana akili zao. Hatimaye Dina akaufungua mdomo bila ya kutamka
lolote, akamruhusu Richard amlishe!

* * * * *

Jioni ya saa kumi na moja, Dina akiwa ameamka sekunde chache zilizopita na kabla hajakiweka vyema kichwa chake kutafakari, akausikia mlango wa chumbani kwake ukigongwa. Moja kwa moja akahisi ni Richard ndiye angekuwa anaugonga mlango huo. Akakumbuka wakati alipoachana naye mara tu baada ya kumaliza kula chakula cha mchana walichokula pamoja, Richard alimuaga na kumtaka apumzike, akisema wataonana baadaye. Ndipo naye alipoamua kulala na kupata usingizi mzuri hadi alipoamka na kusikia mlango ukigongwa.

Alipoufungua, akashangaa kumwona mhudumu wa vyakula akiwa amesimama na tray iliyobeba birika mbili, zote zilikuwa ndogo zenye ukubwa uliotofautiana, na kijaluba cha sukari, pembeni kukiwa na sahani iliyofunikwa na kitambaa.

“Sijaagiza!” Dina alisema, usoni akiwa na mshangao.
“Mzee Richard ameniagiza nikuletee,” mhudumu alisema.

Mzee Richard! Dina alishangaa na kutaka kujiuliza mtu huyo ni nani. Ghafla akapata jibu kuwa ni heshima aliyokuwa akipewa Richard. Akatabasamu na moyoni kukasuuzika baada ya kukiri, Richard alikuwa akimjali.
“Karibu,” alimwambia mhudumu na kumpa nafasi ya kuingia.

Mhudumu aliingia chumbani na kuangaliwa na Dina aliyekuwa amesimama mlangoni kwa ajili ya kumsubiri atoke.

“Nakwenda,” mhudumu aliaga baada ya kuviweka kwenye meza vitu alivyoingia nao.

“Yeye yuko wapi?” Dina aliuliza wakati mhudumu akiwa mlangoni anatoka.

“Yupo duka la kahawa akinywa chai,” mhudumu alijibu.

“Ahsante na karibu tena,” Dina alisema kisha akaufunga mlango nyuma ya mgongo wa mhudumu aliyetoka.

Dina aliiendea tray iliyoletwa na mhudumu na kuvipekua vitu vilivyoletwa. Birika kubwa ilikuwa na chai, birika ndogo ilikuwa na maziwa na alipokifunua kitambaa kilichofunika sahani, akaiona keki iliyomtamanisha, akatengeneza tabasamu dogo. Huduma ya V.I.P! aliwaza.

Akiwa anakaribia kumaliza kunywa chai aliyoletewa, simu ya chumbani kwake iliita. Alishituka na kuiangalia. Ilikuwa ni mara ya kwanza kuisikia ikiita tokea alivyoingia asubuhi. Hakuwa na uhakika kama alikuwa akipigiwa yeye au simu hiyo iliingia kwa makosa. Aliamini kama angekuwa ni Richard ndiye anayempigia basi angempigia kwa simu yake ya mkononi kama alivyofanya asubuhi.

Akaifuata simu hiyo na kusimama kando yake, badala ya kuiinua, akasita. Akaiangalia kama vile kilikuwa kitu cha ajabu kilichojenga uhai na kutoa mlio. Kisha kama vile anategua bomu, aliinua simu hiyo kwa uangalifu na polepole, akaiweka sikioni.
“Haloh,” alisema kivivu baada ya kuipokea huku akiamini sio yeye anayepigiwa.

“Umekwisha kunywa chai?” sauti ya kiume kutoka upande wa pili wa simu ilisema.

Dina akatabasamu kwenye simu baada ya kuigundua sauti ya Richard.
“Nimeshakunywa,” alisema.
“Nasikia uko duka la kahawa ukinywa chai?”

“Ni kweli. Utakuja?”
“Labda nikishaoga.”

“Basi nakuomba ufanye kitu kimoja,” Richard alisema kwa utulivu. “Ukishaoga uvae lile gauni jeusi katika zile nguo tulizozinunua leo.”

“Umelipenda?”

“Ni kati ya nguo zilizokupendeza mno wakati ulipokuwa ukizijaribu dukani, pia ni nguo ya jioni inayostahili kuingia nayo restaurant kwa chakula cha usiku.”

“Sawa mkubwa,” Dina alisema kiutani.
“Utanifuata nikishamaliza kuoga?”

“Utakapokuwa tayari njoo duka la kahawa.”

Akiwa bado hajamaliza kuzungumza na Richard kwenye simu, simu yake ya mkononi ikaita. Akaiangalia pale kitandani ilipokuwepo, lakini hakwenda kuipokea, alisubiri hadi alipomaliza kuzungumza na Richard

ndipo alipoifuata. Ilikuwa imekwishaita zaidi ya mara mbili, na alipokuwa anaichukua ikaita tena. Alikuwa John!

“Mbona umechelewa kuipokea simu?” John alianza na lawama. “Bado nipo kazini!” Dina alidanganya.
“Vipi mzima?”

“Mimi mzima, nilitaka kukufahamisha kuwa nimekwisharudi Dar, vipi huko Arusha?”

“Ni kipindi cha baridi na ni kali.”
“Umefikia hoteli ipi?”

“Masai Shield.”

“Masai Shield?” John aliuliza kwa sauti iliyojaa mshangao kuonyesha alikuwa haamini Dina kufikia kwenye hoteli kubwa na ya kifahari kama hiyo.
“Aisey, hiyo hoteli ni ya kifahari sana! Richard uko naye?”

Wivu! Dina aliwaza.
“Tumemuacha huko huko Dar. Nasikia anaweza akaja baada ya siku mbili au tatu,” Dina alidanganya tena.
“John, nitakupigia baadaye nikipata mwanya, sasa hivi bado tuko bize sana.”
“Poa, Dina. Baadaye.”

“Baadaye John.”

“I miss you!”
“I miss you too!”
Zikawa ni simu zilizofuatana! Mara baada ya kumaliza kuongea na John, simu yake ikaita tena. Safari hii alikuwa Mohsein!

“Dina, vipi mambo?” Mohsein alisema kwenye simu.
“Poa. Vipi, za huko Dar?”

“Huku poa. Wangu hata kunipigia simu kunifahamisha kama umefika salama?”

“Tumefika na kuingia kazini moja kwa moja na jamaa bado nipo naye karibu.”

“Mmefikia hoteli gani?”

Dina akahisi na huyo naye atapigwa na mshangao kama aliopigwa nao John. “Masai Shield!” alisema.

“Eti wapi Dina?” Mohsein alipayuka kwenye simu kwa sauti iliyojaa mshangao.

“Masai Shield!”

“Unaona Dina? Huyo jamaa yupo kwenye kukupumbaza…” “Nitakupigia baadaye!” Dina alisema kwa

mkato na kukata simu. Dina akakunja uso kwa hasira. Alitamani aizime simu yake ili asiwe na mawasiliano na watu hao wawili ambao wote alijua hoja zao zilianza kujikita kumjadili Richard, na yeye kwa wakati huo hakuwa tayari kulijadili hilo. Alihitaji amani, na kwa mara ya kwanza akakiri kuwa, Richard ndiye aliyekuwa akimpa amani aliyokuwa akiihitaji tokea alivyowasili hapo Arusha. Akatamani awe karibu naye kwa wakati huo, kuliko kuwa na mazungumzo na watu hao wawili yanayomjadili Richard!

Dina alikwenda kuoga huku akihisi watu hao wawili wakiwa kama mzigo kwake. Alipomaliza kuoga, aliiva nguo aliyoambiwa na Richard aivae.

Alipendezwa na nguo hiyo! Akaenda duka la kahawa kumfuata Richard. Alipokuwa akitoka kwenye lifti kuingia duka la kahawa, kila aliyekuwepo eneo hilo kuanzia wafanyakazi na wateja ambao wengi wao walikuwa ni Wazungu walimwangalia. Alionekana kama mlimbwende aliyekuwa akitembea juu ya jukwaa la mashindano ya urembo. Akamwona Richard, akatengeneza tabasamu dogo lililopokewa na Richard aliyekuwa amekaa peke yake mezani.

“Umependeza!” Richard alisema wakati akiwa amesimama na kumvutia kiti Dina.

“Ahsante,” Dina alisema wakati akikaa. “Utaongeza chai?”

“Hapana.” Mhudumu akafika.

“Hapana, sihitaji chochote,” Dina aliyekuwa akitabasamu alimwambia mhudumu kabla ya kuulizwa.

“Ningependa tuzunguke zunguke nje ya hoteli uiangalia mandhari iliyoizunguka hoteli, lakini baridi iliopo huko nje ni balaa!” Richard alisema baada ya mhudumu kuondoka.

“Mchana kulikuwa na baridi vile, sasa hivi kutakuwaje huko nje! Lakini hii hoteli ni nzuri nje hadi ndani Richard, utadhani upo kwenye pepo! Na yale mandhari ya nje yanatamanisha uzunguke zunguke kama ulivyosema.”

“Mwezi wa Novemba tutarudi tena, hali ya hewa itakuwa imebadilika na tutaweza kutembea tembea kwa miguu. Au unasemaje?”

Kikazi au kibinafsi? Dina alijiuliza. Mazingira halisi ya siku moja hiyo yalikwisha kuonyesha kuwa, wameurudisha uhusiano wao, kwa hiyo ujio mwingine wa kuja tena Arusha hakuujua ungekuwaje. “Sawa,” alijibu kwa sauti ya chini huku akiiangalia meza. Alikiri kwa hatua ambayo wameifikisha kwa siku hiyo, kamwe asingeweza kukataa chochote atakachoambiwa na Richard!

“Unaonaje tukienda baa kupata kinywaji cha kuvuta muda ili baadaye tukale chakula cha usiku?” Richard alisema.

“Sawa,” Dina alikubali.

Wakaenda! Wakati wakisubiri mhudumu aje awaulize na kuwahudumia vinywaji watakavyoagiza, Richard akakumbuka kinywaji alichomwona nacho John wakati akimpelekea Dina alipowakuta kwenye hoteli ya

BBH eneo la bwawa la kuogelea. Richard akajiuliza kama Dina angekiagizia tena kinywaji kile alichopewa na John?

Crème de Menthe! alikikumbuka kinywaji hicho.

* * * * *

Usiku walikula chakula ghali na Richard aliagiza kinywaji cha Champagne. Mhudumu alipowahudumia kwa mara ya kwanza kuwatilia kinywaji hicho kwenye glasi zao na kisha kuondoka, Richard akawa wa kwanza kuinua glasi yake juu na kumwambia Dina, “Tunywe kwa furaha ya kuurudisha uhusiano wetu. Cheers!”

Kauli hiyo ya Richard ikawa imemwingiza Dina ili akiri kwa kauli yake mwenyewe kuwa, hatua ya kukubali kuigonganisha glasi yake na ya Richard na kutamka neno ‘cheers’ atakuwa tayari amekubali kuurudisha uhusiano huo!

Kwanza Dina alionekana kusita na kujikuta akimfikiria John, kisha akamfikiria Mohsein! Tuhuma ya kuongeza mwanamume wa tatu ilimtuhumu, akauona ni uhuni usiokubalika kwake. Akakiri moyoni lazima amteme mmoja wao. Mohsein akawa kafara, akalengwa kuachwa yeye!

“Cheers!” alisema na kuigonganisha glasi yake na ya Richard, akanywa funda moja kabla ya kuirudisha glasi mezani.

Richard naye akafanya hivyo hivyo.

Baada ya kumaliza kula, hawakuondoka mapema mezani. Waliendelea kuagiza Champagne na kuzungumza, walionekana kutulia na mazungumzo yao yalitawaliwa na sauti za chini huku wakiwa wanaangaliana ana kwa ana. Mwanga hafifu wa mshumaa uliokuwa ukiwaka kwenye meza yao, ulionyesha sura zao zikiwa kwenye masikilizano na kuzingirwa na mandhari ya mahaba kwa kila mmoja wao.

Usiku huo, Dina hakulala chumbani kwake, alikwenda kulala chumbani kwa Richard!

* * * * *

Dina alihamia rasmi chumbani kwa Richard ilipofika siku ya pili baada ya kukubaliana chumba alichokuwa akilala kirudishwe. Wakaanza kuishi kama bibi na bwana. Walilala, waliamka na kwenda kazini pamoja huku uchipuaji wa penzi jipya ukishamiri kwa kasi. Kila jioni baada ya kumaliza kazi, walichagua pa kwenda kama hawakuhitaji kurudi mapema hotelini. Ikawa kama vile huko Arusha walikokwenda, walikwenda zaidi kama fungate kuliko kikazi.

***

MOHSEIN alibaki na kinyongo tokea siku aliyokatiwa simu na Dina! Kitendo hicho alikichukulia ni dharau aliyofanyiwa! Hakuamini kama kulikuwa na dharura iliyomfanya Dina aikate simu hiyo ghafla, tena bila hata kuomba samahani au kutoa neno lolote la kumtafadhalisha kabla ya kuikata simu hiyo. Moja kwa moja Mohsein akakichukulia kitendo hicho alichofanyiwa na Dina kilikuwa ni kiburi kilichoonyesha kumthamini Richard na kumdharau yeye!

Tukio hilo likawa limemdhihirishia kuwa, tayari Dina ameanza kuwa karibu na Richard! Ni mazingira ambayo alikuwa ameyatabiri awali kuwa, uendaji wa pamoja wa safari hiyo, lengo lake lilikuwa ni hilo, lakini Mohsein hakutarajia kama lingefanyika kwa haraka hivyo. Hofu iliyoingia wivu ikaanza kumtafuna, wasiwasi wa kuwa huenda Richard na Dina wamekwishafanya mapenzi ikampandisha jazba. Dhana hiyo ikamgubika kwenye wingu kubwa la wivu. Donge likamkaa kooni, akatambua kuwa, Dina ndio basi tena kwake! Kitendo cha kuhisi Richard amekwishaingiliana kimwili na Dina huko Arusha waliko kilikoleza moto wa wivu uliokuwa ukiuteketeza moyo wake. Akatamani kupiga kelele, akajizuia. Akaanza kumlaumu Dina moyoni kwa kujirahisisha kwake kwa Richard!

Kwa mara ya kwanza aliilaumu nafsi yake kwa kukubali kujiingiza kwenye penzi la kumpenda Dina, alikiri alikuwa akimpenda na alikuwa akimhitaji awe karibu naye wakati wote. Lakini pia, akamwona Dina kuwa ndiye aliyemwingiza kwenye penzi na baada ya muda mfupi ameamua kumwumiza moyo! Aliiona ilikuwa ni aina ya dhihaka aliyofanyiwa. Mohsein akaapa na yeye lazima amwumize Dina kama vile alivyoumizwa yeye!

Akaanza kufikiria njia za kulipiza kisasi za kumkomoa Dina. Akamkumbuka John!

Alikuwa hajawahi kumwona, lakini alikuwa na habari zake zote! Ni Dina ndiye aliyemwambia wakati alivyomjulisha kuwa ana mchumba! Dina alizungumzia mengi yanayomhusu John na kumjulisha hadi anakofanyia kazi. Akapanga amfuate John kazini kwake! Akaenda! Akamwulizia kwa mlinzi, mlinzi akamwambia yupo, Mohsein akaomba aitiwe.

John alipotoka akashangaa kumwona mtu asiyemjua!

“Naitwa Mohsein, najua hunijui, lakini mimi nakujua,” Mohsein alisema huku akiangaliwa na John kwa makini. “Nadhani wewe ni mume mtarajiwa wa Dina? Au sivyo?”

Kwanza John alisita kujibu, akaonyesha wasiwasi wa kutojua kule anakopelekwa kimazungumzo. “Ni nani aliyekueleza kama mimi ni mume mtarajiwa wa Dina?” aliuliza.

“Dina!” Mohsein alijibu kiuhakika.

John akaganda na kuonekana kushitushwa na jibu alilopewa. “Ilikuwaje akakwambia wewe?”

“Tunafanya kazi pamoja. Alishanipa kadi ya mchango ya Send off ili nimchangie. Katika maongezi yetu ya kawaida alinitajia unapofanya kazi na ndio sababu nipo hapa kwa ajili yako. Swali langu liko palepale, wewe ndiye mume wake mtarajiwa?”

“Ndiyo ni mimi,” John alijibu akionekana bado yuko kwenye wasiwasi.

“Sasa sikiliza, mimi ni mwanamume mwenzio!” Mohsein alizungumza kwa sauti ya kishari iliyokaza. “Hawa wanawake unatakiwa uwajue kabla ya kuamua kuwaoa. Uzijue tabia zao na ujue uadilifu wao. Je, una kifua cha kuzijua habari zake?”

John alianza kuonekana kuchanganyikiwa baada ya kuambiwa hayo. “Nipo tayari,” alisema akijaribu kuifanya sauti yake imjengee taswira kuwa ni kweli alikuwa tayari. Hata hivyo uso wake ulijenga hofu ya kile alichokuwa akisubiri kuambiwa.

“Tatizo sio kuwa tayari,” Mohsein alisema kama vile Mwalimu anayemwelekeza kitu mwanafunzi wake. “Kifua chako kipo tayari kuhifadhi siri ninayotaka kukwambia? Sio tena uende ukapayuke kwake, Ooh, Mohsein ndiye aliyeniambia!”

“Niamini, sitomwambia!” John alijaribu kusema kwa utulivu. Mohsein akawa na uhakika kwa wakati huo mapigo ya moyo ya John yalikuwa yakipiga kwa nguvu kifuani pake, na hapo ndipo alipokuwa akipataka! “Nadhani unajua kama Dina yuko Arusha?” alisema.

“Ndio nafahamu,” John alijibu huku sura yake ikionekana kama aliyepigwa na msukule.

“Najua amekuaga kuwa anakwenda kikazi, lakini kwa taarifa yako hakwenda kikazi, bali amekwenda kustarehe na mtoto wa tajiri mwenye kampuni, anaitwa Richard!”

Kutajiwa jina la Richard, John akahisi aina ya kizunguzungu kikiwa kimemwandama. Mapigo ya moyo wake yakaanza kumwenda mbio, damu ikamchemka na uso wake ukawa mzito. Akajizuia ili asiyumbe au kuanguka.

“Najua amekwenda Arusha, lakini kikazi!” hatimaye John alipata nguvu ya kusema. “Unataka kuniambia hakwenda kikazi?”

“Kiofisi imetafsiriwa kikazi, lakini ni zaidi ya hivyo!”

John alijishika kiuno akauinamisha chini uso wake na kuviangalia viatu vyake, akaonekana kufikiri haraka haraka. “Namfahamu Richard, lakini sikujua kama wana mahusiano ya aina hiyo,” alisema. “Kwa hiyo waliondoka pamoja?”

“Walipanda ndege moja kwenda Arusha!”

Ilikuwa ni habari mpya kwake! Dina alikuwa hakumwambia kama angesafiri kwa ndege. “Safari hiyo Dina alikuwa akiijua kabla?” aliuliza.

“Mbona aliambiwa mapema tu, siku tano kabla!” “Na alijua kama angesafiri na Richard?”

“Richard ndiye aliyemuita kumfahamisha safari hiyo na kumuahidi kuwa wangeondoka pamoja kwa ndege. Haikuwa safari ya ghafla!”

Dina alinidanganya! John aliwaza baada ya kukumbuka kuambiwa na Dina kwenye simu kuwa, Richard alibaki Dar es Salaam. “Naomba kukuuliza swali moja la msingi…” alisema na kumwangalia Mohsein machoni.

“Niulize,” Mohsein alisema kwa kujiamini.

“Kwa nini umekuja kuniambia habari hizi?” John aliuliza na sura yake ikawa makini kumwangalia Mohsein usoni.

Swali hilo lilionekana dhahiri kumyumbisha Mohsein na akaonekana kukosa jibu sahihi. “Ina maana nimekosea kuja kukwambia?” alijikuta akiuliza badala ya kujibu.

“Sina maana hiyo! Nataka kukuuliza swali jingine…” Mohsein hakujibu!.

“Ulikuwa ukinijua?”

“Tatizo nilikuwa sijakuona, lakini nilikuwa nikijua kuna mtu kama wewe ambaye anataka kumuoa Dina! Kwani vipi?”

John alishusha pumzi kwa nguvu kama aliyechoka, kisha akasema, “Basi nimekusikia na nitazifanyia kazi habari ulizonipa.”

“Wewe ni mwanamume mwenzangu na mimi hili jambo limeniumiza. Kwa nini akufanyie upuuzi wa namna hii? Dina atakuwa na maana gani ya kukubali kuolewa na wewe halafu papohapo atembee na mwanamume mwingine? Wewe chunguza hizi habari na mwenyewe utajionea. Lakini utakuja kunipa mkono kama nilichokwambia ni kweli!”

“Sawa nimekusikia,” John alisema na kuonyesha hakuwa tayari tena kuendelea kuwepo hapo. “Nashukuru kwa taarifa yako!” akamuaga Mohsein na kabla ya Mohsein hajajibu, John akaondoka.

Mohsein akabaki ameduwaa huku akimwangalia John alivyokuwa akiondoka.

John alirudi kufanya kazi akiwa na mtafaruku wa mawazo, muda mwingi alijikuta akizubaa kuzifikiria tuhuma alizotuhumiwa nazo Dina. Moyo wake ulikuwa ukifukuta na mapigo ya moyo wake yalikuwa yakienda kasi. Wivu ulikuwa umetawala kila sehemu ya kiungo chake na hatimaye kujigundua kuwa, hata mikono yake ilikuwa ikitetemeka! Kila wakati alikuwa akisonya peke yake na kuna kipindi alitamani aipige ngumi meza yake ya ofisini!

Ingawa hakuwa na uhakika na sababu hasa zilizomfanya mtu aliyejitambulisha kwake kwa jina la Mohsein kumletea habari hizo, lakini alikuwa mwepesi wa kuziamini kutokana na ukweli kuwa, hata yeye mwenyewe kwa siku za hivi karibuni alijengwa na mashaka makubwa yaliyomtishia kuwa, huenda Dina na Richard wakaurejesha uhusiano wa mapenzi kati yao baada ya Dina kuajiriwa kwenye kampuni ya baba yake Richard ambako Richard anafanya kazi. Lakini, laiti asingekuwa na hofu hiyo tokea awali, kitendo cha Mohsein kumjia na kumpa habari hizo kingemuweka kwenye mashaka ya kutomuamini. Na pengine angemuwekea dhana kuwa, huenda Mohsein alimtaka Dina kimapenzi na baada ya kukataliwa ndipo

akaamua kumfanyia fitina.

Lakini ni ile hofu aliyokuwa nayo awali dhidi ya ajira aliyopewa Dina kwenye kampuni ya baba yake Richard ndio iliyomfanya avutike na madai yaliyotolewa na Mohsein, ujio huo wa Mohsein akauona kama vile Mungu alimwelekeza aje amthibitishie mashaka aliyokuwa nayo dhidi ya ajira hiyo kuwa, yalikuwa ni ya kweli! Pamoja na kuziamini habari alizoambiwa na Mohsein, lakini mara kwa mara John alijikuta akiwa kama haamini kama ni kweli Dina angeweza kumfanyia usaliti wa aina hiyo.

Ni usaliti ambao awali walipeana viapo vya kutosalitiana. Mara kadhaa walikwisha kumjadili Richard, wakaapa kupambana naye kuhakikisha hafanikiwi kuwatenganisha huku Dina akichukua jukumu la kula kiapo kuwa, hata iweje, katu asingeweza kurudiana na Richard! Leo kusikia Dina amekiasi kiapo hicho na kukubali kumsaliti, John alijihisi akiteketea kwa maumivu aliyoshindwa kuyafananisha na mengine yoyote yaliyowahi kumtokea tangu ajitambue kuwa anaishi duniani!

* * * * *

WIVU wa MOHSEIN unampelekea kumuuza DINA kwa JOHN....Je nini kitatokea???
***RICHARD amemuweka DINA kimapenzi....je? Atamuoa???

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ingawa hakuwa na uhakika na sababu hasa zilizomfanya mtu aliyejitambulisha kwake kwa jina la Mohsein kumletea habari hizo, lakini alikuwa mwepesi wa kuziamini kutokana na ukweli kuwa, hata yeye mwenyewe kwa siku za hivi karibuni alijengwa na mashaka makubwa yaliyomtishia kuwa, huenda Dina na Richard wakaurejesha uhusiano wa mapenzi kati yao baada ya Dina kuajiriwa kwenye kampuni ya baba yake Richard ambako Richard anafanya kazi. Lakini, laiti asingekuwa na hofu hiyo tokea awali, kitendo cha Mohsein kumjia na kumpa habari hizo kingemuweka kwenye mashaka ya kutomuamini. Na pengine angemuwekea dhana kuwa, huenda Mohsein alimtaka Dina kimapenzi na baada ya kukataliwa ndipo akaamua kumfanyia fitina.

Lakini ni ile hofu aliyokuwa nayo awali dhidi ya ajira aliyopewa Dina kwenye kampuni ya baba yake Richard ndio iliyomfanya avutike na madai yaliyotolewa na Mohsein, ujio huo wa Mohsein akauona kama vile Mungu alimwelekeza aje amthibitishie mashaka aliyokuwa nayo dhidi ya ajira hiyo kuwa, yalikuwa ni ya kweli! Pamoja na kuziamini habari alizoambiwa na Mohsein, lakini mara kwa mara John alijikuta akiwa kama haamini kama ni kweli Dina angeweza kumfanyia usaliti wa aina hiyo.

Ni usaliti ambao awali walipeana viapo vya kutosalitiana. Mara kadhaa walikwisha kumjadili Richard, wakaapa kupambana naye kuhakikisha hafanikiwi kuwatenganisha huku Dina akichukua jukumu la kula kiapo kuwa, hata iweje, katu asingeweza kurudiana na Richard! Leo kusikia Dina amekiasi kiapo hicho na kukubali kumsaliti, John alijihisi akiteketea kwa maumivu aliyoshindwa kuyafananisha na mengine yoyote yaliyowahi kumtokea tangu ajitambue kuwa anaishi duniani!

* * * * *

Jioni baada ya kutoka kazini, John hakwenda moja kwa moja nyumbani kama ilivyo kawaida yake, badala yake alikwenda baa na kukaa kaunta. Aliamua kukaa kaunta kwa sababu ya kuepuka kupata ushirika wa mtu anayejuana naye. Alihitaji awe peke yake, asizungumze na mtu yeyote. Mzongo wa mawazo ulishakuwa mshirika tosha kwake! Akanywa vya kutosha na muda wote wa kunywa alikuwa amekipakata kichwa kilichojiinamia kwenye mkono wake.

Hatimaye aliamua aondoke hapo baa. Aliuhisi ulevi ukiwa tayari kichwani, lakini hakuwa na uhakika kama alilewa vya kutosha, pengine aliridhika na kiwango alichokunywa na kukubali kinatosha. Alitoka baa na kuiwasha pikipiki, akarudi nyumbani. Alifika nyumbani usiku uliozidi saa nne, alikuwa hajala chakula cha usiku na hakukihitaji kukila. Alichohitaji ilikuwa ni pombe aliyokwishainywa kwa ajili ya kukabiliana na maumivu yaliyoletwa na Dina.

Wakati alipokuwa akiufungua mlango alijihisi alikuwa akiyumba, lakini aliamini alikuwa akiyumba kistaarabu. Akaenda moja kwa moja chumbani kwake na kusimama kwenye kabati la kuvalia nguo. Akaichukua picha iliyosimamishwa ambayo ilijengewa fremu yenye nakshi ya kupendeza. Ilikuwa ni picha

aliyoipiga akiwa pamoja na Dina, waliipigia ufukoni ikizionyesha nyuso na vifua vyao. John alikuwa kifua wazi kama alivyokuwa Dina, wote walikuwa na mikufu ya dhahabu shingoni mwao, lakini Dina aliongezeka kwa kuwa na sidiria ya kuogelea huku miili yao na nywele ndefu za Dina zikionyesha kulowa maji kuonyesha walitoka kuogelea. Dina alikuwa nyuma ya John akiwa amemuegemea kwa kumuinamia huku ameizungusha mikono yake shingoni mwa John, wote walikuwa wakicheka kwa furaha. Ilikuwa picha nzuri!

Akiwa ameishika picha hiyo kwa tahadhari kama vile alikuwa akiogopa isianguke, John alirudi taratibu kinyumenyume huku akiiangalia picha hiyo hadi alipofika kitandani na kukaa. Akaendelea kuiangalia. Mawazo yake yakaanza kuhama, ikawa kama vile picha hiyo ilikuwa ikimkumbusha vipindi vyote vya raha wakati akiwa na Dina. Aliyakumbuka maeneo mbalimbali yaliyowaletea furaha walipokuwa pamoja, lakini kwa wakati huo yalikuwa yakimletea mashambulizi yaliyokuwa yakimwumiza moyoni. Kumbukumbu za furaha na vicheko vilivyotawala vikamkumbusha jinsi walivyokuwa wakizienzi enzi zao za upendo huku kila mmoja akijiona amefika kwa mwenzake.

Hali hiyo ya kuyakumbuka matukio hayo ilimfanya John azubae hapo kitandani kama taahira aliyeudhiwa. Ghafla akayahisi machozi yakimtoka. Akaiweka picha kandoni mwake, kisha akajilaza chali kitandani huku kichwa akiwa amekipakata kwenye viganja vya mikono yake na kuiangalia dari ya chumbani kwake. Machozi yakiwa yanatiririkia kupitia kwenye ncha za macho yake, John akaijenga taswira ya kumwona Dina alipokuwa akijinadi kwa kula viapo tofauti huku akimhakikishia kuwa, mwili wake ni kwa ajili ya John na sio Richard au mwanamume mwingine yeyote!

“Ni wewe ndiye uliyechaguliwa John!” John aliisikia sauti ya Dina ikisema na kufanya mwangi uliojirudia. Ilikuwa ni kauli aliyokuwa akiambiwa na Dina mara kwa mara. Lakini kwa hapo alipo, John aliiona kauli hiyo kama iliyozungumzwa miongo kadhaa iliyopita!

Hasira zikaanza kushindwa kudhibiti uwezo wa akili yake kuweza kujizuia. Akajiinua ghafla, kikafuatia kitendo cha haraka cha kuichukua ile picha na kuitupa kwa kuibamiza ukutani. Fremu ikajiachia na vipande vya vioo vilivyovunjika kuangukia chini na vingine kubingiria hadi kwenye picha ilipoangukia! Kwa sekunde kadhaa akaiangalia ile picha ambayo ilikuwa imejifunika, akalitafsiri tukio la kujifunika kwa picha hiyo ni kama dalili za kumalizika kwa penzi lao! Akajikuta akilikataa wazo hilo na kujaribu kuliondoa mawazoni mwake. Akili yake haikuamini kama tukio la aina hiyo linaweza likawatokea wao! Ndipo alipotambua kuwa, ni yeye ndiye anayetakiwa kuliokoa penzi hilo lisipotee. Ni yeye ndiye aliyetakiwa kumrudisha Dina kwenye himaya yake!

Kumbukumbu za kuwepo kijijini kwao zikamrudia, akamkumbuka mganga aliyekuwa amemwendea! Akayakumbuka maagizo ya mganga na dawa alizopewa ambazo alihakikishiwa zingemfanya Dina awe kama Kondoo wake endapo atajipaka dawa hizo usoni muda mfupi kabla hajakutana naye ana kwa ana.

Namwendea huko huko Arusha! aliapa.

****

JOHN aliamka mapema asubuhi kabla hakujapambazuka vizuri akiwa amenyongea na kukosa amani ya

moyoni. Mawazo yake yalielea kwenye bahari ya wivu kila alipoijenga taswira ya uwepo wa Dina na Richard peke yao jijini Arusha. Furaha ilikuwa mbali na yeye na kuhisi maumivu ya moyo huku akihofia huenda moyo wake umeathirika kiafya. Alikiri kuzidiwa kete na Richard, mpinzani wake wa muda mrefu ambaye leo anamshuhudia akitumia utawala wa fedha kumyang'anya Dina kwenye mikono yake.

John aliiwazia karata yake ya mwisho ambayo ingekuwa ni silaha pekee ya kupambana na Richard; karata ya ushirikina aliyopewa na mganga! Ilikuwa ndio tumaini pekee la kumrudisha Dina mikononi mwake. Aliamini ndio itakayommaliza Richard, ni karata itakayozifanya pesa na utajiri wa Richard visionekane vina umuhimu mbele ya Dina. Ni karata itakayomfanya Dina atekwe na penzi lake na kumwona yeye ndiye kila kitu kwake!

Akaanza kuijenga taswira ya jinsi atakavyomkabili Dina huko Arusha na nguvu ya dawa atakayokuwa amejipaka muda mfupi kabla ya kumkabili itakavyoweza kuifanya akili ya Dina itii kumsikiliza kila atakalomwambia. Aliipanga safari hiyo iwe na lengo moja la kufika na kumchukua Dina na kurudi naye Dar, huku akimuacha Richard akiwa haamini kile kilichotokea mbele yake!

Lakini kabla ya kuianza safari hiyo ya kwenda Arusha, John alijikuta akipanga kwenda kumwona mama yake Dina na kumshitakia kuhusu usaliti unaofanywa na Dina, lakini pia, akaamua kuifanya safari hiyo iwe ya siri, hata mama yake Dina asiijue.

Alimkuta mama Dina akiwa amekwisha kujiandaa kimavazi kwa ajili ya kwenda kazini. Alikuwa peke yake mezani akinywa chai tupu kama kichangamsha mwili kabla ya kupata kifungua kinywa kamili atakapokuwa yuko kazini. Ujio wa John asubuhi ya mapema hivyo ulimshitua mama huyo. Akamkaribisha John, John akakaa kwenye meza. Naye akaungana na mama mkwe wake kujimiminia kikombe cha chai tupu.

Nafasi hiyo ya kunywa chai pamoja, John akaitumia kuzijenga tuhuma zake dhidi ya Dina huku mama huyo akiwa makini kuzisikiliza.

"Ni nani aliyekwambia hizi habari?" mama Dina aliuliza baada ya John kumaliza tuhuma zake.

"Aliyeniambia ni mtu wa karibu sana na Dina, lakini sitokutajia jina kwa sababu nilimuahidi kuwa, sitomtaja."

"Sawa," mama Dina alisema kwa utulivu. "Siwezi kukulazimisha unitajie, lakini kwa mimi ninavyofahamu, huyo mtu amekudanganya mwanangu. Richard namchukulia kama mtoto wa hapa nyumbani kutokana na jinsi tunavyoishi na wazazi wake na yeye mwenyewe analielewa hilo. Na hata Dina naye analielewa hilo! Uwepo wa pamoja kwa Richard na Dina haukuanza juzi kwa sababu ya Dina kuanza kazi kwenye kampuni ya baba yake Richard, walijuana zamani na ukaribu wao ni wa muda mrefu na wako hivyo kama mtu na dada yake, na sivyo hivyo unavyofikiri mkwe. Aliyekwambia amekudanganya!"

John akatambua alikuwa akitwanga maji kwenye kinu! Hakumlaumu mama huyo, lakini alishindwa kumuelewa ni vipi alikuwa akiliangalia tukio la kukutana kwa Richard na Dina wakati huo anaouzungumzia, kuwa walikuwa na ukaribu wa dada na kaka kama majirani. Akaona asipoteze muda kuanza kumwelezea kwa kumthibitishia kuwa, Richard na Dina walikuwa kwenye urafiki wa mapenzi wakati huo na angeweza kuiwekea msisitizo hoja hiyo kwa kumthibitishia kuwa, ni Dina mwenyewe ndiye aliyeizungumza.

“Basi huyu mtu atakuwa hakunidanganya mimi, bali amejidanganya mwenyewe,” John alisema kwa kuhitimisha kauli ya ‘kubali yaishe!’

“Uwe mwangalifu na binaadamu mwanangu, ni watu wabaya!” “Kweli mama!” John alisema.

“Halafu mkwe, mwenzio aliniambia ulikuwa na mpango wa kuleta mahari hivi karibuni, unatarajia lini?”

John akazikumbuka pesa hizo za mahari alivyompa mganga aliyemfuata kijijini. “Ni kweli nina mpango huo mama, nitamtuma mshenga hivi karibuni,” John alisema na kuyakwepesha kumwangalia usoni mama mkwe wake kwa sababu alikuwa akidanganya.

“Mahari ni muhimu mwanangu ukitoa mapema, itatupa sisi wazazi nguvu ya kumsihi mwenzako awe mwangalifu na vitendo vinavyoweza kuashiria mashaka kama haya uliyokuja nayo asubuhi hii. Toa mahari haraka ili na sisi tuanze vikao vya harusi na hili la vikao litasaidia kuiweka akili ya mwenzako kumfanya ajione tayari ni mke wa mtu ili awe na nguvu ya kukabiliana kuepuka vishawishi vingine. Usidhani kama kila mtu anapenda nyie mfunge ndoa, wapo watakaojitokeza kuizuia ndoa yenu isifanyike kwa kutumia hila tofauti kama huyo mtu uliyemtaja. Jitahidi mwanangu ulete mahari mapema ili muwazibe midomo wabaya wenu!”
“Mama nimekusikia, naahidi nitalitekeleza hilo hivi karibuni,” John
alisema huku hatia ikiwa imemtawala. Akaaga.

Kauli ya mama yake Dina kuhusu mahari ilimuweka John kwenye angalizo la awali kuwa, kama angekuwa ameilipa mahari hiyo angekuwa na nafasi ya kumkabili moja kwa moja Richard huko Arusha anakokwenda na angeweza kumpa onyo la kutojihusisha kimapenzi na Dina! Lakini kwa kuwa bado hajailipa mahari hiyo, hakuwa na haki ya kumkabili Richard. Uamuzi wowote wa kumfanyia rabsha Richard, Richard angeweza kuuchukulia hatua ya kumpeleka polisi!

* * * * *

John alianzia kwenda kazini ambako alitoa udhuru na kupewa ruhusa ya siku tatu bila ya malipo. Huko kukamchelewesha kuwahi kwenda kituo cha mabasi. Alipofika aliyakuta mabasi yote yakiwa yamejaa kukawa hakuna nafasi ya kuongeza abiria. Akalazimika kupanda basi linaloishia mji mdogo wa Chalinze ambako aliteremka na kwenda kusimama njia panda ambako hupita mabasi yanayokwenda Tanga, Arusha, Mombasa na Nairobi. Huko akafanikiwa kupata nafasi kwenye basi litokalo Morogoro ambalo lilikuwa likienda Arusha.

Baada ya safari ndefu ya kilomita kadhaa, basi lao likalazimika kusimama kwa muda wa dakika kumi mjini Mombo kwa ajili ya chakula cha mchana. John aliteremka kutoka kwenye basi lakini hakwenda kula chakula, ilikuwa ni kawaida yake akisafiri huamua kutokula hadi ahitimishe safari yake. Akaagiza soda. Wakati akiinywa soda, simu yake iliita.
Alikuwa Dina!

Simu hiyo ikamchanganya, akasita kuipokea moja kwa moja. Alikuwa hajajiandaa kiakili kuzungumza naye. Akahisi kama vile Dina amemwona hapo mjini Mombo akiteremka kutoka kwenye basi. Akagundua alikuwa

akipoteza muda kwa kujituhumu kipumbavu. Akaipokea simu. “Hai,” alisema.

“Mh, vipi mambo?” Dina alisema kwa kuchangamka.

“Huku poa ni kama ulivyokuacha,” John alisema kwa sauti tulivu, lakini akilini hakukuwa na utulivu.
“Vipi huko?”
“Huku mzigo tu.”

“Kuna jipya lolote?”
“Ah, litoke wapi?”

John akapata akili ya kuuliza. “Huwa mnapiga kazi kuanzia asubuhi mpaka saa ngapi?”

“Huwa tunapiga hadi saa kumi na moja, baada ya hapo tunarudi hotelini.”

John akawaza, kama atawahi kufika Arusha angalau kwenye saa kumi na mbili za jioni, basi kwenye muda wa saa mbili usiku angeweza kumfuata Dina hotelini. Na huko angemchukua na kwenda naye kwenye hoteli ambayo angefikia, labda vinginevyo, Dina amwombe walale pamoja kwenye hoteli ya Masai Shield alikofikia. Lakini wazo hili la pili kidogo alijikuta akilitia wasiwasi kutokana na kutojua kama Dina na Richard wanalala chumba kimoja au kila mmoja na chake.

“Lakini sio kazi za kukuchokesha sana?” John alisema baada ya kuridhika na hesabu zake.

“Kiasi,” Dina alijibu kwa sauti ya maringo.

“Jamaa vipi, kishatia timu?” John kwa mara ya kwanza aliuliza swali lililomlenga Richard kwa aina ya utani.

“Nani Richard?”

John akagundua swali la Dina lilikuwa la kuvutia pumzi kulijibu swali hilo. Aliamini hakukuwa na sababu yoyote ya kuuliza hivyo wakati alikuwa akijua ni nani anayeuliziwa. “Ndiyo,” alijibu.

“Nasikia ameingia leo,” Dina alisema.

Hasira ikachana kwenye moyo wa John! Ananidanganya! aliwaza na kulaani kwa kumalizia na tusi. Ilibaki alimanusura ashindwe kuidhibiti akili yake, na alikwishaanza kuinua ulimi wake kutaka kusema mbovu kupitia kwenye simu, lakini ghafla busara ilimjia, akajizuia. “Kwa hiyo hamjaonana?” alisema huku akiilazimisha akili yake itulie.

“Bado sijaonana naye, labda nitakaporudi hotelini huenda nikamwona kama na yeye atakuwa amefikia huko.”

Likawa eneo jingine la John kujizuia baada ya kuongopewa tena! “Aisii,” alisema kwa unyonge na kutamani kuaga ili akate mawasiliano, lakini akashindwa kufanya hivyo kwa kuogopa Dina asije akaingiwa na hisia za mashaka za kujiona ameshitukiwa. Isitoshe, ni Dina ndiye aliyekuwa amepiga simu, kwa hiyo

atalazimika asubiri hadi Dina mwenyewe atakapoaga kwenye simu.

“Okay John, nilitaka kusikia sauti yako tu. Huenda baadaye usiku nikakupigia tena,” Dina alisema.

John akashukuru Dina alivyotamka hivyo. “Poa Dina, hata mimi nimefurahi kuisikia sauti yako,” alisema.

“Kwa hiyo baadaye.” “Poa.”

Wakakata mawasiliano. John akasikitika peke yake huku akiirudisha simu mfukoni.

* * * * *

Waliwasili mjini Arusha mwanga wa jioni ukiwa umeshapotea na John alipoiangalia saa yake ikaonyesha zilikuwa zimebaki dakika chache kufika saa kumi na mbili na nusu. Alipoteremka kwenye basi akakumbana na baridi kali, akakodi teksi haraka kabla baridi haijatawala mwilini mwake. Akapelekwa kwenye hoteli moja ndogo iliyokuwa mitaa kadhaa kutoka stendi.

Aliingia hotelini na kukaribishwa.

“Utakaa siku ngapi?” Mhudumu wa mapokezi alimwuliza John. “Usiku mmoja,” John alijibu. “Kesho asubuhi naondoka!” Akapewa chumba kilichopo ghorofa ya kwanza.

Huko chumbani, John alioga haraka haraka, yalikuwa maji ya moto na yaliweza kuurudisha uchangamfu uliokuwa umepotezwa kutokana na uchovu wa safari. Akabadili shati, akavaa fulana nzito ya baridi. Kingine alichokibadilisha ilikuwa chupi, lakini suruali aliirudia ile ile aliyokuwa amesafiri nayo ambayo ilikuwa ni jeans. Baada ya kubadili hizo nguo, John alifikiria kwenda kula, lakini akalipuuza wazo hilo baada ya kuwaza huenda atakapokutana na Dina, Dina anaweza akamkaribisha chakula cha usiku kwenye hoteli ya Masai Shield. Hakuwa na uhakika na hali ambayo angeikuta huko, lakini alikuwa na matumaini Dina asingeweza kumletea ubishi wowote wakati wa mazungumzo yao.

John alizitoa kutoka kwenye begi dawa alizopewa na mganga, akaziandaa juu ya meza. Akiwa amekaa kwenye kochi dogo la humo chumbani, alizitia pamoja dawa hizo kwenye mkebe mdogo wa plastiki na kuzichanganya, baadaye akachukua kichupa kidogo chenye mafuta na kuyachanganya mafuta hayo pamoja na zile dawa. Akaanza kuzichanganya tena na wakati huo huo akitia nia iliyokusudia kumfanya Dina pindi atakapokutana naye, akili ya Dina ipumbazike. Baada ya kuimaliza shughuli hiyo, akaingia hatua ya kujipaka dawa hizo usoni na mikononi hadi aliporidhika. Akaenda kujiangalia kwenye kioo kama kulikuwa na mwonekano wowote wa kuonekana zile dawa alizojipaka, baada ya kuridhika hakuna dalili zilizoonyesha kuwa amejipaka dawa, John akajiandaa kutoka.

Alitoka hotelini na kukodi teksi iliyokuwa imeegeshwa kwenye baa iliyokuwa jirani na hoteli aliyofikia. Hakuwa mgeni na mji wa Arusha, hivyo mara tu baada ya kuingia kwenye teksi akamwagiza dereva ampeleke kwenye hoteli ya Masai Shield.

* * * * *

Richard ndiye aliyekuwa wa mwisho kumaliza kuvaa. Alikuwa amesimama mbele ya kioo akijiangalia alipokuwa akijifunga tai huku Dina akiwa amekaa kitandani naye akimalizia kujivika hereni kwenye sikio lake. Ni muda mfupi uliopita watu hawa wawili walikuwa wametoka kufanya mapenzi na kisha kuoga na kujiandaa kwa ajili ya kwenda kula chakula cha usiku na baada ya kumaliza kula, walikubaliana waende kucheza kamari kwenye Casino iliyomo humo humo hotelini. Richard ndiye aliyemshawishi Dina ili akaijue kamari inavyochezwa. Dina alikuwa hajawahi kwenye maisha yake kuingia kwenye Casino yoyote.

Wote walionekana nadhifu na mwonekano wao ulidhihirisha walikuwa ni watu wenye kuogelea kwenye maisha ya kifahari. Dina alikuwa amevaa gauni la jioni lenye kitambaa chepesi, refu na lilifuata sambamba na mwonekano wa umbile lake kuanzia kifuani hadi chini. Kwa yeyote ambaye angemwona asingekuwa na hoja yoyote ya kupinga ughali wa gauni hilo dukani na ulimbwende uliopo kwa msichana huyo. Licha ya mwonekano aliokuwa akionekana Dina ndani ya gauni hilo, lakini Dina alizidi kurembeshwa na vito vya thamani vya dhahabu yenye kiwango bora inayomeremeta. Shingoni alikuwa na mkufu mwembamba na mrefu, wenye kito cha almasi iliyokuwa ikifanya miali inayong'aa kila kilipogeuka, masikioni mwake kulikuwa na hereni za mviringo mfano wa bangili huku vidole vyake viwili vya mkono wa kushoto vikivikwa pete, moja yenye kito cha almasi na nyingine iliyotengenezwa kwa mfano wa ua lichanualo. Kwenye maungio ya kiganja na mkono wa kushoto kulionekana bangili nne zilizolaliana huku mkono wake wa kulia ukarembeshwa na saa ndogo nyembamba ya kike yenye thamani kubwa. Vitu vyote hivyo vilivyokuwa mwilini mwake zilikuwa ni zawadi alizonunuliwa na Richard.

"Upo tayari?" Richard alimwuliza Dina na kukitingisha kidogo kitanzi cha tai kwa ajili ya kuiweka sawa.

Dina aliinuka moja kwa moja kutoka kitandani na kusema, "Twenzetu!"
Wakatoka.

Walikaribishwa na mkuu wa mgahawa ambaye alikwishaanza kumzoea Dina na akawa anamuita kwa jina la 'Mrs. Richard!' Walikaa kwenye meza ambayo ilikuwa imewekwa kibao chenye neno 'Reserved' na mara baada ya kukaa, mhudumu alikiondoa kibao hicho.

Wote waliagiza chakula kilichofanana, viazi vilivyokaangwa na kutiwa vitunguu vilivyokaangwa juu yake na kuku wa kukaanga wa kuchovywa na unga wa ngano uliochanganywa na mayai. Pamoja na kila mmoja kujaziwa maji baridi kwenye glasi ndefu mfano wa puto zilizokuwa zimejenga ukungu wa baridi, lakini pia Richard aliagiza mvinyo mweupe kwa ajili ya kusukumizia chakula chao.

Baada ya kumaliza kula, Richard na Dina hawakuwa na haraka ya kuondoka mezani, hawakutaka kuwa watu wa mwanzoni kuingia Casino. Waliamua kuagiza mvinyo mwingine na kuendelea kuzungumza kwa taratibu, yeyote ambaye angewaona asingesita kuwatabiri kuwa ni wapenzi wapendanao.

* * * * *

John aliteremka kutoka kwenye teksi iliyokuwa imesimama sawia kwenye mlango unaoingia moja kwa moja ndani ya jengo la hoteli ya Masai Shield. Teksi ikaondoka na yeye akageuka kuangalia mlangoni. Wahudumu wawili wenye sare za kazi wanaopokea wateja waingiao, walikuwa wamesimama ndani ya mlango wa kioo unaojifungua wenyewe pindi unapokaribiwa na mtu anayetaka kuingia au kutoka. Wote walimwona John alivyoteremka kwenye teksi na wakawa wanamwangalia.

Mara tu mlango ulipojifungua, John akaisikia harufu nzuri kutoka humo ndani; ni harufu ya aina moja ambayo duniani kote utakumbana nayo mara tu ukiingia kwenye hoteli za kifahari kama hizo. Alipokuwa akiingia aliwasalimia watu wale na wote waliitika kwa nidhamu na kumkaribisha.

Mteja ni Mfalme! John aliwaza baada ya wahudumu wale kumuinamishia vichwa wakati walipokuwa wakisalimiana. Ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuingia kwenye hoteli hiyo ingawa alikuwa akiiona na kuipita kwa mbali wakati wa siku za nyuma alipokuwa akija Arusha. Aliingia ukumbini kulikokuwa na mandhari ya kupendeza iliyokuwa ikimulikwa kwa taa zenye nuru hafifu ambayo miali yake ilichomoza kutoka kwenye matundu madogo na membamba yaliyopo kwenye dari iliyonakshiwa kwa ujenzi wa kisanii.

***JOHN ameamua kumuibukia DINA huko huko Arusha.....kimya kimya....NII kitatokea?

**** MAMA DINA amekumbushia suala la mahali.....pagumu hapo!!!

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI NA NNE

John aliteremka kutoka kwenye teksi iliyokuwa imesimama sawia kwenye mlango unaoingia moja kwa moja ndani ya jengo la hoteli ya Masai Shield. Teksi ikaondoka na yeye akageuka kuangalia mlangoni. Wahudumu wawili wenye sare za kazi wanaopokea wateja waingiao, walikuwa wamesimama ndani ya mlango wa kioo unaojifungua wenyewe pindi unapokaribiwa na mtu anayetaka kuingia au kutoka. Wote walimwona John alivyoteremka kwenye teksi na wakawa wanamwangalia.

Mara tu mlango ulipojifungua, John akaisikia harufu nzuri kutoka humo ndani; ni harufu ya aina moja ambayo duniani kote utakumbana nayo mara tu ukiingia kwenye hoteli za kifahari kama hizo. Alipokuwa akiingia aliwasalimia watu wale na wote waliitika kwa nidhamu na kumkaribisha.

Mteja ni Mfalme! John aliwaza baada ya wahudumu wale kumuinamishia vichwa wakati walipokuwa wakisalimiana. Ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuingia kwenye hoteli hiyo ingawa alikuwa akiiona na kuipita kwa mbali wakati wa siku za nyuma alipokuwa akija Arusha. Aliingia ukumbini kulikokuwa na mandhari ya kupendeza iliyokuwa ikimulikwa kwa taa zenye nuru hafifu ambayo miali yake ilichomoza kutoka kwenye matundu madogo na membamba yaliyopo kwenye dari iliyonakshiwa kwa ujenzi wa kisanii.

Kwenye ukumbi huo ambako kulikuwa na ukimya uliovunjwa na mziki mororo wa ala tupu uliosikika kwa sauti ndogo, eneo hilo lilikuwa na sofa za kupendeza ambazo baadhi zilikuwa zimekaliwa na wateja; wengi wao wakiwa ni Wazungu. Pia kulikuwa na matangazo ya huduma mbali mbali yaliyokuwa yakiwaka kwa kunakshiwa na taa za rangi kwenye baadhi ya kuta zilizomo humo ndani. John akaliona eneo alilokuwa akilihitaji; eneo la mapokezi ambalo lilikuwa lipo mbele yake. Kwenye meza ndefu iliyojengwa kwa muundo wa upinde kulionekana baadhi ya wateja waliokuwa wakihudumiwa na wafanyakazi watatu wa idara hiyo mapokezi. Wafanyakazi wote watatu walikuwa ni wasichana warembo wenye sare za kazi zilizofanana.

John alikwenda kusimama kwenye meza hiyo na kusubiri mmoja wa wafanyakazi hao amaliziane na baadhi ya wateja waliokuwepo hapo. Akapatikana mmoja aliyemwendea John.

“Karibu; nikusaidie nini?” msichana huyo wa mapokezi alimwambia John kwa lugha ya Kiingereza.

“Nataka kuonana na mgeni wangu, kati ya Richard Ken au Dina,” John alisema kwa kujiamini kwa kutumia lugha ya Kiingereza ambayo hakuwa na umahiri nayo sana.

Msichana akainua simu na kupiga, akaonekana kusikilizia kwa makini. Akairudisha.
“Hawapo chumbani, nadhani watakuwa restaurant wakila chakula cha jioni,” msichana alisema.

Hawapo chumbani! John alishangaa.
“Naweza kwenda kuwaona? Mimi ni mfanyakazi mwenzao,” alisema na kujaribu kuificha taharuki aliyoipata.

“Unaweza kwenda kuwaona,” msichana alisema na kuonyesha kumalizana na John, akataka kuondoka kwenda kuhudumia mteja mwingine aliyefika hapo ambaye alikuwa ni Mzungu.

“Unaweza ukanielekeza? Siijui restaurant yenu ilipo,” John aliwahi kusema kabla msichana yule hajaondoka.

Msichana akamwelekeza. “Ahsante,” John alisema.

“Unakaribishwa!” msichana alisema na kuonyesha tabasamu bandia la kikazi kisha akamfuata yule mgeni akiyekuwa amewasili.

Pamoja na kuwa alitarajia kitu kama hicho kingeweza kutokea, lakini ule ukweli uliojitokeza kutokana na kauli ya yule msichana wa mapokezi kutoa kauli iliyoonyesha kuwa, Richard na Dina hawakuwepo chumbani, ilimdhihirishia John kwamba, Richard na Dina walikuwa wakikaa kwenye chumba kimoja, ikawa kama vile jambo hilo hakuwahi kulifikiria kabla!

Udhihirisho huo uliomdhihirishia kuwa Richard na Dina walikuwa wakitumia chumba kimoja ulimchanganya. Hasira na wivu vilimjia kwa wakati mmoja na alijishangaa jinsi alivyoweza kujizuia mbele ya yule msichana kutoonyesha kuchanganyikiwa alikokupata. Mapigo ya moyo wake yalikuwa yakimwenda mbio wakati alipokuwa akielekea katika lifti itakayompeleka kwenye ghorofa ulipo mgahawa ambako ndiko alikoelekezwa waliko Richard na Dina. Mkanganyiko uliokuwa kichwani mwake ulimfanya alijihisi kutamani kumuua yeyote kati ya Dina au Richard! Akili yake ilimtuma kutoukubali uzoba aliokuwa akifanyiwa na watu hao.

Akiwa amesimama nje ya mlango kuisubiri lifti iwasili, John alirudia kama mara mbili au zaidi kushusha pumzi za hasira kama vile afanyavyo mtoto mwenye hasira aliyetoka kulia kwa ghadhabu. Alijaribu kuituliza akili yake na kujihisi kama anayeshindwa kuidhibiti. Subira yake ya kuisubiri lifti ilimfanya asitulie sehemu moja, alizunguka huku na kule na kuiona lifti hiyo ikichukua masaa kadhaa kuwasili. Lifti ikawasili, akaingia.

Lifti ilimchukua na kwenda kusimama kwenye ghorofa yenye mgahawa. John alitoka akiwa na baadhi ya wateja wengine waliokuwa wakienda kula kwenye mgahawa aliokuwa akielekea. Yeye na wale wateja kwa pamoja walikaribishwa na msimamizi wa huduma za mgahawani.

“Nataka kuonana na Richard Ken, nimeambiwa yuko huku anakula,” John alimwambia mkuu wa mgahawa aliyekuwa ameanza kumwonyesha meza ya kwenda kukaa.

* * * * *

“Yesu wangu!” Dina alisema na papohapo kuonyesha kushituka wakati uso wake akiwa ameuelekeza mlangoni ambako wateja walikuwa wakiingia.

“Kitu gani?” Richard aliuliza na kuangalia alikokuwa akiangalia Dina. Akaonekana kutokigundua kilichokuwa kimemshitua Dina. “Vipi?” aliuliza tena huku akiurudisha uso wake kumwangalia Dina.

Dina alikuwa bado akiangalia mlangoni, kisha kwa sauti ndogo kama vile alikuwa anaongea peke yake akasema kwa kifupi, “John!”

Ndipo Richard akapata mshituko ulioungana na kitendo cha kuangalia tena mlangoni. Kauli yake ikapotea baada ya kumwona mkuu wa mgahawa akimwonyesha John mahali walipo!
John akawa kama aliyezubaa huku akiangalia upande walipo Richard na Dina.

“Wacha nimfuate kule kule!” Dina alisema ghafla na kuinuka. “Mwache aje hapa hapa!” Richard alisema na kumzuia Dina kwa
kumshika mkono. Richard alishaingiwa na wasiwasi kunaweza kukatokea patashika kati ya Dina na John endapo wangebaki peke yao na ndio sababu ya kumzuia Dina. Lakini pia alikifanya kitendo hicho kwa sababu alikuwa akijiamini kupigana, aliwahi kuchukua mafunzo ya karate wakati alipokuwa akisoma Uingereza. Hata hivyo alishakuwa na zaidi ya miaka miwili tokea aliposimama kuendelea na mafunzo hayo na hakuwa na mazoezi ya aina nyingine yoyote tokea alivyorudi nchini, hata hivyo aliamini angeweza kumdhibiti John asimfanyie fujo yoyote Dina kama angewafuata hapo.
“Niache nikazungumze naye,” Dina alisisitiza kwa kujiamini. Richard akamuachia! Dina akaondoka na kuharakisha kwenda
kumkabili John kabla hajaingia eneo la ndani zaidi la mgahawa lenye wateja waliokuwa wakila chakula.

Akiwa amesimama huku akimwangalia Dina aliyekuwa akimjia, John alishindwa kuamini kama anayemwona hapo alikuwa ni Dina yule yule aliyekuwa akimlia viapo vya uaminifu. Alijiona kama aliyekuwa akimwangalia Dina mpya mwenye uzuri ulioongezeka ghafla kiasi kwamba hata baadhi ya wateja waliokuwemo humo mgahawani walikuwa wamegeuka kumwangalia.

Dina alipokuwa akielekea kule alikosimama John, hatua zake ziliufanya ule mkufu wa dhahabu wenye kito cha thamani aliouvaa shingoni, kidani chake kichezecheze na kutoa miali ya kung’ara kila kilipokuwa kikitikisika kifuani kwake, na wakati huo huo hereni za dhahabu zilizokuwa mfano wa bangili kubwa nazo zilikuwa zikiyumba masikioni mwake wakati akitembea. Mwonekano wa Dina ulimfanya John apigwe na ganzi huku akishindwa kuamini kama yeye ndiye mmiliki wa mapenzi wa msichana huyo anayekuja mbele yake. Akili yake ilikuwa imepumbazwa na uzuri wa binti huyo aliyeonekana kuwa kwenye daraja la juu la kimaisha. Hasira iliyokuwa imemvaa wakati akiwasili hapo ikaanza kunywea taratibu!

Ghafla akaiona fahari ya kummiliki msichana mzuri wa aina hiyo, tukio hilo likamfanya akumbuke kuwa ni msichana huyo ndiye anayemfanya aingie kwenye ushindani wa kumgombania kati yake na Richard! Na ndiye aliyekuwa akimhangaisha kwenda kwa waganga kwa ajili yake ili afanikiwe kumrudisha kwenye himaya yake!

Siwezi kumuachia Richard! aliapa ghafla. Akayakumbuka madawa aliyojipaka usoni kuwa yalikuwa na uwezo wa kuipumbaza akili ya Dina pindi atakapoangaliana naye machoni! Na hicho ndicho kilichomleta hapo Arusha; aje amchukue na kurudi naye Dar es Salaam!

“Vipi?” Dina aliuliza alipomkaribia John huku sura yake ikiwa kwenye mshangao na nusu kwenye kuchanganyikiwa.

Kitendo cha Dina kumwangalia sawia John kwenye macho yake wakati alipomwuliza swali hilo, ndicho John alichokuwa akikihitaji. Alihitaji Dina ayaangalie macho yake kwa kuamini madawa aliyojipaka ndipo yatakapofanya vyema kazi yake. Na yeye akayatuliza macho yake machoni mwa Dina na kupoteza sekunde kadhaa kama sehemu ya kukoleza ufanyaji kazi wa dawa hizo kabla ya kulijibu swali la alilolizwa.

“Nimekufuata turudi Dar es Salaam!” John alisema baada ya kujitosheleza na muda alioutumia

kuangaliana na Dina, na hata aliposema hivyo, alisema kwa kujiamini. Akatarajia Dina angegwaya.

Lakini badala ya kugwaya, Dina akashangaa!
“Hebu njoo huku!” alimwambia John kwa sauti ya upole lakini yenye amri. Alikuwa akijielewa jinsi anavyoweza kumdhibiti John na alikuwa na uhakika John angefuata alichosema.

John akamfuata! Wakaenda ulipo ukumbi wa baa, wakakaa kwenye sofa. Mhudumu akafika muda huo huo na kuwauliza wanachohitaji kunywa.
“Utakunywa nini?” Dina alimwuliza John.

John akazitambua fikra za Dina kuwa zipo kwenye kumwongoza kama alivyokuwa amezoea siku zote. Kwa kuwa na yeye alikuja hapo kwa imani ya kuleta mapinduzi ya kuyageuza mazoea hayo kwa kuamini dawa alizojipaka, akaona sasa ilikuwa zamu yake kuchukua utawala wa kumtawala Dina kimapenzi.

“Sihitaji kinywaji chochote Dina!” John alisema kwa sauti aliyotaka Dina aione ni amri.
“Nimekuja kukuchukua turudi zetu Dar! Kwa hiyo tuondoke!”

Dina akatengeneza tena mshangao usoni na kumwangalia John. “John umelewa?” aliuliza kwa kujiamini na kuonyesha kiburi kidogo kwenye sauti yake ili kuonyesha ni yeye ndiye mwenye turufu ya utawala wa kumtawala John.

“Ni mzima na akili yangu!” John alijibu kifedhuli huku mikono akiwa ameituliza juu ya magoti yake. Ghafla akajiona ana nguvu za kupambana na Dina kimazungumzo, akaamini dawa alizopewa na mganga zilikuwa zikimpa nguvu hizo!

Jibu la John likamfanya Dina amwangalie mhudumu aliyekuwa bado amesimama akisubiri maagizo.
“Nikikuhitaji nitakuita,” alimwambia mhudumu kwa lengo la kumwondoa.
Mhudumu akaondoka.

“Umekuja kunichukua wakati unajua nimekuja huku kikazi?” Dina alimwuliza John kwa utulivu baada ya mhudumu kuondoka.

“Nimeamua! Kwa hiyo tunaondoka pamoja hadi hotelini nilikofikia!” John alisema kwa sauti yenye ushari.
“Na kesho asubuhi tunarudi Dar es Salaam!”

Dina hakujibu haraka. Alitulia kwa sekunde chache huku akimwangalia John kwa dalili zile zile za mtu aliyemzoea huku akionekana kama anayetaka kuisoma akili ya John.
“Unajua John sikuelewi!” alisema na safari hii sauti yake ilikuwa na ukali fulani.

“Hunielewi kwa sababu lugha niliyoizungumza huijui? Au hunielewi kwa lipi?” John aliuliza.

Hata hivyo, John alikuwa ameanza kushangazwa kumwona Dina akiwa bado anaonyesha aina fulani ya ubishi. Alitarajia Dina hadi muda huo angekuwa tayari amekwishapumbazwa na dawa alizojipaka na angekuwa anatii kila analoelezwa. Alitarajia endapo Dina kama angetokea kuhoji, basi angehoji maswali madogo madogo yasiyoashiria aina yoyote ya kuleta ubishi; lakini mwonekano uliokuwepo hapo ulianza

kuwa tofauti na matarajio hayo. Dina alikuwa bado akionyesha kuwa na akili zile zile za utawala dhidi yake! John akaanza kuuhoji uwezo wa dawa alizojipaka kama zilikuwa na uwezo wa kumbadilisha Dina.

“Utakujaje ghafla bila ya kuniarifu?” Dina aliuliza kwa sauti iliyoonyesha kukerwa na kuonekana joho la utawala wa kumtawala John likiwa bado maungoni mwake.
“Halafu kufika tu unaniambia umekuja kunichukua unipeleke hotelini kwako! Hakuna kunisalimia, hakuna kuulizana! John umechanganyikiwa?”

“Nadhani nina haki ya kukwambia hivyo! Dina, mimi ni mchumba wako!” John naye alisema kwa ukali wa kujibu mapigo.

Dina akatoa kicheko kidogo cha dharau.
“Haki ya kunikokota unavyotaka? Bado hujawa na haki hiyo John!’ alisema kwa utulivu huku akitingisha kichwa chake kuonyesha kusikitika. “Hata mahari yenyewe hujanilipia unaanza kusema hivyo! Je, ukinioa itakuwaje?”

John akamkumbuka mama yake Dina na kauli hiyo ya mahari. Akanywea kiaina, lakini akajipa matumaini ya kuyatawala mazungumzo hayo. Bado alikuwa akiamini dawa zake zingefanya kazi.
“Lakini mimi bado ni mchumba wako Dina!” alisema kwa ajili ya kuendeleza ligi ya ubishi. “Kuna makosa gani kukwambia hivyo?”

“Najua kuwa ni mchumba wako, lakini ndio uamue kunifuata huku Arusha bila ya kunifahamisha kama unakuja?” Dina alisema, kisha ghafla akaonyesha kukerwa na kitendo hicho.
“Kwa nini hukuniambia kama unakuja wakati mchana wa leo tulizungumza kwenye simu? Ulikuwa na mawazo gani kichwani mwako? Huniamini? Lengo lilikuwa ni kunifumania?”

John akapigwa na butwaa! Lakini halikuwa butwaa lililoletwa na kauli hiyo kali ya Dina; bali lilitokana na kule kutomwona Dina kutokuwa na dalili za kulainika! Alijiona bado akizungumza na Dina yule yule ambaye siku zote yuko juu yake.

“Kwa hiyo hatutakwenda hotelini nilikofikia?” John aliuliza swali ambalo alikuwa na uhakika sio jibu la swali alililoulizwa.

“Nakuomba kitu kimoja John!” Dina alisema kiukomavu na kumwangalia John machoni. “Naomba urudi Dar! Kama unalo lolote la kuniambia hata kama nimekuudhi, basi unisubiri hadi nitakapokuja Dar. Samahani kwa kukwambia hivyo, lakini sikudanganyi John; kweli umeniudhi!”

John akapoteza mhimili wa kujizuia, akaonyesha kuanza kuchanganyikiwa. Alizirudisha nyuma nywele zake kwa kuzisukuma na vidole vyake vya mkono. “Dina, bado unanipenda?” aliuliza huku akiwa amekiegesha upande kichwa chake. Swali lake halikuulizwa kimahaba, lilikuwa na aina ya ushari.

“John bwana! Maswali gani hayo unayoniuliza?”

John akagundua alikuwa akipoteza muda kusubiri nguvu za dawa alizojipaka zifanye kazi. Yule mshenzi amenitapeli! aliwaza. Akaachana na mawazo hayo ya kishirikina ambayo yalikuwa yamemjengea subira

kwa wakati wote. Akairudisha akili yake kwenye uhalisia wa jambo analokabiliana nalo kuwa, Dina na Richard walikuwa wanalala chumba kimoja humo hotelini! Na isitoshe pia, amewafumania wakiwa kwenye meza moja wakila chakula wakionekana dhahiri ni wapenzi!
Wivu ukarudi upya na subira ikamtoka!

“Mimi najua kila kitu Dina! Usifikiri miye zoba!” John alibwata huku akionekana kuchachamaa ghafla. “Nina habari zenu zote kuhusu wewe na yule mshenzi wako uliyekuwa naye pale mezani!” alisema na kunyoosha mkono kuelekeza upande uliko mgahawa ambako yuko Richard.
“Kwa taarifa yako, najua kama ulisafiri naye kwenye ndege moja! Isitoshe vilevile, najua kama unalala naye chumba kimoja!” alinyamaza na kutweta huku macho yake yakitambaa mwilini mwa Dina.
“Ni nini kilichokubabaisha Dina? Au ni hiki kijiguo pamoja na hizi dhahabu alizoanza kukununulia? Hukuwanavyo hivi wakati ulipoondoka Dar! Uwongo? Kwa muda huu mfupi wa kuja hapa Arusha tayari umeamua kunisaliti? Umeisahau ahadi uliyoniahidi kuhusu huyu jamaa? Umesahau kama uliapa Miungu yote kunihakikishia kuwa hutotembea naye? Umesahau yote niliyokutendea? Umesahau tulikotoka? Unanifanyia haya ukiwa na pete yangu ya uchumba kidoleni mwako Dina?”

Dina aliganda. Akaonekana kama mlemavu asiyeweza kuzungumza. Alikuwa amenywea kama aliyenyeshewa. Akaonekana kama sanamu lenye kupepesa macho. Kiburi na kule kujiamini kukatoweka. Aligwaya!

John alikuwa tayari ameghadhibika!
“Tunaondoka pamoja kwenda hoteli nilikofikia!” alisema na kuukamata mkono wa Dina.

Dina akaufyetua mkono wake kutoka mkononi mwa John.
“Bwana tutakuja kuongea Dar!” Dina alisema na kuonekana kurejewa na fahamu. Akasimama kutaka kuondoka.

John akawahi kumzuia Dina kwa kumshika tena mkono.
“Huwezi ukazungumza na mimi halafu ukataka kuondoka kienyeji, rudi kwenye kiti!” alisema kwa sauti ndogo kujaribu kuwafanya watu wasifuatilie kinachoendelea hapo.

Dina akanywea tena, safari hii macho yake yakawa yameingia woga! Na yeye naye akazungukwa na kiwingu cha hofu kama ya mwenzake ya kuogopa watu wasilifuatilie tukio lao. Akarudi kwenye sofa.
“Mimi nazungumza na wewe halafu unaondoka!” John alisema,
munkari ulikwishaanza kumpanda. “Sasa mimi nakwambia, kwa yule mshenzi wako hurudi! Na utaondoka na mimi!”

“John mimi nipo kazini! Sasa mambo gani haya unayonifanyia? Utaniharibia kazi…” Dina alilalamika kwa sauti ya kujitetea, alikuwa hajawahi kumwona John akiwa katika hali ya hasira kama anayomwona nayo hapo na hali hiyo ilianza kumwogopesha.

“Kazi ya kuja..!” John alitaka kutukana, lakini na yeye akashindwa kumalizia alilotaka kulitamka.
“Nitakutukana Dina!” alisema kwa hasira. “Sijawahi kukutukana hata mara moja! Tafadhali Dina!”

Dina hakujibu!

John akasimama.
“Twende!” alisema kwa jazba. Dina hakujibu wala hakuinuka!

Hasira na wivu vikampagawisha John! Akamuinamia Dina na kuukamata mkono wake karibu na kwapa, akaanza kumuinua kwa nguvu. “Nadhani ulikuwa hunijui!” alisema na kuanza purukushani ya kumvuta Dina ambaye alikuwa akigoma kuinuka.

Tukio hilo likaanza kuwavutia wateja na wafanyakazi waliokuwepo eneo hilo. Wahudumu wawili wa kiume wakaenda eneo walilokuwepo Dina na John, wote kwa pamoja wakamvaa John ili amwachie Dina huku wakimsihi aache vurugu. Kitendo hicho kikamfanya Dina apate upenyo wa kuchomoka. Akafyetuka kama mtego ulioteguka, akakimbia kurudi mgahawani alikomuacha Richard!

John alikuwa mtu wa kufanya mazoezi mara kwa mara hasa ya kuogelea na kukimbia, akatumia nguvu za kushitukiza kuwasukuma wahudumu wale wawili waliokuwa wamemzuia na kuwabwaga chini. Akaitumia nafasi hiyo kumkimbiza Dina aliyekuwa nusu anakimbia nusu anatembea!

* * * * *

Richard alikuwa amekosa amani muda wote tokea Dina alivyokuwa ameondoka. Aliwaona Dina na John wakiongozana kuelekea ulipo ukumbi wa baa na kupotea machoni kwake, tokea wakati huo kukawa na ukimya! Alikuwa na uhakika, John alikuja hapo Arusha ghafla kwa kushitukiza na alikusudia kumshitukiza Dina. Hakujua ni nini kilichomleta ghafla, lakini alihisi huenda kuna kidudu mtu aliyemvujishia mahusiano yake na Dina yalivyo hapo Arusha.
Hakutaka Dina akakabiliane na John kama Dina alivyokuwa amesisitiza wakati John alipokuwa ameingia hapo mgahawani. Alikuwa na wasiwasi Dina asingekuwa salama kuwa peke yake na John. Kitendo hicho cha kuondoka pamoja na kwenda kuzungumzia baa na ukimya uliokuwa unazidi kuendelea kukamfanya akose amani. Kuna kipindi alijikuta alishawishika kutaka kumtuma mhudumu wa humo hotelini ili afuatilie nyendo za watu hao wawili, kisha aje kumripotia. Lakini alijikuta akikwama kuutekeleza uamuzi huo kwa hofu ya kuruhusu watu wengine waingilie mambo yasiyowahusu.

Wasiwasi aliokuwa nao kuhusu Dina aliyekuwa mikononi mwa John akiwa peke yake, ulimfanya ajikute akiinywa pombe ya mvinyo kwa kasi iliyomshitua hata yeye mwenyewe. Aliliona jukumu la kumtetea na kumlinda Dina lilikuwa ni lake endapo John ataamua kufanya lolote la kumdhuru. Kwa hiyo, kitendo cha kuendelea kuwepo hapo akiendelea kumsubiri Dina arudi kikawa kinamtia kwenye hali hiyo ya kupoteza umakini wa unywaji wake. Ghafla akawaona wateja waliokuwa wakiendelea kula chakula humo mgahawani walioko upande ambao wanaliona eneo la ukumbi wa baa, wakigeuza sura zao kwa mpigo na kuliangalia eneo hilo.

Richard akatambua kuna walakini unaotokea kati ya John na Dina!

* * * * *

Hakusubiri! Richard aliinuka na kuanza kujitoa katikati ya meza na kiti alichokuwa amekalia. Akawaona wahudumu wakitaharuki, kisha wote kwa pamoja akawaona wakielekea eneo la baa. Tukio hilo likamfanya Richard afanye papara ya kutoka, na alipokuwa akitoka miguu yake ikakisukuma kiti kilichokuwa nyuma

yake, kikapiga mwereka na kutoa sauti ya kuanguka. Akiwa hajali tukio la kuangusha kiti kutokana na akili yake kutekwa na kule watu wanakoangalia ambako ndiko waliko Dina na John, ghafla akamwona Dina akitokeza huku akikimbia kumfuata kule aliko! Baadaye akafuatia John aliyekuwa akimkimbiza Dina! Richard hakufikiri mara mbili, alijua Dina yuko hatarini na lilikuwa jukumu lake kumtetea. Akachomoka, lakini hakumfuata Dina!

Alimkabili John!

Wakavaana katikati kama fahali wawili wenye hasira. Wakashikana na kuzoana kimzobemzobe, wakaangushana kwa kishindo kwenye meza iliyokuwa jirani yao ambayo ilikuwa haina wateja. Nyenzo za kulia chakula zilizokuwa zimepangwa kwenye meza hiyo zikaanguka kwa kishindo cha kelele na kutawanyika chini. Hali ya vurugu ikawa imetawala kwa watu hao wawili. Wote walikuwa wameangukia sakafuni na kila mmoja akitaka kuwahi kuinuka kabla ya mwenzake. Wakakikirishana huku kila mmoja akionyesha misuli yake, lakini akawa ni Richard ndiye aliyewahi kutupa ngumi iliyompata John kwenye paji la uso. John alisukumwa chini na nguvu ya ngumi hiyo, Richard akawahi kupanda juu ya mwili wa John ambaye alianza kutoka damu sehemu aliyopigwa ngumi na kuanza kuikaba shingo ya John kwa mikono yake huku akitumia nguvu zote, kama vile alipania kumuua!

Wahudumu ambao walikuwa wakipiga kelele ya kutaka walinzi wa hoteli waitwe, walikwenda kwa pamoja kwenye ugomvi uliokuwa ukiendelea huku Richard akionekana amemdhibiti vyema John katika ile hali ya kumkaba koo. John akaonekana anapoteza nguvu!

“Mtoeni anamuua mwenzake!” kelele za wahudumu na wateja hasa wanawake zilisikika zikihimizana. Baadhi ya wahudumu wa kiume wakamvamia Richard na kuanza kumvuta kumwondoa kutoka mwilini mwa John na kufanikiwa kuwaachanisha. Kitendo hicho cha kuwaachanisha kikampa nafasi John ya kuokota kisu kabla ya Richard hajapata mhimili mzuri wa kujiinua. Kilikuwa kisu cha kulia chakula kati ya nyenzo zilizokuwa zimeeanguka chini, John akazitumia nguvu zake zote kumchoma kisu hicho Richard sehemu ya ubavuni!

Richard alipiga ukelele na kuangukia ubavu uliochomwa kisu na kukishikilia kisu hicho kilichojikita ubavuni mwake. Wakati huohuo damu ikachukua nafasi yake kutoka! Tukio hilo liliwachanganya watu wote waliokuwepo eneo hilo, sura zilizohamanika kwa hofu na taharuki iliyowatawala mioyoni mwao wakaonekana kuanza kuhaha kutafuta eneo la kukimbilia. Baadhi yao wakakimbilia kwenda kusubiri lifti.

Wakati vurugu za kila mmoja aliyekuwepo hapo akisema lake, John aliinuka na kuokota kisu kingine. Uso wake uliopigwa ngumi ukiendelea kuchirizika damu kwenye sehemu iliyopigwa, alianza kutamba kwa kuzunguka kama Sokwe na kuonekana kupagawa. Sura yake iliogofya, macho yake yaliyotapakaa damu aliyokuwa akijaribu kuifuta mara kwa mara kwa kutumia eneo la mkono karibu na bega lake yalionekana kuingiwa na woga. Akaanza mkwara wa kuwatisha kuwachoma kisu wateja wa hoteli waliokuwa wamesimama mbele yake. Wateja hao wakaanza kurudi nyuma huku wakitoa nafasi ya kumpisha John apite.

Kelele za kushakiziana zikaanza, “Jamani mkamateni anakimbia huyo!”

John alikuwa bado akitamba na kisu chake mkononi, aliupindisha mgongo wake kama anayepigana

miereka. Alikuwa na mwonekano wa kutisha, alikuwa kama mwendawazimu aliyepandwa na kichaa, aliyazungusha macho yake yaliyoonekana kuwa makubwa ghafla, akawa kama aliyekuwa akitafuta kimbilio. Akawaona baadhi ya wateja waliokuwa wakiwahi kuingia kwenye lifti kulikimbia eneo hilo. Naye akatimua mbio kuelekea huko huko kwenye lifti!

Kelele za taharuki zikasikika! “Huyo anakuja!”

Watu waliokuwa wamekwishaingia ndani ya lifti ambayo ilikuwa haijafunga mlango wakapagawa walipomwona John akikimbilia kwenye lifti walipo wao!

“Jamani huyo anakuja!” kelele za kutaharuki zilisikika kutoka ndani ya lifti.

****WIVU umezua vita!!! vita ya kumuwania DINA....DINA asiyekuwa na msimamo!!!

***NANI ATAIBUKA MBABE????

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA KUMI NA TANO

Kelele za taharuki zikasikika! “Huyo anakuja!”

Watu waliokuwa wamekwishaingia ndani ya lifti ambayo ilikuwa haijafunga mlango wakapagawa walipomwona John akikimbilia kwenye lifti walipo wao!

“Jamani huyo anakuja!” kelele za kutaharuki zilisikika kutoka ndani ya lifti.

Lifti ikaonekana sio tena sehemu ya kujiokoa! Vurugu mechi za kila mmoja kutaka kuwahi kutoka kwenye lifti zikaanza kuleta tafrani. Wengine waliowahi kutoka wakajikuta wakiangukia mlangoni kutokana na kihere cha kumkwepa mtu waliyekwishamhesabia kuwa ni mwendawazimu. Baadhi yao walioshindwa kujiinua kwa haraka waliamua kutambaa kwa magoti kumkwepa John aliyekuwa akielekea kwenye lifti. Ndani ya sekunde zisizozidi tatu, lifti ikawa haina mtu hata mmoja!

Mlango wa lifti ukaanza kujifunga, John akawahi kuuzuia kwa kutanguliza mguu na mkono wake. Akaingia! Lifti ikajifunga mlango, watu waliokuwepo kwenye ukumbi huo wote kwa pamoja wakajikuta wakiuangalia mshale uliopo juu ya mlango wa lifti ukionyesha lifti ilikuwa ikishuka chini!

Eneo la mapokezi lililopo chini nako kukawa na sintofahamu ya habari za kutatanisha zilizowafikia kuhusu rabsha inayoendelea mgahawani, habari zikapokewa kwa mitazamo tofauti na kuwaletea mkanganyiko watu waliokuwepo huko. Kila mmoja alisema lake baada ya mwito wa haraka wa kutakiwa walinzi wa hoteli wawahi kwenda eneo hilo. Taarifa hizo zikawakurupua baadhi ya walinzi waliokuwepo kuwahi kwenda mgahawani kwa kutumia ngazi badala ya lifti ambayo ilionekana kuchelewa kufika chini.

Lifti aliyokuwemo John ilifika chini na kupishana na wale walinzi walioamua kutumia ngazi. Mlango ulifunguka na watu waliopo pale wakamwona John akitoka akiwa ameshika kisu mkononi huku akiwa na damu usoni na mkononi. Taharuki ikawafika, kila mmoja akatoa njia kumpisha John aliyekuwa akikimbia kuelekea mlangoni huku akitishia kumchoma kisu yeyote aliyekuwa mbele yake!

Mlango wa kioo ukajifungua wenyewe baada ya John kuukaribia, akatoka nje huku wafanyakazi na baadhi ya wateja wakishangaa kumwangalia akitokomea!

***

DINA alikuwa amechanganyikiwa! Hali hiyo ikawa inamzidia kila alivyokuwa akimwangalia Richard aliyekuwa amelala sakafuni huku akiwa amezungukwa na watu. Wakati huo huo mtu mmoja aliyekuwa amepiga magoti kando ya mwili wa Richard alionekana akitoa huduma ya kwanza kujaribu kuizuia damu kwa kumuwekea nguo sehemu yenye jeraha la kisu.
Meneja wa hoteli ambaye aliwasili muda mfupi baada ya John kufanikiwa kutoroka bila ya kukamatwa, aliwahakikishia baadhi ya wateja na wafanyakazi waliokuwepo eneo hilo kuwa, gari la wagonjwa lilikuwa lipo njiani baada ya kulipigia simu kulihitaji. Walinzi wachache wa hoteli waliowahi kufika kabla ya John

hajawahi kutoroka na lifti, nao walikuwa wakishutumiwa kwa kushindwa kumzuia John alipokuwa akitoroka kwa kutumia lifti. Lakini wao walikuwa wakijitetea kuwa, mazingira yaliyokuwepo hayakuwawezesha kuweza kumkabili John, dai lao kubwa likiwa; hali aliyokuwa nayo John ilikuwa sio hali ya kumvamia bila ya kuwa na silaha, vinginevyo angeweza kumjeruhi mtu mwingine au pengine hata kuua!

Gari la wagonjwa liliwasili pamoja na gari la Polisi. Wahudumu wa gari hilo waliingia na machela, moja kwa moja walimchukua Richard na kumwingiza kwenye gari la wagonjwa ambako walichukua kifaa cha hewa ya oksijen na kukipachika eneo la usoni mwa Richard na kuondoka naye kumwahisha hospitali. Polisi waliowasili walipewa maelezo ya haraka kutoka kwa mashuhuda, hususan wafanyakazi wa hoteli waliokuwepo eneo hilo wakati wa mtafaruku huo ulipotokea.

Dina akawa mlengwa namba moja wa kuisadia polisi, wakaondoka naye kumpeleka kituoni!

* * * * *

Mara tu baada ya kufanikiwa kutoroka kutoka hoteli ya Masai Shield, John aliitumia nafasi hiyo kujipa huduma ya kwanza ya kuizuia damu iliyokuwa ikimtoka usoni kwa kuikandamiza kwa nguvu sehemu yenye jeraha kwa kuitumia leso yake hadi damu hiyo ilipoacha kutoka. Akajifuta baadhi ya sehemu zilizoingia damu na kufanikiwa kwa kiasi kidogo kuiondoa damu yote, kisha aliivua saa yake ya mkononi na viatu alivyokuwa navyo, vyote akavitupa kwenye kichaka cha eneo la kichochoro alichokuwepo. Baada ya kujiridhisha na hali aliyokuwa nayo, akajitokeza barabarani na kukodi teksi iliyomrudisha hotelini kwake.

Alipoingia hotelini, mwonekano aliokuwa nao ulimwogopesha mfanyakazi wa mapokezi aliyekuwa zamu.

“Vipi?” mfanyakazi huyo aliuliza huku akionyesha dhahiri alikuwa ameshituka.

“Nimevamiwa na wahuni!” John alimlalamikia mhudumu huyo. “Wapi?”

“Maeneo ya huko mitaani,” John alisema na kuzuga kuelekeza mkono wake upande hewa anakokuzungumzia. “Walinivamia kwa nyuma, wamenipiga na kuninyang’anya pesa na vitu vingine!”

Mfanyakazi wa mapokezi akaiangalia miguu ya mteja wake na kumwona hana viatu.
“Wamekupora na viatu?” aliuliza kama vile viatu ndio vilikuwa muhimu kwake.

“Na saa pia wamechukua!”
“Walikuwa wangapi?”

“Siikumbuki idadi yao, nadhani hawakupungua watano. Walinivamia kama mbwa mwitu!”

“Simu yako nayo?”

“Hawakufanikiwa kuichukua, nilipata upenyo nikawachomoka na kukimbia!”

“Itabidi tuliripoti tukio hili polisi!”

“Halafu iweje?” John aliuliza kwa mshangao.
“Sidhani kama polisi watanisaidia kunirudishia pesa na vitu nilivyoibiwa! Isitoshe wanaweza kunipotezea muda wangu kwa ajili ya kwenda mahakamani wakati sikumbuki hata sura ya mmoja wa vibaka hao. Ninachoshukuru wameniachia uhai wangu. Sihitaji kufanya kesi na mtu yeyote! Nipe funguo yangu ya chumbani nikapumzike!”

“Pole sana!” mtumishi wa mapokezi alisema kisha alitoa funguo na kumpa John.

Huko chumbani, John akiwa amechanganyikiwa alivichukua vitu vyake alivyokuwa amevitoa kwenye begi saa chache zilizopita wakati alipokuwa amewasili kwenye hoteli hiyo akitokea Dar es Salaam na kuanza kuvirudisha tena ndani ya begi. Alikuwa ameamua kutoroka usiku huo kurudi Dar es Salaam haraka iwezekanavyo! Alikuwa na uhakika polisi watakuwa wanamtafuta kwa udi na uvumba kutokana na tukio la kumchoma kisu Richard!

Akafanikiwa kuvirejesha vitu vyote kwenye begi na kuamua kuondoka, lakini alijikuta akisimama ghafla na begi lake mkononi kabla ya kuufungua mlango wa chumbani. Kilichomfanya asimame hapo mlangoni ni baada ya kujiuliza angeelekea wapi akishatoka hapo hotelini? Alikuwa na uhakika muda huo kusingekuwa na uwezakano wa kupata usafiri wa haraka utakaomtoa nje ya Arusha! Usafiri pekee ambao ungeweza kumwondoa haraka na kumfikisha angalau mji wa Moshi ungekuwa ni wa teksi, lakini hakuwa na fedha ya kukodi teksi ya kuweza kulipia kwa umbali mrefu kama huo. Isitoshe, bado angehitajika kuwa na pesa nyingine za kulipa gharama za usafiri za kumfikisha Dar es Salaam.

Akaukumbuka usafiri wa malori ambayo mengi huanza safari nyakati za jioni hadi usiku. Akaamini usafiri huo ungemsaidia kumwondoa hapo Arusha, lakini kikwazo kikawa, alikuwa hajui wapi angeyapata malori hayo usiku huo. Kwanza alikuwa halijui eneo linaloegeshwa malori hayo, pili, woga wa kukamatwa na polisi ulikwisha kumwingia. Hofu hiyo ikamjengea hadhari endapo atahangaika kwenye mitaa kuyatafuta malori ya kumuwezesha kusafiri usiku huo kungeweza kuchangia kumkamatisha kirahisi kwa polisi. Hali ya kuchanganyikiwa ikaanza kumtesa!

Aliondoka taratibu pale mlangoni alipokuwa amesimama na begi lake, akarudi kitandani na kukaa huku akionekana kuchoka ghafla. Majuto ya tukio alilolifanya la kumchoma kisu Richard yalikuwa yakimtafuna wakati wote na wakati huo huo akinung’unikia moyoni kuwa yote hayo yasingetokea kama sio Dina kumsaliti! Lakini pia kwa upande mwingine alijilaumu mwenyewe kwa hatua aliyoifanya ya kumchoma kisu Richard. Alijua ulikuwa ni wivu na hasira vilivyomfanya atende hayo. Nafsini alijirai mara kwa mara kuwa, alichotakiwa kufanya baada ya kugundua ukweli kuwa Dina alikuwa amemsaliti, ilikuwa ni kuondoka pale hotelini, kisha angefanya maamuzi mengine dhidi ya Dina mbele ya safari.

Maji yalishamwagika!

Hata hivyo kuna wakati alikuwa akijiridhisha kwa kujipa moyo kuwa kitendo alichokifanya kilistahili kwa Richard kwa sababu alitaka kumfanya bwege! Alimwona Richard ndiye aliyepaswa kulaumiwa kwa sababu alikuwa akiyajua mahusiano yake na Dina, na pia, alikuwa akifahamu kuwa, walikuwa wakikaribia kufunga ndoa! Kwa nini Richard anifanyie ushenzi kama huu? alijiuliza. Alitaka kunifanya zoba? Alinidharau kuwa nisingeweza kumfanya lolote? John akapiga kite cha hasira humo chumbani, akajiinamia na kukipakata mikononi kichwa chake. Alikiri alikuwa amejiingiza kwenye matatizo mazito ambayo hakuyatarajia, na kwa

mara ya kwanza alijikuta akiilani siku ambayo yeye na Dina walionana kwa mara ya kwanza! Yasingenifika yote haya! aliwaza.

Akiwa bado amejiinamia, mawazo yake yalirudi hotelini Masai Shield na kulifikiria tena tukio lililotokea. Alijikuta akitaka kufahamu hali ya kiafya aliyonayo Richard baada ya kumchoma kisu. Hofu ilikuwa imemtawala kwa kitendo hicho, lakini alijipa matumaini kuwa, kisu alichokitumia kumchoma nacho Richard kilikuwa ni kisu cha mezani cha kulia chakula na aliamini hakikuwa na urefu mkubwa wa kuweza kuingia kwenye mwili wa binadamu na kuleta madhara ya kutishia uhai wa mtu. Hakitakuwa kimemsababishia madhara makubwa! alijipa imani. Sidhani kama anaweza akafa! Wazo hilo likamfanya auinue juu uso wake na kufumba macho. Akasali kimya kimya yasitokee maafa kama hayo.

Kuingiwa na wazo la kuwa anaweza akawa ameua, alijikuta akiingiwa na hofu nyingine ya aina yake! Wazo la kutoroka usiku huohuo likarudi kwa kasi mpya, lakini pia akapata mashaka na uamuzi huo. Alikiri kuwa, hata kama angeweza kuutekeleza uamuzi wa kutoroka usiku huo, bado lingekuwa sio suluhisho, angeendelea kutafutwa na polisi bila kujali kama ameua au hakuua, kwani kosa alilokuwa amelifanya bado ni la jinai na lazima angetafutwa kwa ajili kushitakiwa.

Kwa mzunguko huo, John alikiri kukimbia sio dawa ya tatizo hilo, labda angekimbilia nje ya nchi kama vile Kenya. Ingekuwa ni rahisi kwa kutokea hapo Arusha kuweza kukimbilia Nairobi, lakini angekimbilia kwa nani huko Nairobi? Kwanza katika maisha yake alikuwa hajawahi hata kulikanyaga jiji hilo! Pili, alikuwa hamjui mtu wake yeyote anayeishi huko!

Lakini pia, tatizo jingine alililoliona mbele yake ni familia aliyoingia nayo kwenye ugomvi. Familia ya mzee Ken Korogwe! Familia tajiri yenye uwezo wa kuapa kupania kumtafuta na wakampata! Ni familia yenye nyenzo zote za uwezeshaji wa kurahisisha kutafutwa kwake popote atakapokimbilia na angepatikana! Ni familia ambayo kwao dunia ni kama kijiji pindi wakianza msako wa kumtafuta. Kwa hiyo hata kama angekimbilia maeneo ya Alaska au Australia ambako ni mbali kwa kutokea ukanda wa Afrika ya Mashariki, bado angekamatwa! Hapo pakamvunja nguvu! Akakiri hana pa kukimbilia!

Kukiri huko kuwa hana pa kukimbilia, John akaanza kufikiria kujipeleka mwenyewe polisi! Aliuona uamuzi huo ndio wa busara, angejipeleka na angelielezea tukio zima linalohusisha mahusiano ya mapenzi kati yake na Dina na wale wote waliojihusisha na Dina kwa njia moja au nyingine na angemtaja Mohsein kuwa ndio chachu ya kuyajua yote hayo.
Akauafiki uamuzi huo wa kujipeleka mwenyewe kituo cha polisi!

* * * * *

Mtumishi wa Idara ya Mapokezi wa hoteli aliyofikia John hakuridhika na maamuzi yaliyofanywa na John kwa kuliacha tukio la kuvamiwa na wahuni kisha kuporwa liishie kimya kimya. Matukio ya aina hiyo yaliwahi kutokea siku za nyuma kwa wateja wao ambao walidai kama alivyodai John kuwa matukio yaliyowakuta yasiripotiwe polisi kwa ajili ya kukataa usumbufu. Awali walikuwa wakizikubali hoja za namna hiyo zilizotolewa na wageni wao wa hoteli, matokeo yake hoteli hiyo ikaingia lawamani kuwa ni hoteli inayoshirikiana na vijana wa kihuni kuwaibia wateja wa hotelini hapo.

Lakini baada ya kuathirika kibiashara kutokana na sifa mbaya iliyowakuta, utawala wa hoteli hiyo ulichukua

hatua za makusudi kurudisha heshima ya hoteli hiyo kwa kujiweka karibu na polisi kwa matukio yote ya kihalifu ambayo yangewatokea wateja wao. Lakini licha ya kujiweka karibu na polisi, pia wakaamua kuandika waraka kwa wafanyakazi wote kuwa watoe taarifa kwa uongozi wa hoteli pindi linapotokea tukio la kihalifu kwa mteja wao. Waraka huo ukasisitiza, yeyote atakayeshindwa kufanya hivyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Sheria hiyo mpya ndio iliyomlazimisha mtumishi huyo wa mapokezi kutolipuuzia tukio la vibaka kumvamia John lisiishie kimya kimya. Akaenda kuliripoti kwa meneja wake wa zamu usiku huohuo.

“Anaitwaje huyo mteja?” meneja wa zamu alimwuliza mtumishi wake baada ya kupokea taarifa hizo.

“John Sailas, anatokea Dar es Salaam na aliwasili jioni ya leo. Amepanga chumba namba 112, kwenye fomu ya maelezo amejaza kukaa kwa usiku mmoja. Maelezo yake yanaeleza ni mwajiriwa wa cheo cha karani wa stoo na anatarajia kurudi Dar es Salaam baada ya kuondoka Arusha.”

“Alikuaga anakwenda wapi wakati alipotoka kabla ya kuvamiwa na vibaka?”

“Alikuja na kuacha funguo kwangu na kusema anatoka. Hakuniambia wapi anapoelekea na sikumwuliza. Aliporudi ndio akanieleza kuwa alivamiwa na vibaka.”

“Ulimwuliza ni wapi alikovamiwa na vibaka?”

“Aliniambia alivamiwa maeneo ya katikati ya mji, hakunitajia sehemu rasmi. Tatizo ni kuwa, hakuonyesha kutaka kulizungumzia sana tukio hilo na sijui ni kwa nini. Hata nilipomshauri tuliripoti tukio hili polisi, alikataa.”

“Itabidi tuwaarifu polisi, wao ndio watakaoamua kama waje kumhoji au waliache kama mhusika anavyotaka. Huwezi kujua matokeo ya aina hii yana athari za aina gani. Je, kama ni jambazi ametoka kufanya uhalifu na kupata misukosuko kisha akasingizia kuwa ni vibaka ndio waliomvamia? Hili suala ni la kuliripoti polisi na wao watajua cha kufanya!”

Muda mfupi uliofuata, madai yaliyotolewa na John ya kuvamiwa na vibaka, meneja wa zamu wa hoteli hiyo akayaripoti polisi!

***

DINA Nzasa akiwa Kituo cha Polisi cha Mkoa wa Arusha alifanyiwa mahojiano na kachero Mussa kuhusu tukio lililotokea hoteli ya Masai Shield. Kabla ya kuruhusiwa kuondoka, alikiri kumfahamu John na akaelezea kuwa ni mchumba wake, lakini pia, alikiri kitendo kilichofanywa na John kilitokana na wivu wa kumtuhumu kuwa anatembea na Richard.

“Ni kweli unatembea naye?” kachero Mussa aliyekuwa akimhoji alimwuliza.

“Siwezi kukujibu swali hilo!” Dina alijibu.

Mussa akajikuna kichwani kwa kutumia kalamu aliyoishika. “John alikuja kufanya nini Arusha?”

“Sijui.”

“Uliujua ujio wake?”

“Sikuujua. Nilimwona akiingia ghafla hotelini!”
“Alikuwa akijua kama upo Arusha?”

“Ndiyo, isitoshe nilimuaga.”

“Alikuwa akijua kama ulifikia hoteli ya Masai Shield?”

“Awali hakujua ningefikia hoteli ipi kwa sababu hata mwenyewe nilikuwa sijui ningefikia wapi. Lakini baada ya kuwasili hapa Arusha ndipo nikawasiliana naye kwa simu nikamwambia kuwa nimefikia hoteli ya Masai Shield.”

“Unasema John anakutuhumu kuwa unatembea na Richard, ni mahusiano gani yaliyopo kati yako na Richard mpaka John afikirie kitu kama hicho?”

“Kama nilivyokwambia awali, Richard ni bosi wangu. Hakuna zaidi ya hilo.”

“John aliwahi kuziweka wazi hisia za tuhuma hizo kwako?”

“Kwa kipindi chote cha uhusiano wetu amekuwa na hisia hizo na alikuwa akizizungumza kwangu.”

“Unayo sababu yoyote unayoijua ya kumfanya awe na hisia hizo?” “Kwa sababu nilianza mahusiano naye baada ya uhusiano wangu na Richard kuvunjika. Hilo ndilo linalomfanya John asiwe na imani kuwa uhusiano wangu na Richard umekufa.”

“Lakini si anajua kama mko pamoja kikazi?”
“Anajua.”

“Kabla ya tukio hili, kuliwahi kutokea tukio la wao kukutana na kutupiana maneno kwa ajili yako?”

“Sidhani, kwa sababu hakuna yeyote kati yao aliyewahi kunilalamikia.”

“Ulisema John alipofika pale hotelini alikukuta ukiwa umekaa meza moja na Richard?”

“Ndiyo.”

“Alisema nini baada ya kuwakuteni?”

“Kabla ya kutukaribia pale mezani, niliwahi kuinuka nikamfuata na tukazungumza pembeni.”

“Alikwambia nini baada ya kuwa naye?”

“Tatizo alikuja kiushari, aliponiona tu, akadai kutaka kuondoka na mimi ili twende kwenye hoteli aliyofikia yeye. Nikamkatalia!”

“Alikupa sababu ya uamuzi wake huo?”
“Sababu ni kuwa mimi ni mchumba wake.”

“Sio kwa sababu amegundua kuwa una mahusiano ya mapenzi na Richard?”

Dina hakujibu.

“Alikutajia hiyo hoteli aliyofikia?”

“Tulikosa kuelewana kabla hata ya kunitajia hoteli yenyewe. Akataka kunichukua kwa nguvu, ndipo nilipoamua kukimbia, akanifukuza. Richard akamzuia na matokeo ndio hayo yaliyotokea.”

“Unaweza ukatabiri endapo kama hatorudi hotelini ni wapi muda huu anaweza akawepo? Nakuuliza hivyo kwa sababu hatutarajii kumkuta hotelini akiwa amejificha baada ya kufanya tukio kama lile ingawa bado hatujajua ni hoteli ipi aliyofikia.”

“Mimi ni mara yangu ya kwanza kuja Arusha na hajawahi kuniambia kama ana jamaa yake yoyote hapa Arusha.”

“Unayo picha yake?”

“Unamaanisha kwa kule hotelini nilipo?”

“Kama ni hotelini au kwenye simu yako, nikiwa na maana kama nitaihitaji leo ninaweza nikaipata?”

“Sina kawaida ya kutembea na picha yake.”

Baada ya hapo, Mussa akaonekana kutokuwa na maswali zaidi ya kuhoji. Akalazimisha kuhoji maswali mengine ya hapa na pale lakini yakakosa msaada wa kumsaidia kuweza kujua John angepatikana vipi.

“Richard amepelekwa hospitali gani? Nataka kwenda kumwona!” Dina alisema baada ya kuhisi askari huyo hana maswali mengine zaidi.

“Bado sijajua. Itanibidi nifanye mawasiliano na wenzangu walioondoka naye. Huenda tukaenda pamoja hospitali.”

Kachero Mussa alimsindikiza Dina hadi nje ya Kituo cha Polisi na kumpeleka kwenye gari la polisi, akamwomba amsubiri humo kwenye gari. Kisha Mussa alirudi ndani kituoni na kufanya mawasiliano ya

simu na polisi waliokuwa wameongozana na Richard alipokuwa akipelekwa hospitali.

Dina akiwa peke yake kwenye gari la polisi kwa takribani dakika zisizopungua kumi, alikuwa kwenye shinikizo lililokuwa likimchanganya. Tukio la kupigana kati ya Richard na John lilimkosesha amani wakati wote na kujikuta akipata wakati mgumu wa kupata jibu baada ya kujiuliza, ilikuwaje John akajua kuwa yeye na Richard walisafiri pamoja kwenye ndege? Na alijuaje yeye na Richard walikuwa wakiishi chumba kimoja?

Dina akakumbuka jinsi alivyokuwa amemdanganya John kwa kumwambia alikuwa hakusafiri na Richard kwenye safari hiyo ya kuja Arusha. Au ni mama ndiye aliyemwambia John kuwa, yeye na Richard walisafiri pamoja kwenye ndege? alijiuliza. Swali hilo likayafanya mapigo yake ya moyo yafanye mshituko baada ya kutambua upo uwezekano wa mama yake kumwambia John ukweli huo! Dina alijikuta akitamani kujitafuna vidole vyake baada ya kugundua alifanya kosa kutomhadharisha mama yake kuhusu siri hiyo!

Ujio wa kurudi kachero Mussa hapo garini ukamwondoa Dina kwenye jinamizi lililokuwa likimwandama baada ya kushituliwa na mlango wa gari uliofunguliwa na kumwona Mussa akiingia na kukaa nyuma ya usukani.

“Wenzangu walioshiriki kumpeleka Richard hospitali, wanasema Richard yuko chumba cha upasuaji akifanyiwa upasuaji. Nadhani suala la kwenda kumwona ni mpaka kesho atakapokuwa amepelekwa wodini,” kachero Mussa alisema na papohapo akaliwasha gari.
“Ni vyema nikurudishe hotelini na kesho asubuhi nitakufuata kukupa taarifa za hospitali.”

“Wanasemaje kuhusu hali yake?” Dina aliuliza huku akijaribu kuituliza akili yake.

“Wanasema, aliingizwa chumba cha upasuaji akiwa anaongea. Inaonyesha hayuko kwenye hali mbaya inayohatarisha maisha yake.”
“Mungu atamsaidia!” Dina alisema.

“Amen,” Mussa alijibu na kuliondoa gari.

* * * * *

Kwa mara ya kwanza tokea awasili hapo Arusha na kuyafurahia maisha ya kifahari kwa kunywa mivinyo mitamu, vyakula vya bei ghali vyenye ladha inayokufanya ujisikie kula, kulala kwenye chumba cha kifahari cha hoteli yenye hadhi ya nyota tano, Dina kwa mara ya kwanza alijikuta akiiangalia hoteli hiyo kwa mtazamo tofauti. Sasa hoteli hiyo alivyokuwa akiteremka kutoka kwenye gari la polisi alikuwa akiiona kama ngome fulani ya Kishetani! Wakati akiingia hotelini humo eneo la mapokezi aliyahisi macho ya wafanyakazi yakimwangalia tokea mlangoni na baadhi yao walidiriki kumpa pole na yeye alizipokea kwa kujibu kwa sauti hafifu.

Chumbani ambako mara baada ya kufika alijitupa kitandani kama mzigo akiwa na nguo zake. Macho yake yaliangalia juu kwenye dari iliyonakshiwa na kujikuta akiirudisha kumbukumbu ya kuwaona Richard na John walivyokuwa wakipigana. Tukio hilo lilikuwa limenasa kwenye ubongo wake na kuwa kama gurudumu la sinema lililokuwa likijizungusha kichwani mwake kwa wakati wote. Ni tukio lililomfedhehesha kila

alipolifikiria.

Ghafla akaanza kulia! Majuto yalikuwa yamemwinamia na kila kitu kikaanza kujitokeza kinyume. Alijiona ni mgeni hotelini hapo, hakuwa na mtu yeyote ambaye angeweza kumshirikisha kwa kumweleza matatizo yaliyomfika! Lakini pia, hata hapo Arusha alikuwa ni mgeni napo, hakuwa na mtu ambaye pengine angesema amfuate nyumbani kwake au amuite hapo hotelini angalau amshirikishe kulijua jinamizi linalomwandama usiku huo!

Alikuwa peke yake!

Baada ya kulia kwa dakika kadhaa akiwa peke yake humo chumbani, hatimaye akili ikamjia kuwa kulikuwepo na mtu hapo Arusha ambaye angeweza kuzungumza naye! Aliamini huyo angeweza kushirikiana naye kulizungumza tatizo hilo pengine kwa mapana zaidi ingawa aliamini kusingekuwa na maelewano kati yao.

Alikuwa amemkumbuka John!

Alitaka kuzungumza naye angalau amfahamishe kuwa polisi walikuwa wakimtafuta na alikuwa tayari hata kumpa msaada wa kifedha usiku huo ili atoroke. Alikiri nafsini mwake kuwa ni yeye ndiye aliyehusika kumwingiza John kwenye wakati huo mgumu. Fikra hizo za kumwona John ameingia ndani ya matatizo kwa ajili yake zilimwumiza moyo, akamwonea huruma kijana huyo na kutambua ni jinsi gani anavyompenda!

Nafsi yake ikawa ikimsuta jinsi alivyomsaliti mchumba wake huyo, akaulaani moyo wake jinsi ulivyoshindwa kukabiliana na vishawishi vilivyomkabili. Lakini bado alijiona anayo nafasi ya kumwomba msamaha John na angeweza kuitumia nafasi ya kumpigia simu kuzungumza naye, pia angeitumia nafasi hiyo kumshawishi aondoke haraka hapo Arusha kwa kumtahadharisha kuwa polisi wanamtafuta na angemwahidi kumsaidia kwa kumpa pesa za kutosha alizopewa na Richard! Angeweza kumtumia pesa hizo kwa njia ya simu kwa kuzituma kupitia moja ya ofisi ya kampuni ya simu ambayo ina tawi lake hapo hotelini ambalo linafanya kazi kwa saa ishirini na nne.

Dina alijifuta machozi kwa kutumia kiganja chake, kisha akajifuta kamasi nyembamba kwa kutumia nguo aliyoivaa. Uamuzi wa kumpigia simu John ndio ungefuata, lakini alijikuta akipata kigugumizi cha kuufanya uamuzi huo. Alikuwa akiogopa kuzikabili lawama atakazopewa na John, hakuwa na uhakika angezijibu vipi shutuma hizo. Akapiga moyo konde, akaichukua simu yake na kumpigia John.

John hakupatikana!

Nguvu zikamwishia, kilio kikawa faraja yake!

***DINA katika majuto, RICHARD hoi hospitali, JOHN katika harakati za kutoroka.....NINI HATMA YA SAKATA HILI.

RIWAYA: WIVU
MTUNZI: BEKA MFAUME

SEHEMU YA MWISHO

MLIO wa simu ndio uliomshitua kutoka usingizi! Alichukuliwa na usingizi bila ya kujitambua alipokuwa amejilaza wakati akilia. Alishangaa kuiona asubuhi imeshafika na ndipo alipojitambua alikuwa amelala na lile gauni alilokuwa amepanga aende nalo Casino akiwa na Richard usiku uliopita. Kujiona ameamka akiwa na gauni hilo kukamtonesa kulikumbuka zogo la usiku lililotokea hapo hotelini. Simu iliyokuwa ikiita ilinyamaza, lakini sekunde chache baadaye ilianza kuita tena.

“Haloh,” Dina alisema baada ya kuipokea simu ya chumbani kwake, kisha akapiga mwayo.

“Samahani,” sauti ya kike ilisema kwenye simu. “Una mgeni wako hapa mapokezi. Amejitambulisha kwa jina la kachero Mussa.”

Ndipo fahamu kamili zilipomrudia kuwa alikuwa na ahadi na kachero huyo asubuhi hiyo.

“Naomba anipe dakika kumi za kujiandaa,” Dina alisema kwenye simu. Kisha akamsikia msichana aliyepo kwenye simu akizungumza na mtu, akajua alikuwa akizungumza na kachero Mussa.

“Anasema utamkuta akikusubiri hapa mapokezi,” hatimaye msichana wa mapokezi alisema.

“Mwambie anisubiri mgahawani, anaweza akaagiza kifungua kinywa kwa bili yangu,” Dina alisema na kisha kukata simu.

Alitumia muda zaidi kuliko ule aliouahidi. Alikoga, kisha alijikwatua kwa vipodozi akiwa amekaa kwenye stuli iliyopo mbele ya kioo cha kujiangalia wakati wa kuvaa. Moyo wake ulikuwa bado mzito kutokana na sintofahamu iliyokuwepo kati ya John na Richard. Wote alitaka kujua taarifa zao zikoje. Kwa John ni kwa ajili ya kujua kama amekwishakamatwa na polisi, na kwa Richard ni kuhusu afya yake inavyoendelea baada ya upasuaji aliyofanyiwa.

Kwa upande wa Richard angalau alikuwa na matumaini ya kuonana naye pindi atakapokwenda kumwona hospitali atakapoongozana na kachero Mussa. Alikuwa na uhakika asingemkuta kwenye hali ya kuruhusiwa kuzungumza na wageni kwa kuwa hali yake ya kiafya ingekuwa bado haijatengemaa. Akaijenga taswira ya atakavyomwona Richard akiwa kitandani. Taswira hiyo akaijenga kwa kumwona Richard akiwa hajarudiwa na fahamu kikamilifu kutoka kwenye madawa ambayo angekuwa amepewa kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji. Alijua asingeweza kuzungumza naye zaidi ya kumwangalia na kisha angeondoka, lakini akajenga matumaini ya kuzungumza naye wakati wa jioni atakavyorudi tena hospitali. Alikuwa na uhakika muda huo John angekuwa amerudiwa na fahamu kikamilifu.

Akapanga jioni atakapokuwa anarudi tena hospitali itamlazimu anunue maua na kadi ya kumtakia Richard uponaji wa haraka.

Akiliona tatizo la Richard likiwa halimwumizi sana kichwa, Dina alikiri tatizo la John ndilo lililokuwa likimpa wakati mgumu. Alijiuliza kwa muda huo wa asubuhi John angekuwa wapi? Alijua John asingekuwa mpumbavu wa kuendelea kuwepo hotelini wakati akijua amefanya tukio ambalo limemwingiza kutafutwa na polisi, lakini pia akajengwa na wasiwasi zaidi huenda John hakulala kabisa huko hotelini. Fikra hizo zikamfanya ayahisi machozi yakimlengalenga machoni baada ya kuifikiria hali ambayo angekuwa nayo John. Akaijenga taswira ya kumwona John akiwa kwenye wakati mgumu akiishi kwenye hali ya kukosa

amani kutokana na woga wa kukamatwa na polisi! Kwa mara nyingine, Dina alijisikia vibaya baada ya kujiona ndiye aliyeisababisha hali hiyo kwa John!

Wazo la kumpigia tena simu John likamrudia. Shinikizo la kutaka kumsaidia kwa kumpatia pesa za kumsaidia kutoroka likaanza tena kuisumbua nafsi yake, aliamini kitendo hicho kingeweza kumwonyesha John kuwa yuko pamoja naye kwenye tatizo hilo. Kwa upande mwingine, aliuona msaada huo ungekuwa ni sehemu ya kumwomba John msamaha kwa kile kilichotokea!

Aliifuata simu yake iliyokuwa bado ipo kitandani na kumpigia John. Alipokuwa akisubiri simu hiyo ianze kuita upande wa pili anakopiga, kimya hicho cha kusubiri pamoja na kwamba kilikuwa ni cha muda mfupi, lakini kilimuweka kwenye wakati mgumu. Kilimjengea woga wa kukabiliana na jibu kutoka kwenye simu kuwa, mteja anayempigia hapatikani. Akaomba hilo lisitokee.

“Samahani, mteja unayempigia hapatikani, jaribu tena baadaye!” sauti kutoka kwenye simu ilisikika.

Dina aliishiwa nguvu! Akaushusha chini mkono wake uliokamata simu, kisha akauinua juu uso wake uliokata tamaa. Alikuwa na uhakika John alikuwa amezima simu yake na asingeweza kumpata! Hakuhitaji kujiuliza ni kwa nini, yeyote angekuwa kwenye mazingira kama aliyonayo John, angefanya hivyo. Akatamani John apate akili ya kuiwasha simu yake kisha ambipu japo mara moja. Alitamani iwe hivyo, lakini kwa hali halisi, ilikuwa sawa na mtu mwenye kiu anayetamani kukiona kidimbwi cha maji jangwani!

Ghafla akamkumbuka kachero Mussa, alikwisha kumsahau!

Kitendo cha kumkumbuka kachero huyo kuwa alikuwa akimsubiri kikamtoa chumbani haraka. Akamkuta akiwa anamalizia kifungua kinywa alichokiagiza. Kilikuwa ni kifungua kinywa kilichokamilika, kinachojulikana kwa jina la English Breakfast.

“Samahani kwa kukuweka sana,” Dina alisema huku akivuta kiti na kukaa kwenye meza aliyokuwepo Mussa.

“Usijali,” Mussa alisema huku akijifuta mdomo kwa kitambaa cha mezani.
“Nashukuru kwa kifungua kinywa.”

“Usijali,” Dina alisema. Kisha aliagizia chai na vipande vya mikate ya kuokwa.

Dina alianza kunywa juisi na kusubiri chai aliyoiagiza.
“Hali ya Richard inaendeleaje?” aliuliza baada ya kumeza funda la juisi.

“Bado sijapata habari zake,” Mussa alisema huku akijaribu kutoyatuliza macho yake.
“Nilipitia kituoni kujua kama kungekuwa na ripoti yoyote iliyoletwa na askari aliyekuwa akimlinda hospitali, hata hivyo alikuwa bado hajaiwasilisha. Nadhani askari mwenzake wa kuchukua nafasi yake atakuwa amechelewa kwenda kumtoa.”

“Na vipi kuhusu John?”

“Kuna mtu mwenye jina lake amekamatwa jana usiku na polisi,” Mussa alisema.
“Tutaanza kwenda huko ili ukamthibitishe kama ndiye yeye, kisha ndipo tutakapokwenda kumwangalia Richard.”

Taarifa ya kukamatwa kwa John ikampotezea Dina hamu ya chai aliyoiagiza!

“Nitakunywa chai nitakaporudi!” Dina alisema huku akivuta nyuma kiti alichokalia na kusimama. Alijua asingeweza kuinywa chai ambayo angeletewa na hakutaka kachero Mussa alibaini hilo. “Twenzetu!” alimalizia kwa kusema hivyo akiwa amekwishajitoa kwenye meza.

“Kwa nini usingekunywa kabisa,” Mussa alishauri.
“Huwezi kujua, unaweza ukajikuta umechaelewa kurudi, ukarudi hapa mchana baada ya shughuli ya huku na kule. Unajua mambo yetu ya kipolisi hayana dogo.”
“Mara nyingi sipendi kunywa chai asubuhi,” Dina alidanganya.

“Nimekwishazoea kufanya kazi wakati wa asubuhi bila ya kunywa chai.”

Mussa akataka kuongeza neno, lakini alisita baada ya kumwona Dina akiwa amekwishaupachika mkoba wake begani na kutangulia kuondoka. Akaamua kuongozana naye. Wakapita kwa mtunza fedha ambako Dina alilipa gharama za kifungua kinywa alichokula Mussa.

Wakati wakiwa wamekwishatoka nje ya hoteli, Dina alijikuta akiwa kwenye wakati mgumu kimawazo. Alikuwa tayari amechanganyikiwa na habari za kukamatwa kwa John, lakini alipata ugumu pale alipokuwa akijitahidi kuificha hali hiyo isionekane na kachero huyo anayeandamana naye.

Wakiwa kwenye gari, kachero Mussa hakuonyesha kuwa kwenye mdadi wa kuzungumza, sehemu kubwa ya mwonekano wake alipokuwa akiliendesha gari, alionekana kuwa kwenye tafakuri iliyomtuliza. Ukimya ukajitokeza kati yao, Dina akaomba hali hiyo iendelee kuwa hivyo, kwani naye alihitaji utulivu utakaomuweka kwenye kujiandaa jinsi atakavyokabiliana na John. Hakujua angeongea naye nini wakati akiwa amesimamiwa na polisi, lakini kilichokuwa kikimsumbua zaidi ni pale atakavyolijibu swali la kachero huyo litakalomtaka athibitishe mbele ya John kama huyo aliyekamatwa ni John! Alikuwa na uhakika jibu la kukubali kumthibitisha John lingekuwa kama usaliti atakaokuwa amemfanyia John!

Siku mbili, tatu za nyuma alipokuwa kwenye gari akienda ofisini akiwa na Richard, Dina alikuwa akifurahia kuiangalia mandhari ya jiji hilo la Arusha kila alivyokuwa akipita, lakini asubuhi hiyo, kwa mara ya kwanza tokea afike kwenye mji huo, Dina aliuona mji huo kama eneo asilotaka kuliona kwenye maisha yake! Hali hiyo ilimfanya kukitumia kimya kilichowekwa na kachero Mussa kufumba macho yake wakati wote huku akiusikilizia myumbo unaofanywa na gari wakati likipita kwenye miinuko ya barabara au wakati likikata kona. Kibaya zaidi, hakutaka hata kushuhudia kule anakopelekwa!

Alijikuta akifumbua macho baada ya kulisikia gari hilo limesimama na kisha likazimwa injini. Akajua wamefika! Lakini alipoyaangaza macho yake akashangaa kuliona gari hilo likiwa limesimama nje ya hospitali ya Mount Meru. Akamwangalia kachero Mussa kama vile uangaliaji wake ungemfanya Mussa aujibu mshangao wake. Hata hivyo, Mussa hakuonekana kukijua kilichokuwa kinafanyika kwa Dina, yeye alikuwa ameinama akihangaika kuufungua mkanda wa kiti cha gari.

“Umeamua tuanze kwa kumwangalia Richard?” Dina aliamua kuuliza. Mussa alishusha pumzi kwa nguvu na kuangalia mbele ya kioo cha gari, akaonekana kama vile alikuwa akiwaangalia watu waliokuwa wakikatisha

mbele ya gari hilo.
“Hapana!” alijibu bila ya kuacha kutazama mbele. Jibu hilo likamtia hofu Dina. Akawa na wasiwasi kuwa, maadam kama siye Richard aliyewafanya waje hapo, basi atakuwa ni John! Dhana ikamjenga kuwa John atakuwa alikumbana na kipigo cha polisi baada ya kukamatwa na majeruhi aliyoyapata ndio yatakuwa yamemfanya alazwe hospitalini hapo.

“John amelazwa?” Dina aliuliza na sauti yake ilishindwa kuificha hofu aliyokuwa nayo huku akiwa bado hajayabandua macho yake kumwangalia kachero Mussa.

“Amefariki!” Mussa alijibu kama vile alikuwa akizungumza peke yake. Akageuka na kumwangalia Dina aliyekuwa tayari amepigwa na mshangao usoni. Akaendelea, “Alipatikana kwenye chumba chake cha hoteli aliyofikia akiwa amejinyonga!”

Shingo ya Dina ikalegea ghafla, mboni za macho yake zikajibinua kuelekea juu!

* * * * *

Kitendo cha Dina kuzirai mle ndani ya gari kulimfanya kachero Mussa achanganyikiwe baada ya kujaribu kuutingisha mwili wa Dina kwa lengo la kumuamsha bila ya mafanikio. Akatambua kulihitajika huduma ya kihospitali ili kuweza kukabiliana na tatizo hilo. Akaufungua mlango wa gari na kuchomoka kwa kasi, akakimbilia idara ya mapokezi ambako alijitambulisha cheo chake kwa mfanyakazi wa hospitali mwenye beji iliyomwonyesha ni mtumishi wa mapokezi aliyekuwa anataka kuingia chumba cha mapokezi akitokea nje na kumweleza kilichomsibu.

“Kwa hiyo huyo dada yuko kwenye gari yako?” mtumishi huyo aliuliza kwa utulivu kama vile tatizo alilloambiwa halikuhitaji huduma ya dharura.

“Ndiyo yupo kwenye gari yangu!” Mussa alisema na kuonekana akikosa utulivu.

“Subiri nikutafutie watu wa kwenda kumchukua,” mfanyakazi yule wa mapokezi alisema. Akaanza kurudi alikotoka, lakini kabla hajachanganya hatua akatokea mtu, mtu huyo akamfanya asimame, wakaanza kusalimiana na kitendo hicho kiliwachukua takribani dakika moja kama vile hakukuwa na jambo la dharura alilotakiwa mtumishi huyo wa hospitali alishughulikie.

Kitendo hicho kikamchafua Mussa. Hasira iliyompanda kichwani ikamsukuma kutaka kumfokea mtumishi huyo wa hospitali, lakini kabla hajafanya hivyo, akatokea mhudumu wa wagonjwa ambaye ni mwanamke, akaitwa na yule mtumishi.

“Omba msaada wa mwenzako ili mfuatane na huyu bwana, ana mgonjwa wake yuko kwenye gari amezidiwa,” alisema yule mtumishi wa mapokezi.

Kitendo hicho kikamfanya kachero Mussa azishushe hasira zake. “Utaandamana na huyu dada kwenda kumchukua mgonjwa wako,”
mtumishi wa mapokezi alimwambia Mussa, kisha akaendelea kuzungumza na mtu wake na kuonekana amelimaliza tatizo hilo.

Muuguzi wa kike na wa kiume walikisukuma kitanda cha magurudumu hadi kwenye gari alilokujanalo Mussa, wakamtoa Dina na kumpakia kwenye kitanda na kumuwahisha kwenye chumba cha daktari huku Mussa akifuata nyuma yao.

* * * * *

Dina alihifadhiwa kwenye chumba maalumu hadi aliporejewa na fahamu. Alirejewa na fahamu akiwa peke yake baada ya muuguzi wa kike anayemwangalia akiwa ametoka nje. Dina hakutambua yuko wapi, lakini akahisi kama yuko hospitali. Akafumba macho kujaribu kuvuta kumbukumbu ya kutaka kujua ilikuwaje akawepo hapo. Harufu ya madawa ya binadamu ikamhakikishia kuwa yuko hospitali, lakini akawa bado hajaelewa alifikaje hapo. Akavuta tena kumbukumbu kutaka kujua mara ya mwisho alikuwa wapi kabla ya kufika hapo. Akaikumbuka hoteli ya Masai Shield!

Kuikumbuka hoteli hiyo ikawa kama vile imemfungulia rejesho la kumbukumbu zilizokuwa zimepotea. Akaanza kukumbuka kimoja baada ya kingine…

Amefariki! hatimaye akaikumbuka kauli ya kachero Mussa alivyokuwa naye kwa mara ya mwisho kwenye gari akimzungumzia John!
Muuguzi akaingia!

“Umeamka?” muuguzi aliuliza huku akionyesha tabasamu dogo akiwa amesimama kando ya kitanda alicholalia Dina.

Dina hakujibu, kumbukumbu iliyomrejea ikaanza kumtoa machozi. Muuguzi akaingia kwenye kazi ya kubembeleza. Juhudi zake zikafanikiwa kumtuliza Dina asilie kwa sauti, lakini aliendelea kutokwa na machozi. Ghafla akataka kijiinua, akajilazimisha kujizoa zoa huku akionekana kukosa nguvu.

“Unataka kwenda wapi?” muuguzi alimwuliza.
“Nataka kukaa,” Dina alijibu.

Muuguzi akamsaidia kumuinua, Dina akakaa kitandani na miguu yake ikaning’inia bila ya kukanyaga sakafuni. Baada ya kukaa, akabaki kimya.

“Unajisikiaje?” muuguzi aliuliza baada ya kumwona Dina yuko kimya. “Naomba unipeleke nikamwone!” Dina alisema bila ya kufafanua. Muuguzi akajua alichokimaanisha Dina.

Taarifa za kujinyonga kwa John zilikuwa zikijulikana na baadhi ya wauguzi, mmoja wa wauguzi hao alikuwa ni huyo anayemuuguza Dina kwenye chumba cha mapumziko ambaye pia alishiriki kumtoa Dina kutoka kwenye gari alipokuwa amezirai. Muuguzi huyo pia, alikuwa na taarifa zilizomjulisha kuwa, Dina ana

mahusiano na John ingawa hakuujua kwa undani uhusiano wao ulikuwa ni wa aina gani. Hivyo, kauli hiyo ya Dina kutaka kwenda kumwona anayetaka kumwona akawa ameielewa vizuri kuwa, Dina alikuwa akitaka apelekwe chumba cha maiti kumwona John!

“Mimi sina mamlaka ya kukupeleka,” muuguzi alimwambia Dina. “Msubiri daktari akija umfahamishe, yeye ndiye mwenye mamlaka ya kukupeleka.”

Dina hakujibu. Alizubaa na kutulia bila ya kutikisika sehemu yoyote ya mwili wake, hakuonekana hata kupepesa macho yake. Muuguzi akabaki ameshangaa.

“Hivi ni kweli John amekufa?” Dina aliuliza na kuonekana kama amerudi ghafla kwenye uhai.

Swali hilo likamuweka muuguzi kwenye wakati mgumu. Akasita kujibu baada ya kukiri swali hilo lilikuwa limemchanganya. Lilikuwa gumu kulitolea jibu la haraka. “Kwani wewe wamekwambiaje?” naye aliuliza.

“Nasikia amejinyo…” Dina hakuimaliza kauli yake, shingo yake ikalegea na macho yake kujipindua tena. Akaangukia ubavu!

Muuguzi akawahi kumdaka Dina kabla hajaangukia chini kutoka kitandani. Akamlaza vizuri na kuirudisha miguu yake kitandani. Akajaribu kumtingisha huku akimuita. Baada ya kuona hakuna dalili yoyote ya kuitikiwa, akaamua kutoka mle chumbani kwa mwendo wa kasi, akaenda kumuita daktari!

* * * * *

Mohsen aliwasili ofisini asubuhi, alikuwa bado akiendelea na majonzi ya kumkosa Dina tokea alivyoondoka kwenda Arusha na alikuwa akiendelea kuumizwa na wivu kwa kujua yuko na Richard. Lile Jinamizi la kumkumbusha vitendo vya kimapenzi alivyokuwa akifanya na Dina wakiwa humo ofisini lilikuwa likiendelea kumtesa. Alikuwa bado akimwona Dina kama vile yuko naye humo ofisini. Alijihisi kama anayechanganyikiwa kadri siku zilivyokuwa zikienda. Mazoea ya uwepo wao wa pamoja kwenye mapenzi ya muda mfupi yalimtesa kana kwamba alikuwa kwenye mapenzi ya muda mrefu na msichana huyo.

Pamoja na kuwa kwenye hali hiyo, lakini kila alipokuwa akimfikiria Dina ndivyo alivyokuwa akijilaumu kwa hatua aliyoichukua ya kumfuata John na kumbwagia mambo ambayo alikiri hayakupaswa kujulikana na John kupitia kwake. Tukio hilo lilikuwa likimkosesha amani baada ya kujiona alikuwa amekosea kuchukua hatua kama hiyo. Kitendo hicho kikamuweka kwenye mashaka kuwa, yote aliyokuwa amemweleza John yangeweza kumfikia Dina. Uwezekano wa John kwenda kumweleza Dina na kisha kulitaja jina lake kuwa ndiye aliyemwambia, aliuona upo. Fikra hizo zikawa eneo jipya lililomkosesha amani kwa muda wote, hasa pale alipojiona angeonekana mshamba wa mapenzi na mwanamume mmbeya!

Hofu hiyo ilimtia kwenye kiwingu kizito, iliyomwingizia majuto na kukiri upuuzi huo aliufanya kwa sababu ya wivu wa kijinga! Fikra hizo za kukiri uhayawani wake zilimuweka kwenye wakati mgumu, ugumu ambao ulimjengea uhakika wa kuja kumgharimu kwa gharama kubwa siku chache zijazo. Kwanza alikuwa na hakika ya kumpoteza Dina kama mpenzi wake ambaye tayari alikwishajikita moyoni mwake. Akakiri hilo litakuwa ni pigo kubwa kwake na kumfanya aanze kuhisi kama vile hakutakuwa na maisha mengine ikiwa atamkosa Dina. Lakini pia, kitendo hicho cha kupeleka umbeya kwa John alikiri kinaweza kumgharimu

kwenye kazi yake! Alikuwa na uhakika Dina angeshikwa na hasira na angemshukia kama Mwewe na hatimaye angemshitaki kwa Richard! Richard angekuwa amepata sababu ya kumfukuza kazi!

Akiwa kwenye lindi la mawazo asubuhi hiyo humo ofisini kwake huku akiwaza jinsi atakavyompoteza Dina na kuipoteza kazi yake, Mohsein alijikuta akipata wazo jipya. Wazo la kutaka kurudi tena kwa John, safari hii kwa ajili ya kumpigia magoti! Alipanga aende kumsihi na kumrai asije akamtaja kwa Dina kuwa ni yeye ndiye aliyeyazungumza maneno hayo. Hiyo ndio aliiona njia pekee ya kuweza kumuokoa asikumbane na adhabu hizo mbili.

Akapanga muda wa kumfuata John kazini kwake. Akaona ni vyema kuitumia nafasi ya ruhusa ya mchana inayotumika kwa ajili ya wafanyakazi kwenda kula, aitumie kwenda kumwona John! Akajiandaa kujipanga namna ya kumkabili kwa mara nyingine ya pili.

Ikiwa imebaki saa moja na ushee muda wa mapumziko kwa ajili ya chakula cha mchana ufike, taarifa za msiba zikaja hapo kazini, taarifa zilizowashitua wafanyakazi wote wa kampuni hiyo.

Lilikuwa tangazo la kufariki kwa Richard!

* * * * *

Kifo cha Richard kilileta hisia tofauti kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo. Wapo waliofurahia kifo hicho kutokana na ujivuni aliokuwa nao kijana huyo wakati wa uhai wake, wakazificha furaha zao na kuunganika kwenye majonzi. Lakini pia walikuwepo walioguswa na kifo hicho kwa kukiri kuwa walikuwa wamempoteza mtu wanayemjua ambaye ni mfanyakazi mwenzao na huzuni ziliwagusa zaidi kwa kumwona Richard amefariki akiwa bado ni kinda.

Mohsein yeye alikifurahia kwa sababu Richard alishakuwa adui yake, akakichukulia kifo hicho kwamba kitakuwa kimeondoa moja ya adhabu mbili alizokuwa akizifikiria. Adhabu ya kufukuzwa kazi na Richard! Pamoja na kufurahia kwa upande huo, lakini upande wa pili ndio uliomfurahisha zaidi. Kifo cha Richard kingemuwezesha kulifaidi penzi la Dina kwa wakati mwafaka, na ili kuliwezesha hilo, alitakiwa kumkabili John hata kama ni kwa kutumia vitisho, kuhakikisha hathubutu kumwambia Dina kwamba yeye aliupeleka umbeya kwake!

Taarifa endelevu za kifo cha Richard ziliendelea kuwasili kwa namna tofauti hapo kazini. Taarifa nyingine zikaletwa kuwa, mzee Ken na mama yake Richard wanaondoka kwa ndege kuelekea Arusha asubuhi hiyo.

Baadaye zikaja taarifa za kipolisi kuwa, Richard aliuawa kwa kupigwa kisu kwenye ugomvi unaosadikika ulitokana na wivu wa mapenzi wa kumgombania mwanamke, lakini hazikumtaja mwanamke mwenyewe. Hatimaye zikaja taarifa zenye mshituko zilizoeleza, polisi walikuwa wamethibitisha ugomvi uliosababisha kifo cha Richard ulimhusisha mume mtarajiwa wa mfanyakazi mwenzake Richard anayeitwa Dina Nzasa, aliyetambulika kwa jina la John Sailas ambaye baada ya tukio la kumpiga kisu Richard aliamua kuchukua uamuzi wa kujinyonga akiwa kwenye chumba cha hoteli aliyokuwa amefikia. Inasemekana John kabla ya kujinyonga aliacha barua yenye maelezo yake na polisi wamelithibitisha hilo kwa kusema kuwa, wanamtafuta mtu mmoja aliyetajwa kwenye barua hiyo kuwa ndiye anayeaminika ni chanzo cha ugomvi huo. Polisi imekataa kulitaja jina la mtuhumiwa huyo kwa sababu za kiusalama.

Taarifa hizo zikawa si njema kwa Mohsein! Kwanza hakuamini kama John alikwenda Arusha na moja kwa moja akatambua kilichompeleka John Arusha ni zile taarifa alizokuwa amempelekea. Msala! aliwaza. Akajua mambo yamekwisha kuharibika na hofu yake ikawa ni barua iliyoachwa na John ambayo iko mikononi mwa polisi. Akawa na uhakika polisi watakuwa wakimtafuta yeye kwa kuamini barua hiyo itakuwa imelitaja jina lake! Mohsein akawa amechanganyikiwa. Akapata wazo la kutoroka kabla ya polisi hawajafika hapo ofisini kumkamata!

Akatoka ofisini kwake, akawaaga wafanyakazi wenzake aliokutana nao kwenye korido kuwa anakwenda kula chakula cha mchana.

Hakurudi tena kazini!

Siku ya pili asubuhi wakati wafanyakazi wakiwa kazini na wengine wakifuatilia mipango ya kuwasili kwa mwili wa Richard ambao taarifa za awali zilisema ungewasili kwa ndege siku inayofuata, ilipofika alasiri ya siku hiyo, taarifa nyingine za msiba zikawasili.

Alikuwa Mohsein!

Taarifa hizo zilipokewa kama mchezo wa kuigiza usiokubalika, hakuwepo aliyekuwa tayari kuziamini, hasa baada ya taarifa hizo kudai, Mohsein alikutwa chumbani kwake akiwa amejinyonga na kuacha ujumbe mfupi kwenye barua iliyoandikwa:

Wivu umeniponza!

Mohsein.

MISA

MISA ya kumwombea John Sailas ilifanyika kwenye Kanisa Katoliki la Kimara Baruti baada ya siku ya arobaini tokea alipozikwa kwenye makaburi ya Kimara. Baada ya misa hiyo, wafiwa walikwenda makaburini kwa ajili ya kupanda Msalaba na kuweka mashada ya maua kwenye kaburi lake. Mmoja wa walioweka mashada hayo alikuwa ni Dina ambaye baada ya kuweka, akahisi hatia kwenye nafsi yake. Machozi yakaanza kumtoka na kilio cha kimya kimya kikafuata.
Ikabidi apewe msaada wa kuondolewa!

* * * * *

Misa ya Richard ilifanyika siku nne tokea misa ya John ilipofanyika. Misa yake ilifanyika kwenye Kanisa la Mtakatifu Peter lililopo Oysterbay. Dina alihudhuria misa hiyo akiongozana na wazazi wake, na wakati walipokuwa wakitoka Kanisani ili kujiandaa kwenda kwenye makaburi ya Kinondoni alipozikwa Richard kwa ajili ya kupanda Msalaba, Dina akasikia akiitwa. Ilikuwa sauti ya kike iliyotoka nyuma yake ikimuita kwa jina lake. Alipogeuka akamwona Judi aliyekuwa ameandamana na kijana mmoja wa kiume.

“Hai Judi!” Dina alisema na kusimama.

Ilikuwa ni mara yao ya pili kuonana tokea walivyoonana kwa mara ya mwisho walipokutana kwenye msiba wa Richard.

“Kutana na mchumba wangu,” Judi alimwambia Dina.
“Anaitwa Martin,”

“Nafurahi kukufahamu,” Dina alisema huku akimpa mkono Martin. Kisha Judi akamtambulisha Martin kwa Dina.
“Martin, kutana na Dina, tulisoma pamoja kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwenye shule ya Sekondari ya Jangwani.”

Martin aliyekuwa bado akiliendeleza tabasamu lake akasema, “Nami nafurahi kukufahamu.”

Baada ya Dina na Martin kusalimiana, Judi aliufungua mkoba wake na kutoa bahasha, akampa Dina.

“Nilihisi tungeonana huku Kanisani,” Judi alisema.
“Nikapata wazo la kuja nayo hii kadi ili nikikuona nikupe. Mungu naye ametuwezesha tumeonana.”

Dina aliipokea kadi aliyopewa ambayo ilikuwa ndani ya bahasha na kusema, “Ahsante.” Hakuhoji ni ya nini kwa sababu angeifungua na kuisoma baadaye.

Wakaagana.

Akiwa kwenye gari ndogo amekaa nyuma pamoja na mama yake huku baba yake akiwa amekaa mbele na dereva, Dina aliifungua bahasha aliyopewa na Judi, akaichomoa kadi na kuisoma. Akagundua ilikuwa ni kadi ya mwaliko inayomwalika ahudhurie sherehe ya kufunga ndoa kati ya Judi na Martin!

Mchomo mkali ukapita na kuuchana moyo wa Dina, akaacha kuendelea kuisoma kadi hiyo, akaamua kuangalia nje ambako watu wachache walikuwa wakitembea kando ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na wakati huohuo magari waliyokuwa wakipishana nayo yalisikika yakitoa mivumo ya kasi ya mwendo. Macho ya Dina yalikuwa yamegubikwa na machozi yaliyomnyima nafasi ya kukiangalia kinachotokea barabarani.

Upepo uliokuwa ukiingia kupitia dirisha lililokuwa upande aliokaa Dina uliyapeperusha machozi na kuyasambaza kwenye ncha za macho yake wakati gari hilo likiwa kwenye mwendo.

Akajifuta machozi ya upande mmoja wa jicho lake kwa kutumia kiganja cha mkono wake.